Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA NNE

## MAJADILIANO YA BUNGE

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 29 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilipata vikaratasi na wengine walinifuata ofisini kuulizia Spika yupo wapi. Kwa taarifa tu ni kwamba natoa nafasi kwanza kama mlivyoona Wenyeviti ili na wao waweze kuzoea kiti hiki. Napenda basi kwa sababu nilikuwa nikiwaona kule ofisini sipo mbali sana na shughuli zote naziona katika chombo maalum.

Nawapongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Ndugai, Wenyeviti wetu waliendesha vizuri sana shughuli humu kwenye Ukumbi wa Bunge, kama mlivyoshuhudia.

Kuna Waheshimiwa Wabunge walijaribu kama kutegeshea kidogo kushtua kama labda watakwama kwenye Kanuni, lakini kama mlivyoona waliweza kutegua yote na tukaendelea na shughuli vizuri. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Simtaji Naibu Spika, kwa sababu yeye kama kawaida mambo yake safi sana, kwa hiyo pia nashukuru sana. Lakini la pili nafanya hivi ili kuniwezesha kukabili kazi za ofisini. Nikikaa muda wote hapa kuna mambo yenu mengine yanaweza yakakwama.

Kwa hiyo, nimeweza kufanya yote. Jana tumekuwa na Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Bunge na limeenda vizuri sana, wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge wameahidi kuwahudumia kwa viwango vya hali ya juu zaidi kuliko wakati wowote. Kwa hiyo, ni vyema mkapata taarifa hiyo nzuri ya wafanyakazi. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 107

**Kuhusu Ujenzi wa Minara ya *VODACOM***

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. MOHAMED H. MISANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kulikuwa na Mradi wa *VODACOM* wa kuwawezesha wananchi wanaosafiri kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kupitia Singida kuwasilliana wakati wote wa safari kupitia mtandao huo ambapo minara ya simu ilijengwa kutoka Dar es Salaam – Dodoma-Manyoni na mnara wa mwisho kujengwa Isuna:-

(a) Je, Mradi huo utaendelezwa lini kwa kujenga minara mingine kuanzia Ikungi, Puma hadi Mwanza ili kuwawezesha wasafiri kuwa na mawasiliano njia nzima?

(b) Je, ni lini mnara utajengwa Makingu ili kuwawezesha wananchi wa Makingu na Misughaa kupata mawasiliano ya simu za mkononi jambo litakalosaidia utekelezaji wa MKUKUTA?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombuni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Awamu ya kwanza ilikuwa ni kujenga njia za simu (*transmission links*) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kupitia mikoa ya katikati mwa nchi ikiwamo Singida. Sambamba na kuweka njia za simu *VODACOM* ilifanikiwa pia kuweka mawasiliano ya *GSM* katika kila mnara uliojengwa na maeneo mbalimbali yalipata na yanaendelea kupata mtandao huu wa *VODACOM*.

Hivi sasa *VODACOM* wanaendelea na kazi ya kufanya tathmini katika maeneo yote yaliyomo ndani ya njia hiyo ambayo hayana mawasiliano. Maeneo yatakayoonyesha kuvutia kwa kukidhi vigezo vya kibiashara yatawekwa kwenye programu ya kutekelezwa mapema iwezekanavyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maeneo ya Makingu, *VODACOM* wamepanga kuyatembelea ili yafanyiwe tathmini. Kazi hii itafanyika kabla ya mwisho wa mwaka huu. Matokeo ya tathmini yakibaini kuwa maeneo hao yanakidhi vigezo vya kampuni, yatawekwa kwenye programu ya utekelezaji mwakani.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, *VODACOM* tayari wameshaweka mnara wa simu Ndago sasa ni lini wataweka Iguguno na Sepuka?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imekuwa inatoa ahadi humu ndani na iliahidi kujenga mnara wa simu eneo la Nkungi Iramba Mashariki, kazi hiyo itafanyika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kumaliza kujenga minara maeneo ambayo ameyataja *VODACOM* itaendelea kutoa huduma katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, pili napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi wa Wizara ya Miundombinu yoyote ni mtoa huduma wa simu anapofika katika maeneo hupenda tu atoe huduma hizo.

Kwa hiyo, ukiacha *VODACOM*, *TIGO* ambayo zamani tukiita *BUZZ* imepanga kujenga mnara kule Ikungi Septemba 2006 na nategemea Septemba 2006 watakuwa na *full coverage* kule Ikungi. Puma na Makingu itapata *weak signal* lakini wanategemea mwakani watapata *full coverage*. *CELTEL* wamepanga na wao vile vile. Makingu na Misughaa *sites* tayari zimeshawekwa katika mpango wao wa mwaka huu na tayari wanafanya *field marketing survey* wakimaliza hapo shughuli za mawasiliano zitaboreshwa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilitoa maelekezo kwa Makampuni ya Simu kwamba wachangie minara ili kurahisisha mawasiliano na kupunguza gharama katika programu zao za kazi. Je, Serikali ni sababu zipi Kampuni hizi zinakaidi maelekezo haya? Au tutunge sheria iwe ni sheria kabisa ili waweze kutekeleza vizuri? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika**,** ni kweli masuala yaku-*share* minara ni wazo ambalo mmelitoa na linafanyiwa kazi. Hivi sasa wenzetu ambao wanatoa huduma za simu wanashirikiana sana katika sehemu mbalimbali anayeweka mnara mwingine anaweka vifaa vyake. Lakini napenda tu ikumbukwe si kila mmoja ana mpango ule ule wa biashara kama mwenzake. Mwingine anaweza akasema napanga kwenda kaskazini mwingine akasema napanga kwenda kusini. Katika hilo anayewahi mwanzo anayekuja mwisho ana-*share* mnara.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa vile barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Zambia na Malawi ni muhimu sana kuwa na mawasiliano na mara nyingi ajali zinatokea. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka simu za mkononi kati ya Mikumi - Iringa mpaka Ilula ambapo kuna simu za *CELTEL?*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika**,** nakubaliana naye kuna umuhimu wa kuweka mawasiliano ya simu

kati ya Dar es Salaam mpakani mwa Zambia kwa ajili ya huduma za mawasiliano na simu. Hivi sasa huduma za mawasiliano ya simu kati ya Dar es Salaam kwenda Tanga, Dar es Salaam kwenda Arusha, kati ya Dar es Salaam kuja Dodoma ni nzuri. Naomba awe na subira hatua kwa hatua Makampuni hayo yataboresha mitandao yao.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ili kuondoa shauku ya kuangalia angalia au ni nani. Kwa kawaida naomba nipate majina ya wageni kabla ya kipindi cha maswali. Lakini pia kwa sababu bado hatujazoea naona bado niendelee kuwa na huruma na suala hili niweze kuwatambulisha sasa wafuatao.

Kwenye *Gallery* mkono wa kushoto tuna bahati ya kuwa na Mama Mzazi wa Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Mama ningeomba usimame Bunge liweze kukutambua. Ahsante, karibu sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi ana wageni wake ambao ni Wajumbe wa Bodi ya Utalii Tanzania, wapo hapa kuhudhuria Kikao cha Bodi ya *TTB.* Ningeomba wasimame pale walipo. Ahsanteni sana. Tunawatakia kikao chenye mafanikio kwa faida ya Taifa letu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Kilosa na Naibu Waziri wa Fedha anao Madiwani saba kutoka Halmashauri ya Kilosa sikuambiwa wako upande gani. Naomba wasimame. Aah hawa hapa kwenye *Speaker's Gallery*. *(Makofi)*

Kuna tangazo hapa kwamba mkisikia harufu fulani hapa jengo limefanyiwa *fumigation* kuua mbu na wadudu wengine katika sehemu hii. Tunaendelea. *(Makofi)*

Na. 108

**Kuhusu Matatizo ya Mawasiliano ya *VODACOM* Tarafa ya Makambako**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni ya Simu ya *VODACOM* imefanya utafiti kuhusu matatizo ya mawasiliano ya simu katika eneo la Tarafa za Makambako na Lupembe – Njombe:-

Je, Serikali kupitia kwa Kampuni ya *VODACOM* inachukua hatua gani ili kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Muvangila Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Hatua zenye lengo la kuboresha huduma za mawasiliano zitolewazo na *VODACOM* zimechukuliwa na utekelezaji wake utakuwa na sehemu mbili. Sehemu ya

kwanza, mawasilliano yataboreshwa mara tu mtambo uliojengwa eneo la Kifanya utakapoanza kufanya kazi.

Sehemu ya pili ya hatua za kuboresha mawasiliano ni mpango uliopo wa kujenga mtambo mpya katika eneo la Matembwe. Mpango huu unatarajiwa kutekelezwa mwakani. Serikali inawaomba wananchi wa maeneo yaliyotajwa waendelee kuvuta subira wakati tatizo hili llinashughulikiwa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Naipongeza Kampuni ya *VODACOM, CELTEL* na *TIGO* na vile vile Serikali katika uwanja huu wa kuboresha mawasiliano nchini. Katika Reli ya Kati hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kama yalivyo katika hizo barabara za kutoka Dar es Salaam, Arusha, Moshi. Napendekeza Serikali kupitia Makampuni haya vile vile wawawezeshe wanaosafiri kwa Reli katika Reli ya Kati wawe na mawasiliano ya moja kwa moja?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa Reli ya Kati tayari tumeanza kuweka *transmission links microwave bank* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, Morogoro hadi Dodoma na sasa tunaendelea na Tabora. Kwa hiyo, vituo vyote ambavyo vina vituo vya reli mawasiliano ya simu yako na ni mazuri kabisa na hatua kwa hatua tutafika Mwanza na sehemu nyingine.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa yapo maeneo yenye minara ya simu za mikononi hayapati mawasiliano. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kushirikiana na Mashirika haya kuona ni sababu gani za msingi ambazo zinafanya maeneo yenye minara ya simu lakini mawasiliano hayapo. Kwa mfano *Area D* kwenye Maghorofa ya *Site Two* nyumba nyingi hazipati mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba inawezekana mnara ulioko hapo na simu yako ni tofauti katika masuala ya mtandao. Lakini Serikali tutaendelea kuwashawishi wawekezaji waweze kuendelea kuboresha huduma zao ili katika maghorofa na maeneo mengine mawasiliano ya simu yaboreke na wananchi wanafaike.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika Mkoa wa Ruvuma Wilaya pekee ya Namtumbo ndiyo haina mawasiliano ya simu za mkononi na *VODACOM* walishawahi kuja kufanya *preliminary*

*surveying* lakini hawajarudi tena. Je, Serikali inaweza ikawashawisha waweze kuja haraka kutuwekea mitambo ya simu za mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuwaomba *VODACOM* watueleze ni kwa nini tu kwa sababu inawezekana vigezo vyao baada ya kufanya *survey* havikidhi mahitaji yao. Lakini tutawashughulikia. Lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge *Ruvuma TTCL* itafika na kule wameomba katika huu mradi wa sasa wa *CDMA* watafika Litembo, Liuli, Namtumbo, *Mbambabay* na Songea Mjini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge mawasiliano yako njiani. (*Makofi)*

Na. 109

**Watu Wanaochomwa Moto kwa Tuhuma za Ujambazi**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuishi ni haki ya msingi ya kila mtu na Katiba ya Nchi inahimiza utu wa mtu uheshimiwe:_

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watu wanaowaua na kuwachoma moto wenzao kwa tuhuma za ujambazi?

(b) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge sababu zilizowafikisha raia kwenye hatua hiyo ya kujichukulia sheria mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge (Biharamulo) kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahimiza utu wa mtu uheshimiwe. Kikatiba kila mtu anayetuhumiwa kutenda kosa lolote la jinai anapaswa kuhukumiwa na Mahakama kwa mujibu wa sheria na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali huchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watu wanaowaua na kuchoma moto wenzao kwa tuhuma za ujambazi. Pale matukio ya aina hiyo yanapotokea huchukuliwa kuwa ni makosa ya jinai hivyo sheria huchukua mkondo wake kwa kuwasaka na kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa wa makosa hayo ili wahukumiwe na Mahakama kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya mauaji au uchomaji moto wa watuhumiwa wa ujambazi unaofanywa na wananchi wanaojiita wenye hasira kali, vinatokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni kukosa uelewa wa sheria za nchi, haki za binadamu, taratibu za uendeshaji wa kesi Mahakamani (*judicial process*). Sababu nyingine ni taratibu hizo

kuonekana kuwa ngumu. Inawezekana pia vitendo hivyo vinatokana na wananchi kukosa imani kwa vyombo vya dola vyenye dhamana ya kutoa haki. Serikali inatoa wito kwa wananchi kuwa wawe wavumilivu wanapowakamata watuhumiwa na kutojichukulia sheria mikononi ili vyombo vya sheria vifanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwakumbusha wananchi kwamba, hata wakiwa na hasira kali kiasi gani kitendo cha kumchoma moto mtu ni kosa la jinai.

**MHE PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa mauaji na uchomaji moto wa binadamu umeanza muda mrefu Mheshimiwa Waziri anaweza akaniambia ni wangapi wameshakamatwa na kuadhibiwa.

Pili, kwa kuwa amesema kwamba kwa kweli haki ya kuishi ni ya kila binadamu anaweza akalihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi kila mauaji yatakapokuwa yanatendeka yawe yamefanywa na Polisi au hawa watu wenye hasira kali watafuatiliwa ili kuona mazingira gani yaliyosababisha binadamu kupoteza maisha ?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba makosa haya ya uchomaji moto yamekuwa yakitokea kwa muda mrefu sasa. Lakini yamekuwa yanachukuliwa makosa ya jinai ya kawaida ya mauaji.

Labda tu ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi watendaji wa makosa haya ya mauaji ni karibu asilimia 30 ndio wako magerezani. Ni vigumu kujua kama mauaji hayo ni kwa kuchoma moto au kupiga risasi au kwa makosa mengine.

Ninachotaka kusema ni kuwaomba wananchi kwamba tabia hii ya kuchoma wenzetu moto kwa makosa yoyote yale au kujichukulia sheria mikononi ni makosa ya jinai. Ni lazima Serikali iwaombe wananchi sasa waache tabia hizo wafuate sheria na Serikali iko hapa kuwahudumia wao. Nashukuru sana.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niongeze swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa huko nyuma mauaji haya yalikuwa yanafanyika zaidi mijini na kwa kuwa hali hii sasa imefika mpaka vijijini. Waziri amekiri kwamba moja ya sababu ni wananchi kupoteza imani na vyombo vya dola. Waziri atatuhakikishia vipi Serikali inachukua hatua ili wananchi waanze kupata sasa imani tena na vyombo vya dola wakati hao ndio wanaosababisha hasira hiyo kali?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa hivi makosa haya yanatendeka mijini na vijijini. Lakini hii ni *concept* ya *mob justice* ni kitendo kinachotokea *symptomatically* ni vigumu kusema ni nani amekianzisha. *Mob* ni *mob* sasa inatokea vijijini na mijini kweli. Ni zile hasira wananchi wanazozipata. Ni jukumu letu kuelimisha wananchi kwamba zipo sheria na wazifuate sheria. Sasa hivi Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inatoa mafunzo kwa wananchi kujua haki zao na taratibu za kisheria.

Naomba tusikilize vipindi hivyo vya redio na televisheni ili wananchi waendelee kujifunza. *NGO* mbalimbali zinaendelea kutoa huduma hii na elimu hii kwa wananchi ili wananchi wazijue sheria na wazizingatie.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Ni kweli kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ni jukumu letu sisi kama jamii kuwaelimisha wananchi. Lakini Serikali haioni kwamba wananchi wanachukua sheria mkononi kwa sababu kwa kufuata historia mhalifu anakamatwa anafikishwa Polisi, lakini kabla mtu aliyemfikisha Polisi hajarudi nyumbani huyo mtu aliyepelekwa Polisi tayari amesharudi nyumbani. Ameachiwa na polisi.

Kwa hiyo, wananchi wanaona kumbe hakuna haja ya kumpeleka mhalifu Polisi ndiyo, maana wanachukua sheria mkononi. Japokuwa si vizuri kuchukua sheria hiyo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Vile vile nimefurahi Waheshimiwa Wabunge wanapouliza maswali ili Serikali ichukue hatua madhubuti.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu yoyote ya kumruhusu mwananchi yoyote kuchukua sheria mkononi. Lakini hapo hapo napenda kuwahakikishia wananchi na Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako Tukufu kwamba vyombo vya dola vitahakikisha vinawajibika kuchukua majukumu yao ipasavyo ili wananchii waendelee kuwa na imani na vyombo hivyo.

Lakini narudia tena hakuna sababu yoyote kwa mwananchi yoyote wa Tanzania awe ni mmoja au katika vikundi kuchukua sheria mikononi kwa sababu Serikali itachukua sheria kwa wale ambao watafanya hivyo.

Na. 110

**Magari Mabovu Mijini**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya magari nchini ni mabovu sana na mengine yakitembea yanatoa moshi mzito ambao unaharibu mazingira na kwa kiasi fulani husababisha maradhi ya kansa:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika muda muafaka wa kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Viti Malum, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Chaurembo kwamba ni kweli baadhi ya magari nchini ni mabovu sana na mengine yakitembea yanatoa moshi mzito ambao unaharibu mazingira na kuweza kusababisha maradhi.

Mheshimiwa Spika, magari yote nchini husajiliwa na kuruhusiwa kutembea katika barabara zetu kwa kufuata sheria zilizowekwa na Bunge lako Tukufu na Kanuni zitokanazo na sheria hizo. Sheria za Kudhibiti Ubora wa Magari zimeainishwa katika Sheria ya Usalama Barabarani Namba 30 ya mwaka 1973.

Mheshimiwa Spika, Mfumo mpya wa usajili wa magari nchini umeweka sharti linalomtaka mwenye kuomba kusajili gari kuonyesha kuwa gari husika limekaguliwa na vyombo vyenye dhamana ya ukaguzi vya Usalama Barabarani na kuthibitika kuwa linakidhi ubora wa kuwepo barabarani.

Endapo gari halikidhi ubora kwa mujibu wa Sheria za Usalama Barabarani basi gari husika haliruhusiwi kusajiliwa na kuwepo barabarani mpaka hapo litakapofanyiwa matengenezo yanayotakiwa. Kwa sasa tunaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali hususan vyombo vya usalama barabarani na taasisi za huduma na usimamizi wa vyombo vya usafiri ili kudhibiti matumizi ya magari machakavu na mabovu barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vile vile kwa kuhusisha ukaguzi wa viwango vya magari tumeongeza uwezekano wa kuwepo kwa udhibiti wa uingizaji wa magari hapa nchini ili kutoruhusu uingizaji wa magari mabovu na machakavu kwa nia ya kulinda mazingira na vile vile kuepuka athari zingine zinazoweza kusababishwa na matumizi ya magari mabovu. *(Makofi)*

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amekubaliana na mimi kwamba magari mabovu yako mengi nchini na magari mengine hutoa moshi mwingi na kuathiri mazingira. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri. Je, Waziri atawathibitishia wananchi kwamba Serikali iko tayari sasa kuzuia magari ambayo yanatoa moshi mwingi yasitembee tena barabarani?

Pili, kwa kuwa *Oil* chafu ikidondoka katika ardhi majani yanakuwa hayaoti tena na kwa kuwa *oil* chafu ikiwekwa vizuri inasaidia *wood treatment.*

Je, Serikali itawasaidia vipi watu wa *garage* katika kuhifahi *oil* chafu ili kusaidia katika *wood treatment* na kutokuharibu mazingira? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na nimesema katika jibu langu la awali kwamba Serikali kwa kushirikiana na wadau wote. Tunaandaa mpango wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na mikakati madhubuti kuhakisha kwamba magari mabovu ama hayaingizwi nchini na kama yameingizwa basi yanafanyiwa tathimini na kama yanamatatizo yatengenezwe kabla hayajaruhusiwa kuingia barabarani. *(Makofi)*

Kuhusu suala la pili, tumekubaliana kwamba Naibu Waziri wa Usalama wa Raia atalijibu.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua zitachukuliwa kwa kushirikiana na Wizara husika ili kutafuta ufumbuzi wa suala alilouliza. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tutafute ufumbuzi muafaka ili tuondoe tatizo hili.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upande wa Serikali wamekiri kwamba hili ni tatizo, na kwa kuwa umri wa gari unaweza kuwa ni mojawapo ya vigezo vinavyoweza kutumika. Je, Serikali katika kuchunguza jambo hili itazingatia umri wa gari linapoagizwa kutoka nje badala ya kufikiria kuzitengeneza tu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yale ambayo ameelezwa kabla, Serikali kwa kweli inafuatilia na inazuia magari ambayo yanatoka moshi. Lakini suala la umri wa gari pia Serikali imezingatia na ndiyo maana katika Bajeti ya mwaka huu tumependekeza kwamba asilimia 20 zaidi itolewe kwenye ushuru wa magari yote ambayo yatakuwa zaidi ya miaka kumi. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona leo. Kwa kuwa sababu kubwa ya magari kutoa moshi mzito ni kutokufanyiwa *service* kwa wakati hata kama si bovu hilo gari. Lakini kama halifanyiwi *service* kwa wakati gari hilo litatoka moshi tu. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kufanya uchunguzi mara kwa mara kuhusiana na tatizo hilo la kutokufanyiwa *service* magari? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakubaliana naye. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba kwa kweli sote tunajua kwamba suala la *service*

ni suala la mwenye gari na ni muhimu kabisa kwamba kwa mwenye gari kuhakikisha kwamba gari lake analifanyia *service* ili kuhakikisha kwamba hatoi fedha nyingi zaidi za kununua *spare parts* pale linapoharibika. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa wananchi ambao walinunua magari wahakikishe kwamba *service* zinafanyika na zinafanyika kwa wakati. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nami ningependa kuongezea jibu la Waziri wa Fedha kama ifuatavyo:-

Suala la utunzaji wa mazingira katika barabara liko chini ya Wizara yangu na nitasema kwenye hotuba yangu Jumatatu jinsi nitakavyoshughulikia hili suala la mazingira katika barabara kuu za nchi hii.

**SPIKA.** Waheshimiwa Wabunge ni lazima nikiri kwamba nilikuwa nafanya makosa kutokumtambua Mheshimiwa Faida katika maswali ya nyongeza, kwa sababu kumbe akiuliza swali la nyongeza wanalazimika Mawaziri kadhaa kujaribu kusaidiana kujibu. (*Kicheko*)

Swali linalofuata Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

Na. 111

**Benki ya Greenland Kutoka Uganda**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, miaka ya 1990 Benki Kuu ilitoa kibali kwa Benki ya *Greenland* kutoka Uganda kufanya biashara ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadaye Benki Kuu kusitisha kazi za Benki hiyo:-

(a) Je, ni hasara gani iliyopatikana kutokana na kutoa kibali kwa Benki hiyo kufanya kazi?

(b) Je, ni wananchi wangapi hadi sasa bado hawajalipwa fedha zao zilizohifadhiwa ndani ya Benki hiyo?

(c) Kwa kuwa, kuna wateja wengine walikufa kabla ya kufungwa kwa Benki hiyo na hakukuwa na taarifa za warithi wao. Je, ni kiasi gani cha fedha zao kilichopo hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanguka kwa Benki ya Greenland na kuwekwa chini ya ufilisi hakujaleta hasara yoyote kwa mteja kwani wateja wa benki hiyo ambao ndio wadau wakubwa wamelipwa na wanaendelea hulipwa amana zao pamoja na riba iliyopatikana hadi kipindi benki hiyo ilipowekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu; hivyo hakuna mteja yoyote aliyepoteza au atakayepoteza fedha zake. Aidha, wadai na wadiwa (*debtors and creditors*) wote wanaendelea kushughulikiwa na mfilisi mteule wa benki hiyo chini ya misingi na utaratibu wa kisheria. hadi kufikia 15 Mei mwaka huu asilimia 98 ya wateja walishalipwa ni asilimia mbili tu ambao hawajachukua amana zao. *(Makofi)*

(b)Mheshimiwa Spika, wateja waliolipwa na Meneja Mteule *(Statutory Manager)* na baada ya kumalizika kwa kipindi chake amana zote za wateja zilizobaki zilihamishiwa Benki Kuu. Hivyo wateja ambao hawajalipwa, fedha zao ziko Benki Kuu zinawasubiri.

Mheshimiwa Spika, asilimia mbili ya wateja ambayo ni sawa na jumla ya wateja 3,477 hawajachukua amana zao. Idadi hiyo inajumuisha wateja wa tawi la Dar es Salaam ambao ni 2,925 wenye amana zenye thamani ya shilingi 76,106,515.05 dola za Marekani 51,317.35 na pauni za Uingereza 1,038.98, na wateja wa tawi la Zanzibar ambao ni 552 wenye amana zenye thamani ya shilingi 8,347,266.09 na pauni za Kiingereza 11,517.49. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, jumla ya idadi ya wateja waliofariki haijulikani kwa Mfilisi mteule, bali itakuwa katika jumla ya wale ambao hawajachukua amana zao. Mteja anafahamika kwamba amefariki pindi warithi wake wanapojitambulisha na taratibu za kisheria zinafuatwa kuwalipa warithi hao.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wateja wote wanafika Benki Kuu na kuchukua amana zao, Bodi ya Bima ya Amana *(Deposit Insurance Board)* ambayo ndiyo Mfilisi Mteule imekuwa ikitoa matangazo mara kwa mara kwenye magazeti kuwataka wateja au warithi wa wateja waliofariki kufika Benki Kuu na vitambulisho vyao pamoja na hati za mirathi ili kuchukua amana zao. ninawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao wanataarifa ya wateja ambao hawajalipwa kuwashauri wafike tawi lolote la Benki Kuu ili waelekezwe jinsi gani wanaweza kulipwa amana zao.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa majibu yake fasaha yenye muelekeo wa kupata maslahi kwa wateja wa benki hiyo; nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akalieleza Bunge lako Tukufu ni sababu gani za msingi zilizosababisha kufungwa kwa benki hiyo na sababu hizo zimekumba mabenki katika Tanzania?

La pili, linapotokea suala kama hili katika benki za aina hii na kufungwa je, wahusika wa benki hizi huwa wanatakiwa kulipa fidia yoyote kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)**: Mheshimiwa Spika, moja, tatizo la *Greenland Bank* lilianzia Uganda ambako ndiko benki mama ilikuwepo.

Benki hiyo ilifilisika huko Uganda, baada ya kufilisika, benki iliyokuwepo Tanzania nayenyewe ikapata matatizo. Benki Kuu ilipopata fununu kwamba kuna matatizo ikateua wakaguzi na baada ya kukagua ikadhihirika kwamba benki hiyo iliyokuwepo Tanzania isingeweza kuendelea na shughuli zake za kibenki. Kwa hiyo, Benki Kuu ikaamua kuifunga.

Kuhusu wenye benki uko utaratibu maalum ambao Benki Kuu huwa inachukua. Ikidhihirika kwamba benki imefilisika kwa sababu za ama wizi ama maadili, ziko sheria ambazo Benki Kuu inaweza ikazichukua kuwashughulikia wale wenye benki. Ikiwa tu ni kwamba ni biashara imekwenda kombo pia kuna utaratibu ambao benki huwa inachukua kuwashughulikia wenye benki. *(Makofi)*

**MHE. SILAJI J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Bodi ya Bima za Amana imeweka kiwango cha juu kabisa cha kumlipa mteja shilingi 250,000/- ikiwa benki itafilisika. Kiwango hiki ni kidogo na muda sasa umepita. Je Serikali kupitia Wizara ya Fedha itakubaliana na mimi kwamba iko haja sasa ya kukiongeza kiwango hiki ili benki ikifilisika wateja wasipunjwe sana katika kurudishwa amana zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)**: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kiwango cha shilingi 250,000/=, ambacho kiliwekwa mwaka 1991, sasa hivi ni kidogo. Wizara tukishirikiana na benki tutaangalia namna ya kuboresha kiwango hicho .

Lakini la pili, kama nilivyomjibu mwanzo Tatizo la *Greeland Bank* halikuanzia Tanzania.Tatizo lilikuwa Uganda kwenye benki mama. Kwa hivyo Benki Kuu kwa kuchukua hatua za haraka iliweza kuhakikisha kwamba benki ilikuwa na pesa za kutosha. Kwa hiyo wale wateja wote waliokuwa na amana *Greenland Bank* wamelipwa kwa fedha zilizokuwepo katika Benki Kuu na Serikali haikuwajibika kwa wateja. *(Makofi)*

Na.112

**Wimbi la Ujambazi Karagwe**

**MHE.GOSBERT M. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wimbi la ujambazi Wilayani Karagwe limekuwa ni tatizo la miaka mingi; na kwa kuwa wananchi wa Karagwe siku zote huishi kwa hofu na mashaka ya kuuwawa na kuibiwa mali zao:-

Je, Serikali ina mikakati gani kamambe wa kulinda maisha ya wananchi wa Karagwe na kuhakikisha inakalika kwa amani na utulivu siku zote?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Blandes, kuwa Wilaya ya Karagwe imekumbwa na uhalifu wa aina mbalimbali. Kwa kiasi kikubwa uhalifu huo unachangiwa na wageni na wahamiaji haramu kutokana na mwingiliano mkubwa na raia wa nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, jana asubuhi wakati nikijibu swali Na. 98 la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, nilieleza kwamba Serikali inajali sana usamalama wa maisha ya raia na mali zao, na kwa kutambua hilo, Serikali imeandaa operesheni maalum chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kushughulikia usalama wa raia wetu wanaoishi katika mikoa ya mipakani kwa kushirikisha vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Serikali ilituma ujumbe ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mheshimiwa Halima Kisungu, kwenda Kigali, Rwanda kuzungumza utaratibu wa kuwarejesha wahamiaji haramu ili kudhibiti tatizo ambalo Mheshimiwa Blandes amelizungumzia. Vilevile jitihada hizo zitatekelezwa kwa kuwa na mazungumzo na Serikali za Kongo, Burundi na Uganda.

Mheshimiwa, Spika kama nilivyosema jana, mapambano dhidi ya uhalifu ni jukumu la kila raia mwema kwa ajili ya kulinda nchi yetu. Hivyo kupita Bunge lako Tukufu natoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za wahalifu na kuacha kukumbatia waingiaji na wageni haramu ambao wengi wao ni chanzo cha uhalifu katika maeneo ya mipakani.

**MHE. GOSBERT M. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, na vilevile namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ni kwamba katika eneo la Karagwe lipo pori kubwa sana linaitwa Kimisi na hilo limekuwa kambi kubwa sana ya majambazi na wananchi wa Karagwe wamekuwa wakiomba kituo cha polisi katika pori hilo. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo hicho katika pori hilo?

Mheshimiwa Spika, la pili, Wilaya ya Karagwe ni Wilaya kubwa sana na imekuwa ikipata matatizo ya ujambazi lakini wanatatizo moja, kituo cha polisi kina gari moja la kufanyia *patrol*, gari ambalo halikidhi mahitaji ya polisi Wilaya nzima ya Karagwe. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza magari, pikipiki pamoja na *redio calls*?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ushauri wake Mheshimiwa Blandes tunauchukua na tutaufanyia kazi ili kuhakikisha kwamba hapo kwenye matatizo tutafute mbinu ya kujenga kituo na ikiwa suala la matatizo tutafute

mbinu ya kujenga kituo na ikiwa suala la matatizo tutayapunguza sana kwa kutafuta gari nyingine, tutafanya kila jitihada ili tupate gari katika Wilaya hiyo ya Karagwe.

**MHE. MUSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, vikosi maalum vya polisi vinavyopambana na majambazi vinafanya kazi nzuri sana sasa hivi, lakini *identity* ya askari hawa iko katika mashaka wakati hawafanyi kazi zao wakiwa wanafichwa na nguo maalum za kuficha sura zao ili wasilipiziwe visasi na majambazi. Je, Serikari ina mapango gani sasa hivi wa kuwapatia *masks* maalum vikosi hivi ili visipate kushambuliwa tena na majambazi wakati wa mapumziko?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na ushauri wake mzuri, lakini hata hivyo Serikali katika kipindi cha Bajeti ya mwaka 2006/2007 imetenga fedha maalum kwa ajili ya kununua vifaa vya kinga vya risasi, na hivi ni *bullets proof vest* na *helmet.* Kwa hiyo, suala la *masks* tutaliangalia ili kutafuta ufumbuzi huko mbele.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwa kuwa majambazi wanavyokwenda kufanya uhalifu wao wanaua raia wasiokuwa na hatia. Je Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wanavyowakamata majambazi hawa kuwashitaki na kosa la mauaji?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu ulivyo ni kwamba unapoua unashtakiwa kwa kosa la mauaji, huo ndiyo utaratibu.

Na. 113

**Kufufua Zao la Kahawa na Migomba**

**MHE. AGGREY D. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baada ya kampeni ya muda mrefu iliyoendeshwa na uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro na ule wa Wilaya, Wananchi wengi katika Wilaya ya Siha wameitikia wito wa kufufua zao la kahawa na migomba na kwa kuwa mifereji ya asili iliyopo eneo hilo imeanza kufufuliwa na wananchi wenyewe kwa nguvu zao na moyo wa kujitegemea:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia jitihada hizo za wananchi ili kilimo cha umwagiliaji kiweze kuimarishwa Wilaya ya Siha?

(b) Je, Serikali kupitia huo moyo wa kujitolea wa wananchi wa Siha haioni ni jambo zuri kufufua miferreji ya Nsunga, Nrao, Kisangara, Kiboko, Kyengia, Kashashi na kadhalika, ili kusaidia katika vita ya kupambana na umaskini nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Deaisile Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwanza kwa kuwapongeza wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro hususani wale wa Wilaya ya Siha kwa juhudi ambazo wanazifanya kufufua mazao wa kahawa na migomba na pia kwa kuanza kuifufua mifereji ya asili kwa kujitegemea.

Kwa miaka mingi sana, mazao hayo yamekuwa yanapata maji ya umwagiliaji na kuosha kahawa kwa kutumia mifereji hiyo ya asili maarufu kwa jina la *mifongo*. Kwa sababu mifereji hiyo imetumika kwa muda mrefu na kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji, mingi imechakaa na sasa haikidhi mahitaji ya maji ya kumwagilia. Kwa kutambua hili, Wizara yangu inaweka mkazo katika kukarabati skimu za umwagiliaji maji mashambani zilizochakaa.

Kwa mfano katika mwaka 1986/1987, Serikali ilianzisha mradi wa kukarabati skimu za umwagiliaji za jadi uliyojulikana kama *Rehabilitation of Traditional Irrigation Schemes* katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Uzoefu ulitokana na utekelezaji wa mradi huo ndio unaotumika hivi sasa kukarabati skimu nyingine nchini pamoja na zile za Wilaya ya Siha.

Katika Wilaya ya Siha, Serikali imekuwa inatoa fedha za ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji kama ifuatavyo:-

(i) Katika mwaka wa 2004/2005, kwa kupitia mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (*DADP*) Serikali ilitoa shilingi 8,000,000 kwa ajili ya kukarabati mfereji wa Nangwiriri.

(ii) Katika mwaka wa 2005/2006, Mradi wa *PADEP* umetoa jumla ya shilingi 105,000,000 ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika vijiji vya Koboko Kishisha na Manio.

(iii) Katika mwaka wa 2005/2006 Serikali ilitoa shilingi 6,000,000 ili kukarabati mifereji wa Ndabo.

(iv) Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali ilitoa kupitia *Food Aid Counter Fund*, ilitoa shilingi 148,100,000 kwa ajili ya ukarabati wa skimu ya Msungu.

(v) Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali ilitoa shilingi 15,000, 000 kwa ajili ya ukarabati wa mifereji ya Nrao na Koboko.

Mheshimiwa Spika, nimewaelekeza wataalam wa umwagiliaji katika Kanda ya Kilimanjaro ili waisaidie Wilaya ya Siha kupima na kufanya usanifu wa mifereji yote

ambayo bado haijakarabatiwa ili iingizwe katika mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya wa Siha ikiwa na maandalizi mazuri ya kitaalam. Miradi hiyo itaweza kutafutiwa fedha katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (*DADP's*), *TASAF* na pia kutoka kwenye vyanzo vingine vya fedha.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri najitihada zake ambazo zimeonekana kwamba zimefanyika katika Wilaya yetu ya Siha. Pamoja na jitihada hizo ningeomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba haya maelekezo yaliyotolewa yanaelekeza pia suala la kuweka mabwawa kwa sababu maji yamepungua kwa sababu ya uharibifu wa mazingira.

Pili mifereji ambayo nimeiulizia hapa ni mifereji ambayo sasa hivi tunavyozungumza kuna uharibifu na maji mengi yanapotea. Je, maelekezo hayo ambayo yametolewa yanaelekeza pia kwenda kutengeneza na kukarabati hiyo mifireji kabla ya kuja kwenye huo mpango mkubwa unaozungumzwa hapa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, suala la kujenga mabwawa ni suala linalohitaji uchunguzi. Kama tunavyoelewa Kilimanjaro ni sehemu ambayo ardhi ni ndogo sana. Kwa hiyo, tunapopanga kujenga bwawa lazima tuchunguze kwanza bwawa tukilijenga katika eneo hilo litakuwa na athari kwa maeneo mengine. Inawezekana tukajenga bwawa likaharibu hata mashamba ambayo yalikuwa yanaendelea.

Lakini lengo letu ni kila mahali ambapo tumeweza kujenga bwawa kwa ajili ya kuongeza au kuhifadhi maji tutafanya hivyo. Kwa hiyo, katika eneo hilo kama nako itadhihirika kwamba bwawa litaweza kujengwa hiyo ni dhahiri tutafanya namna hiyo.

Kuhusu maji kupotea, maelekezo ambayo tumetoa kwa ofisi zetu za kanda na wataalam ni kutizama nini kina sababisha mifereji hii kupoteza maji, na wakishabaini sababu matatizo hayo ndivyo ambavyo yatatafutiwa ufumbuzi. Kwa mfano inaweza ikawa mfereji unavujisha maji hayafiki kule yanakokwenda kulingana na kiasi kilichopangwa basi inawezekana ufumbuzi ikawa ni kusakafia mfereji huo.

Kwa hiyo, wataalam watakapofika pale hawatafanya kazi peke yao watashirikiana na wakulima kubaini matatizo na yatakayobainika ndiyo hayo yatakayochukuliwa hatua.

Na. 114

**Ujenzi wa Kiwanda cha Pembejeo za Kilimo**

**MHE. MUHAMMED AMOUR CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya awamu ya nne imekusudia kukuza na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kile cha kawaida:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya pembejeo zote muhimu za kilimo hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ya awamu ya Nne imedhamiria kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Aidha, ni kweli pia kwamba ili kilimo chetu kiwe na tija na kuongeza uzalishaji, ni lazima kuongeza matumizi ya pembejeo hususan mbolea na mbegu bora zilizoboreshwa kibaolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hivyo, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, Sura ya Tatu Kifungu cha 31 (d) kinaelekeza Serikali kama ifuatavyo, nanukuu:

“Mbegu bora na mbolea ni pembejeo zenye umuhimu wa kwanza katika mageuzi ya kilimo na kuongeza tija. CCM katika kipindi cha ilani hii kitazitaka Serikali kuchukua hatua za dhati za kuweka utaratibu wenye uhakika na upatikanaji wa mbegu bora na mboela na kuzifikisha waliko wakulima kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Vyama vya Ushirika na watu binafsi.”

Mheshimiwa Spika, naendelea kunukuu, kinasema: “Aidha utaratibu wa Serikali kutoa ruzuku ya mbolea utaimarishwa na kulenga zaidi kwenye kukuza uzalishaji katika kilimo kuliko manufaa ya kibiashara pekee. Vile vile, kutazamwa uwezekano wa kutoa ruzuku ya mbegu bora ili kuwavutia wakulima wengi zaidi kuzitumia. Serikali itatakiwa kusimamia kwa karibu utekelezaji wa azma ya kurejesha utengenezaji wa mbolea nchini.”

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbolea hapa Tanzania kwa sasa bado ni ya chini sana. Wakulima wanatumia wastani wa kilo 8 za virutubisho vya mimea kwa hekta ikilinganishwa na nchi kama Malawi ambapo wanatumia wastani wa kilo 27 kwa hekta, Afrika ya Kusini kilo 53, India kilo 103 na China kila 279 kwa hekta.

Inapendekezwa matumizi yafikie angalau kilo 59 za virutubisho vya mimea kwa hekta angalau kilo 50 za virutubisho vya mimea kwa hekta ifikapo mwaka 2015 na matumizi ya mbolea yaongezeke kutoka tani 120,000 kwa mwaka hadi kufikia tani milioni moja ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara yangu inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko hatua za makusudi zitachukuliwa kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mbolea nchini mapema iwezekanavyo.

(ii) Kuhamasisha wakulima juu ya matumizi ya minjingu *rock phosphate* ambayo ni *organic* kwa kiasi zaidi.

(iii) Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na nje ya hadi apatikane atakaye wekeza kwa kuanzisha kiwanda cha mbolea.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, viwanda vingi hapa Tanzania huwa vinajengwa Dar es salaam na kilimo hasa kinakuwa mikoani. Je, Serikali iko tayari sasa kuwashawishi au kufanya mipango ya makusudi viwanda hivyo vya mbolea vijengwe katika mikoa ile mitano ambayo ni wazalishaji wakubwa wa mazao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (K. n. y. WAZIRI WA KILIMO):** Mheshimiwa Spika, kweli kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali ina nia ya kuwashawishi wawekezaji kujenga viwanda vya mbolea hapa nchini na tayari pameishakuwepo, tunaweza kusema *incentive*, hamasa ya kuwafanya wafanye hivyo kwa sababu soko limekuwa *guaranteed* kama jinsi tulivyoona kwenye hotuba ya Mheshimwa Zakhia Meghji, katika Bajeti, pesa iliyotengwa kwa ajili ya hiyo mbolea.

Mheshimiwa Spika, sasa, suala la kujenga kiwanda, kuna vigezo mbali mbali ambavyo huwa vinatumika mahali gani mtu anaweza akajenga kiwanda na sana sana huwa ni mahala gani ambapo kuna ile *raw materials*. Mahali ambapo unaweza kupata ile malighafi, na tunaona malighafi ya mbolea sana sana huwa ni gesi, mahala ambapo kuna gesi, mahala ambapo kuana *phosphate*. Sehemu hizo ndizo ambazo unaweza kujenga kiwanda. Kikiishajengeka toka pale, ile mbolea inasafirishwa kokote nchini mahali ambapo inahitajika. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania tumebahatika kwamba tunapata mvua kila mwaka mara mbili au mara tatu. Na kwa kuwa vile vile Tanzania siyo jangwa, sasa ninachokiuliza ni kwamba nchi kama

Misri ambayo inapata mvua mara moja kwa mwaka na nchi yake ni jangwa, Lakini kwa kilimo wametuzidi mara mia moja. Sasa, Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuzifuata nchi kama hizo tukawataka watu wao wakaja angalau watupe njia kama walivyofanya wao?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, siri kubwa ya nchi ya Misri kuwa inazalisha chakula cha kujitosheleza na hata wakati mwingine kuwa na ziada ya mazao hata ya chakula na ya biashara kuuza nchi za nje, ni kwamba wanatekeleza kilimo cha umwagiliaji na utumiaji mkubwa wa mbolea za kemia. Katika Afrika nchi ya Misri ndiyo inayoongoza katika utumiaji wa mbolea za kemia kwa hekta, yaani inazidi nchi nyingine zote. Ndiyo maana na sisi sasa, katika programu ya maendeleo ya sekta kilimo ambayo leo hii mchana huu itapitishwa na Baraza la Mawaziri na katika Bajeti hii ya mwaka huu nitaiwasilisha. Tumezingatia sana kupanua kilimo cha umwagiliaji na pia utumiaji wa mbolea za kemia na mbegu bora. Kwa hiyo, naomba Waheshimwia Wabunge wawe na subira kidogo, tutakapowasilisha Bajeti yetu, nadhani tarehe 5, tutaoa maelezo kwa undani zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunafidia muda ule wa matangazo mwanzoni. Kwa hiyo, tunaendelea na haya maswali mawili ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa William Ngeleja! Mheshimiwa Nyawazwa kwa niaba yake!

Na. 115

**Kiwanda cha Kusindika Muhogo Katunguru**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n. y. MHE. WILLIAM NGELEJA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kufungwa kwa kiwanda cha kusindika mihogo mwaka 1995 kilichokuwa Katunguru Jimboni Sengerema, kuliathiri sana uchumi wa wazalishaji mihogo jimboni Sengerema na waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho:-

(a) Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa Jimbo la Sengerema na Watanzania kwa ujumla sababu zilizopelekea kufungwa kwa kiwanda hicho?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza ni wapi mitambo ya kiwanda cha Katunguru ilipelekwa, na sasa inatumika kwenye kiwanda au shughuli gani?

(c) Je, endapo mitambo ya kiwanda hicho haitumiki kama ilivyokusudiwa huko ilikopelekwa. Je, Serikali iko tayari kuirudisha mitambo hiyo na kufufua kiwanda cha kusindika mihogo Katunguru?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Ngeleja Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa kiwanda cha wanga Sengerema kilichokuwa Katunguru ulikwama kuendelezwa kutokana na ukosefu wa mihogo mibichi ya kutosheleza uzalishaji ambao ndiyo maligahafi kuu.

(b) Mitambo ya kiwanda hicho iliuzwa mwaka 1994 kwa mnunuzi Kampuni ya *Coastal Starch Manufacturing Company Ltd*. Mnunuzi huyo alikuwa apeleke mitambo hiyo Mkoa wa Mtwara.

(c) Kutokana na ukweli kuwa mitambo hiyo ni mali ya kampuni binafsi, Serikali haina uwezo tena wa kuingilia matumizi ya mitambo. Aidha, hali ya uchumi hivi sasa inaendeshwa kwa misingi ya uchumi wa soko huria, ambapo mwekezaji huamua sehemu ya kuwekeza baada ya kuzingatia upatikanaji wa malighafi, miundombinu na matarajio ya kupata faida atakapoendesha shughuli hiyo.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, zao la mhogo katika Mkoa wa Mwanza linalimwa sana, na katika jibu lake la msingi anasema kwamba kutokana na kutokuwa na mihogo ndio maana walihamisha. Haoni kuwa Serikali haikuwatendea haki wakaazi wa Mkoa wa Mwanza kwa kuwahamishia kiwanda chao na kupeleka mkoa mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, utafiti wa kujenga kiwanda ulifanyika mwaka 1979. Kiwanda hicho kilijengwa na kilianza kutumika mwaka mwaka 1984. Uzalishaji ambao ulitegemewa katika kiwanda hicho ni tani 3000 kwa kutumia tani 15,000 za mihogo mibichi. Mwaka 1984, kiasi cha mihogo mibichi kilichokuwa kinapatikana kwa ajili ya kiwanda hicho ni tani 1950 ambazo zilikuwa zinazalisha tani 395 za wanga. Kwa hiyo, ukosefu wa malighafi ndio ulisababisha kwamba kiwanda hicho kifungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ulimbikizaji wa madeni, kwa kuwa kiwanda hicho sasa badala ya kuzalisha tani 3000 za wanga, kilikuwa kinazalisha tani 395, ulimbikizaji wa madeni kutokana na kuendesha kile kiwanda ulikuwa mkubwa kiasi ambacho kiwanda hicho hakikuweza kuendelea. Lakini, vile vile Serikali kwa kupitia Shirika la Viwanda vya dawa, iliwasiliana na Benki ya Uholanzi, wakakubaliana kwamba Benki hiyo ingetoa pesa kwa ajili ya kuweka shamba kubwa la eka 2500 za mihogo. Lakini Wilaya hiyo ya Sengerema ilikosa eneo hilo la eka 2500. Kwa hiyo, kiwanda hicho kikakaa bila uzalishaji mpaka mwaka 1984 kilipouzwa kwa *Coastal Starch Manufacturing Company Ltd*. *(Makofi)*

Na. 116

**Ujenzi wa Viwanda vya Matunda**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inakusudia kujenga Viwanda vya kukamulia matunda hapa nchini kuongeza ajira kwa vijana, lakini pia kama njia mojawapo ya kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais ya kuajiri vijana milioni moja:-

Je, mpango huo utaanza lini na utaanzia kwenye maeneo gani ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Mgogoni, kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu, Wizara yangu imepewa jukumu la kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji kwa maana ya sera na kuhamasisha wawekezaji ili wawekeze kwa kasi zaidi na hasa katika ujenzi wa viwanda vya kukamulia matunda. Jukumu la ujenzi wa viwanda vyenyewe vikiwemo vya kukamulia matunda ni la sekta binafsi. Mpango wa kuhamasisha wawekezaji umeishaanza tayari kwa kuwa na Sera ya Viwanda na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo *(SME Development Policy)*. Msisitizo wa Sera hizi mbili ni kuhakikisha usindikaji wa mazao ya chakula yakiwemo matunda.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kwa kupitia *SIDO* na kwa msaada wa *UNIDO* ilibuni mradi ambao kati ya mwaka 1994 na Machi 2006, umetoa mafunzo ya wajasiriamali na kuwandaa wakufunzi kwa ajili ya mafunzo ya wasindikaji. Lengo la mradi huu ni kuongeza ajira ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la kumuuliza. Kwa kuwa suala la kumiliki matunda lipo katika sehemu nyingi za Tanzania na kwa kweli mengi huwa yanaharibika. Na kwa kuwa baadhi ya mitambo hii ya kukamulia inapatikana kwa bei nafuu sana kama India. Haoni sasa wakati umefika wa Serikali kutia mkono wake juu ya jambo hili ili wananchi wake waweze kupata namna ya kukamua matunda yao na kuweza kuwasaidia kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, mchango wa Wizara ni kutengeneza mazingira mazuri ya wanaotaka kuweka viwanda. Lakini hata hivyo kwa mtu ambaye anataka kujenga viwanda vikubwa vikubwa, Serikali inaweza ikamuunganisha na Benki ambazo zinaweza kutoa mikopo kwa ajili ya kupatiwa mikopo ya kujenga kiwanda hicho.

Lakini hata hivyo mpaka sasa hivi *SIDO* inashirikiana na Taasisi zingine katika kutoa mikopo. Kwa mfano, kuna mifuko ya mikoa ambayo inaitwa *Regional Revolving Fund*, ambayo inatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo.Vile vile kuna mfuko ambao unaendeleza viwanda vidogo ambao unaitwa *SME Competitive Fund*. Huo nao unaweza ukasaidia wawekezaji ambao wanataka wakope. Lakini pia, Benki Kuu mwaka huu imetenga shilingi 1,000,500,000/= kwa ajili ya wale wanaotaka kukopa lakini ambao hawana *collaterals* yaani vitu vya kuonyesha kwa ajili ya kupata mkopo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kuna Matangazo muhimu yafuatayo:- Kwanza, naomba nitambue kuwepo kwenye *Speaker's Gallery*, Mheshimiwa Herman Kyanzi Daniel Kirigini ambaye ni Baba yake Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini. Karibu sana! Mheshimiwa Herman Kirigini, alikuwa Mbunge na pia Waziri katika Awamu ya Kwanza. Naona, Mheshimiwa huyu alipostaafu akafanya jambo zuri tu, akampa *tution* mwanae naye yumo humu Bungeni. Ahsante sana! *(Makofi)*

Pia yupo Dr. Mabeba, Daktari wa Mifugo Mstaafu ambaye ameitumikia nchi kwa miaka mingi sana. Dr. Mabeba, tunakushukuru sana kwa utumishi wako kwa nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa, upande wa kushoto na kulia mlikuwa mnaona watoto wetu, kwa sisi wengine wajukuu zetu ambao ni wanafunzi. Nilikuwa sijapewa majina wanatoka shule zipi. Kwa hiyo, nilishindwa kuwatambua kabla ya kipindi cha maswali. Ninayo furaha sasa kuwatambua watoto walioko mkono wa kushoto ni kutoka Shule ya Msingi ya Martini Luther. Napenda wakati huo huo pia naomba wasimame wa Dodoma Sekondari, wa mkono wa kulia. *(Makofi)*

Kupitia kwenu wanafunzi, naomba niwapongeze sana walimu wa shule hizi mbili kwa kutambua umuhimu wa kuja kujionea wenyewe Demokrasia ya nchi yenu inavyoendeshwa. Hongera sana walimu. Tunaomba wengine nao waige mfano huo. *(Makofi)*

Wapo Viongozi wa Chama Cha Wahandisi wa Majenzi Wazalendo, *Tanzania Civil Engineering Contractors Association*. Wazalendo wanaojaribu kupenya katika Sekta hii ngumu sana ya Ujenzi. Chama chao kinaitwa *TASECA*. Naomba wasimame. Wanaongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Zakaria Nyanza, naomba apunge mkono. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ni Wenyeviti wa Vijiji kutoka Siha na Longido. Karibu sana Wenyeviti wetu wa Vijiji. Ni jambo zuri sana mmekuja kusikiliza jinsi Bunge linavyoendeshwa na kuwasikia Waheshimiwa Wabunge *Live*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo, itasherehekewa Siku ya Taifa la Canada. Sasa, Mheshimiwa Balozi Dr.Andrew McAlister yupo hapa na watakuja Raia kadhaa wa Canada kusherehekea Siku yao. Sisi sote Wabunge tunaombwa, saa 1.45 linapoahirishwa Bunge kwa leo, basi tukutane katika eneo letu la tafrija hapa hapa katika Viwanja vya Bunge ili kuungana mkono Taifa rafiki la Canada ambalo kwa taarifa yenu, hii ni mara ya kwanza katika nchi yetu kwamba Ubalozi wowote umeamua kuienzi Dodoma, Makao Makuu kwa kufanyia Siku ya Taifa lake nje ya Dar es salaam. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa wote muwepo pale. Spika, atakuwapo na kwa niaba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mambo ya Bunge, Mheshimiwa Juma J. Akukweti. Kutakuwa na Hotuba ya Balozi wa Canada

ambayo inahusu mambo ya Ushirikiano wa Maendeleo. Waziri wa Nchi yeye ndiye ameteuliwa kuandaa Hotuba kwa niaba ya Serikali ya Tanzania. Tunaomba wote mtakaoweza, tafadhalini tuweze kuwaunga mkono. Watakuwapo pia Raia wa Canada kutoka Mikoa yote ambako Canada wana miradi ya maendeleo wanayoendesha. Karibuni sana, leo jioni saa 1.45. *(Makofi)*

Taarifa ya Kikao: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, anawatangazia wajumbe wote kwamba kutakuwa na kikao leo saa 5.00 Asubuhi Ukumbi wa *VETA*. Kwa hiyo, saa 5.00 Asubuhi, Mkutano wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya Miundombinu. Kwa hiyo, saa 5.00 mhudhurie mkutano huo.

Kikao caha Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda, anawatangazia wajumbe wote kwamba saa 7.00 mchana leo, katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili Jengo la Utawala, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi. Wajumbe wote wanaombwa wahudhurie, ni kikao kifupi tu. Kutakuwa na kikao cha Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania wa Kupambana na Ukimwi *TAPAC* kitakachofanyika leo sa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Bunge namba 37 kwenye Jengo la Ukumbi wa Zamani, ghorofa ya tatu namba 37. Mwenyekiti Lediana Mafuru Mng’ong’o, anaomba wanachama wote wa Umoja wa Wabunge wa Kupambana na Ukimwi *TAPAC* wakutane hapo saa 7.00 mchana leo.

Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu wataungana na Wajumbe wa Kamati ya Maenndeleo ya Jamii ili kuweza kufanya mkutano kule *VETA* Saa 5.00 Asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, natangaza kwamba kuanzia leo mchana, Visanduku vya kupokelea barua vya Ukumbi huu, vinaanza kutumika. Yote yanahamishwa kutoka kule ili Waheshimiwa msiwe mnalazimika tena, ukitaka barua zako na kadhalika, kwenda Jengo la zamani halafu unarejea hapa wakati wa vikao. Kwa hiyo, mnaombwa sana mmpokee funguo zenu ili tuanze kutumia visanduku ambavyo vinafaragha zaidi vilivyopo hapa nje ya Ukumbi. Majina ya Waheshimiwa Wabunge wote, yapo kwa mujibu wa Mpangilio uliowekwa kuanzia leo tunahamisha kule ili tutumie huku.

Jingine ni kwamba kesho Saa 11.00, Mheshimiwa Waziri Mkuu atafunga hoja yake aliyoiwasilisha Bungeni hapa Siku ya Jumatatu. Sasa, kwa taarifa hasa, Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wageni. Kesho Bunge litakaa kama Kamati ya Matumizi ili kuweza kupitisha Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa, tunapofanya hivyo, ni lazima uwe na vitabu vyote vya Makadirio kwa sababu tunakwenda Vifungu kwa Vifungu. Vitabu vitatu hivi, *Volume II*, *Public Expenditure Regional* na hii *Volume IV*, Matumizi ya Maendeleo Wizara halafu na Mikoa. Bila ya kuwa na hivi, utakuwa unaitikia tu, wala huelewi kinachoendelea ni nini. Kwa hiyo, nawasihi sana Waheshimiwa kesho jioni Saa 11.00 tuwe na vitabu hivi ili kwa bayana tuweze kushughulikia hiyo Kamati ya Matumizi.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007**
**Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, ninao wasemaji 30, lakini ni dhahiri kwamba hawatapata nafasi wote hawa kuweza kuchangia. Kwa hiyo, tutajaribu kama utaratibu wetu wa kawaida ulivyo kuwapa kipaumbele katika hoja za Wizara zinazofuata. Tutaanza na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainabu Gama, ajiandae Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mpango wa Bajeti wa Serikali yetu ya Awamu ya Nne, ambayo ndiyo imechukua madaraka kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ninaomba niwapongeze, nimpongeze kwanza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa sasa rasmi kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu na viongozi wengine wote ambao wameteuliwa na hatimaye kupitishwa na *NEC* kuwa viongozi wa Chama chetu cha Mapinduzi katika nchi yetu ya Tanzania. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Dadangu mpendwa Mheshimiwa Zakhia Meghji na Manaibu Waziri wake kwa kazi kubwa waliyoifanya mwaka huu 2006 ya kuandaa Bajeti ambayo haijapata kutokea. Kwa kweli tunakupongeza sana dada Zakhia na tunakutakia kila la kheri katika kuendeleza shughuli hizi za masuala ya fedha kwa Maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba sasa nijielekeze katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kimsingi, niseme hotuba yenyewe kwa kweli ni hotuba nyeti na inaeleweka. Lakini yako mambo mawili matatu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho, ningeomba niyazungumze na kuyazungumza kwangu nataka kusema tu kutaboresha hasa utekelezaji wa kazi yenyewe katika kufanikisha maendeleo hayo ya wananchi wa Tanzania na hususan wananchi wa Jimbo la Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza, nianze na suala zima la ruzuku kwa ajili ya Pembejeo na hususan mbolea kwa wananchi wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu loa Peramiho ni Jimbo la Wakulima na ninaweza kusema katika Mkoa wa Ruvuma, wazalishaji wakuu wa mahindi kwa ajili ya chakula, ni wananchi wa Jimbo la Peramiho tukishirikiana na Majimbo mengine ndani ya Mkoa wetu na mikoa mingine na hasa ile mikoa mikubwa minne inayojulikana kama *the Big Four*.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuamua kuongeza ruzuku kutoka bilioni saba (7) kwa mwaka uliopita mpaka bilioni 21 kwa mwaka huu, ni cha ujasiri mkubwa

sana. Na mimi nasema kwamba Serikali imefanya maamuzi mazito katika Sekta hii yanayotakiwa kupongezwa sana, ila tatizo langu linakuja, utekelezaji wa kuhakikisha ruzuku hiyo ya bilioni 21 inawafikia wananchi kweli na wale wakulima na hasa wa kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze kwa kusema kwamba, hebu tujaribu kuangalia sura ya mfumo wa ruzuku kwa sasa hivi ilivyo. Inafananaje! Mimi, naomba nichukue kwamba sasa hivi tuna kioo labda kikubwa, tumekiweka hapa mbele na tunajaribu kuangalia ruzuku hiyo sasa inafananaje mpaka hatua hii na tunapofikia hatua ya kuongeza na kufikia bilioni 21.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ruzuku ya mbolea ina sura ya kutokuwafikia wakulima kwa wakati unaotakiwa. Hiyo ndiyo sura ya kwanza ya ruzuku hiyo ama mbolea hiyo ya ruzuku. Lakini, Pili; Mbolea ya ruzuku, ina sura ya kugongana na sura za mbolea nyingine zenye bei tofauti ndani ya masoko ama maduka yanayouza mbolea hiyo ya ruzuku. Hiyo ni sura ya pili inayofanana katika mfumo huo wa mbolea ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, sura ya tatu, ruzuku ya mbolea inaelekezwa zaidi katika kufaidisha wasafirishaji na siyo wale wakulima wenyewe ambao wanatumia mbolea hiyo ya ruzuku. Hiyo ni sura ya tatu ya mwonekano wa hiyo mbolea ya ruzuku ambayo sasa imeongezwa mpaka kufikia bilioni 21. Lakini, bado niendelee kusema. Bado sura ya mbolea hiyo ya ruzuku haiyagusi mazao mengine nyeti na hasa mazao ya biashara ambayo yanahitaji mbolea maalum kama tumbaku na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, sura ya mbolea hiyo ya ruzuku, imeishia katika suala zima la mahindi. Kwa hiyo, hiyo ni sura namba nne ya mbolea ya ruzuku. Lakini, niseme tena, sura ya mbolea hiyo ya ruzuku kwa ruzuku ya usafirishaji inaishia sana sana Makao Makuu ya Mkoa. yakiongezeka kidogo, Makao Makuu ya Wilaya na siyo kule vijijini kwa wakulima wenyewe. Sasa, hapo ndipo ninapoona tatizo zito lipo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri leo wakati anajibu swali, amesema leo mchana kutaenda kufanyika maamuzi mazito ya utaratibu wa ruzuku ya mbolea ili iweze kuwafikia wananchi wangu hasa wale wa Jimbo la Peramiho na wengine wote ambao wanatumia mbolea hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, mimi nasema, hivi tafsiri ya mbolea ya ruzuku tunaijenga katika misingi ipi? Ruzuku hii ya mbolea tunaijenga katika misingi ipi? Nauliza tena, tunajenga ruzuku hii kupunguza gharama za usafirishaji, ama tunataka tufike mbali kupunguza gharama za manunuzi kwa wakulima wenyewe kule vijijini?

Mheshimiwa Spika, naomba hilo labda wakalitazame vizuri zaidi. Ni kweli kwamba wasafirishaji wakipunguziwa gharama za usafirishaji, bei ya mbolea itapungua. Lakini nani ana uhakika kwamba mbolea hiyo ya ruzuku kweli yote inawafikia wakulima kama azma ya Serikali ilivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba, kwa nini tusiamue, wasimamiaji wakubwa wa mbolea hiyo wawe ni Vyama vya Akiba na Mikopo vya wananchi wenyewe kule vijijini. Kwa nini tusifikie maamuzi hayo? Kwa kuwatumia wananchi wenyewe na Vyama vya Akiba na Mikopo na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imesema inaviimarisha katika suala zima la utunzaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mimi naamini ruzuku hii ikifika kule, mimi nina Kata 14 na mpaka sasa hivi kupitia mpango wa fedha Vijijini, tumeishaweza kuanzisha *SACCOS* za wananchi 13 katika Jimbo langu na zinafanya kazi kubwa sana na nzuri sana.*(Makofi)*

Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati tukichangia hotuba ya Mheshinmiwa Rais, nilizungumza sana suala la kuimarisha Vyama vya Akiba na Mikopo na ninamshukuru sana safari hii limejitokeza kwa nguvu kwenye hotuba yake.

Ninaomba liendelee kujitokeza kwa nguvu kwa kuwapa madaraka kamili wananchi kwa maana ya kwamba chombo pekee walichonacho ndicho hicho Chama cha Akiba na Mikopo kinachoweza kumfikia kila mwananchi kule kijijini. Hebu tujaribu kuamua, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nimejaribu kuanza kutengeneza mkakati kwenye Jimbo langu kwa kutumia utaratibu huo na nina amini utafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini uwakala huo tusiwape wananchi wenyewe kupitia vyama vyao? Ama tuamue kumwamini *TFA* peke yake. Tuachane na hili tatizo la watu kubeba mbolea halafu hawawafikishii wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, tunaweza pia kuangalia njia nyingine. Tunacho chombo chetu kinachosimamia Vyama Vya Akiba na Mikopo Tanzania yaani *SCALT*. *SCALT* imekuwa ikikopa fedha kupitia Mfuko wa Pembejeo na imeweza kupeleka fedha hizo kwa wananchi kule vijijini kupitia Vyama Vya Akiba na Mikopo. Kwa nini tusifikirie pia *SCALT* ikasimamia suala hilo?

Ninaomba sana sana suala hili la ruzuku na hasa katika sekta ya pembejeo liweze kupewa nafasi na kufikiriwa kwa hali ambayo labda ni ya kimsingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ni uwezeshaji wa jamii. Nimefurahi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuambia kunatengwa shilingi milioni 500 katika kila Mkoa na ametueleza kwamba shilingi milioni 500 hizo zitapitia kwenye mabenki na ametuambia kwamba Serikali itasimamia kuhakikisha kwamba riba ya fedha hiyo ili kuwakopesha wananchi kwa kila hali na rika itasimamiwa ili kutokuwapa mzigo wananchi na kuhakikisha kwamba fedha hizo zinaweza kuwafikia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi tena kutengeneza kioo changu na kuanza kukagua mfumo wa mabenki nchini. Ni hoja isiyokataliwa, mfumo wa mabenki katika nchi yetu ya Tanzania kwanza mabenki yetu mengi yamebinafsishwa na hayako katika mikono ya Serikali yetu. Lakini pili mabenki hayo hayafikiki na wanyonge kwa urahisi.

Tatu mabenki hayo yanajiendesha kibiashara na siyo kutoa huduma. Vile vile dhana ya mfumo mzima wa mabenki hayo unajiongoza kulingana na matakwa ya wenye mabenki. Hivi ni kweli Serikali inaweza ikaamuru watu wale wanaojiendesha kibiashara wakakubali matakwa ya wananchi walalahoi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe tu kuna Meneja Mkuu wa benki moja nataka kumuona lakini nina mwezi mzima sijamuona mpaka sasa hivi. Sasa je, wale walalahoi watakapoanza harakati za kumiminika kuingia kwenye hayo mabenki kutafuta hizo fedha itawezekana kweli? Serikali imeamua jambo la msingi sana, naomba nguvu za uwezeshaji huu zirudi kwenye vyama vya akiba na mikopo na wala tusiache hela hii iingie katika mabenki ambayo mfumo wao ni wa kibiashara wakati sisi tumeshajijengea na Ilani ya Uchaguzi inasema tuimarishe vyama vyetu vya akiba na mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo la uwezeshaji nimeambiwa ziko Wizara kadhaa zimeagizwa kukaa pamoja na kutengeneza mpango tukishirikishwa na sisi Waheshimiwa Wabunge. Naomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, iingizwe katika kutengeneza mipango hiyo. Ishirikiane na hizo Wizara nyingine kusudi wafanye kazi yao kwa pamoja wa-*promote* hizo ajira, watoe hiyo mikopo na waiwezeshe jamii ya Watanzania na wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho wawezeshwe kwa sababu *SACCOS* zao zipo, miradi ipo, wamekosa uwezeshaji. Kwa hiyo, naomba sana hilo lifanyike. *(Makofi)*

Lakini linapofanyika liendane na muundo mzima wa mfumo wa stakabadhi za maghala. Nalisemea kwa ufupi lakini ni suala la muhimu sana. Ili kuweza kuwakomboa Watanzania, mfumo wa stakabadhi za maghala ndiyo ufumbuzi wa matatizo ya wakulima katika nchi yetu. Mifano imeshajionyesha tatizo lililopo sasa mfumo huo umejigawa katika Kanda kwa mfano mimi Wilaya yangu Makao Makuu ya Kanda yako Mbeya, wale jamaa mpaka wafike Songea imeshapita miezi sita. Hebu tuwawezeshe Maafisa Maendeleo ya Jamii, hebu tuwawezeshe Maafisa Ushirika wajenge hiyo *concept*, wawasaidie wananchi wetu huku sisi Kanda wanaendelea kutusimamia mambo yanakwenda kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sheria inayounda Mabaraza ya Madiwani au sheria inayowekea kuchaguliwa kwa Madiwani itazamwe upya. Sheria ile ndiyo inawabana Madiwani wetu mpaka sasa hivi wasitazamwe kwa jicho linaloondoa matatizo. Naomba irekebishwe ili Madiwani waweze kufikiriwa katika matatizo yao yanayowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho niseme natoa shukrani sana kwa kweli timu ya Mawaziri wetu imeanza kazi nzuri. Naomba nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ukikutana naye mnazungumza mnamaliza, Waziri wa Miundombinu, nampongeza sana tumeshazungumza masuala mengi sana tumeyatatua, ndugu zangu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, nawashukuru sana wananchi wangu wametambua kile mlichokifanya kwenye jimbo. Usalama wa Raia wako njiani kwenda mpakani kwa Mulukulu, Tanzania na Msumbiji kuweka mambo yao. Wizara ya Mambo ya Ndani nawashukuru sana na ninawakaribisha. Wizara ya Fedha, ndiyo usiseme kabisa wameweza kutengeneza umaarufu mkubwa katika Bunge letu. *(Makofi)*

Lakini naomba kuwaambia Waheshimiwa Mawaziri, tunapokuja kuwaona hatuji na hoja zetu kama zetu kama sisi, zile ni hoja za wananchi. Hatuji kuwaomba mtusaidie msaada, tunakuja kuwaomba wajibu wenu kwa wananchi wa Tanzania. Sasa kwa mifano hii ambayo imeonekana kwa Mawaziri ambao mimi binafsi nimeshakutana nao, sasa hivi tuna mkakati mkubwa na Waziri wangu wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ku-*promote* ajira kwenye Jimbo la Peramiho, nimemletea mkakati, anausimamia. Mazingira vile vile. Kwa hiyo, unapata moyo. Kwa hiyo, naamini kabisa hata wale wengine na nichukue nafasi hii kumuomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, aje katika Jimbo langu na aone hayo ninayomwambia ili tuweze kusaidiana kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Peramiho, nikushukuru wewe binafsi, lakini niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi tunavyoshirikiana katika shughuli mbalimbali ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge**,** nimetaarifiwa kwamba Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, hayupo, yuko jimboni ama kwenye kazi nyingine kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, nitamuomba Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, ajiandae na atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Martin Masunga.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi naomba nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa. Nawapongeza na wale walioteuliwa na Mwenyekiti wetu katika Sekretarieti. Nisingesema mmoja mmoja kwa sababu ya muda. *(Makofi)*

Pili, noamba pia niipongeze Halmashauri ya Kibaha Mjini, kwa kupata hati safi na kwenda mbele ya *LAAC* bila *audit query* moja. Naomba mfano huo Halmashauri zingine ziige.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru Serikali kwa kugawa Jimbo la Kibaha ili kupata Kibaha Mjini na Vijijini, imeniwezesha mimi kuwa Mbunge, nashukuru sana. Ombi langu sasa miradi yote ile ambayo inakwenda kwa sura ya Wilaya kwa maana ya *DC* basi itazamwe kwenye Halmashauri mbili. Nasema hivyo kwa sababu tayari kumeanza kuwa na dosari. *(Makofi)*

Suala la mgao wa chakula, Halmashauri hatukushirikishwa Madiwani wangu wanalaumiwa kwamba hawakushirikishwa na sehemu kubwa ya chakula imekwenda Halmashauri nyingine. Masuala ya miradi ya maji ilishirikishwa Halmashauri moja lakini namshukuru Waziri ameshasema twende tukasikilizane ili tutoe vijiji ambavyo tunaona ni muhimu. Suala la mradi Mpela uliotolewa wa *Planning International* shilingi milioni 100 ilitolewa kwenye Halmashauri moja, lakini baada ya kubembeleza ndiyo tukapewa

shilingi milioni 30 kwa ajili ya mbegu na 70 zikaenda kwingine. Sasa mimi nilikuwa naomba kama walivyofanya *TASAF* kututengea naomba ifanywe hivyo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwashukuru wananchi wangu wa Kibaha Mjini, kwa kunichagua kuwa Mbunge, naahidi kuwa nitafanya kazi kwa juhudi yote na maarifa yote niliyokuwa nayo Mungu aliyoniwezesha kuhakikisha wanapata maendeleo. Nimesema nitakuwa mtiifu sana kwao, sitakuwa tayari kula rushwa au kutumia cheo changu kwa faida yangu hata kama itabidi nidhalilishwe mimi na familia yangu. Nitawatetea wananchi wa Kibaha. Nimeshaanza kujitokeza lakini ninawaahidi wasijali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kusema mimi na wananchi wa Kibaha hatutawachekea wafanyakazi wowote wa Serikali, wafanyakazi wote wa *judiciary* watakaoamua kuwanyanyasa wananchi wa Kibaha Mjini, tutakuwa nao kidedea, tutaomba msaada na sisi itakapotokea tutakuja kwenu kuwaambia.

Mheshimiwa Spika, naomba tu ahadi za Rais zimetolewa na naomba kwa ajili ya Kibaha Mjini niseme kwa sababu ni Mbunge wa Kibaha. Ahadi mmoja inasahauliwa kila wakati, Rais wakati anakuja kuomba kura alisema nitahakikisha Kibaha Mjini, isiwe maficho ya Dar es Salaam, nitahakikisha naleta viwanda, ahadi hii huwa haisemwi. Wananchi wanangojea kwa hamu sana, wanajua kwenye suala la ajira na wao wataajiriwa.

Kwa hiyo, katika ahadi zote pamoja na hii naomba isiachwe. Lakini namuomba Mheshimiwa Rais, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 7 unaendelea wa 8 na wa 9 kuna mambo ambayo ni mikakati inawekwa kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuhakikisha wananchi wanashirikishwa na wakati huo huo wanasaidiwa katika uchumi na wao wausikie uchumi umewaingia.

Mheshimiwa Spika, ahadi hizi kumi naomba kutoa ushauri kwamba kila ahadi ipangiwe mkakati wa utekelezaji na ikiwezekana basi iwe na malengo katika miezi sita, sita kusudi kila baada ya miezi sita kusudi kila baada ya miezi sita ikifika tunatazama tumefikia malengo ambayo yatakwenda mwisho wa miaka mitano tutakuwa tumetimiza ahadi zile ili katika miezi sita tunafanya mapitio tena kweli hii ahadi itatekelezeka baada ya miaka mitano hii itakuwa nzuri. Kwa mfano, tunazungumza suala zima la elimu, tumefanikiwa kwenye suala la uandikishaji wa wanafunzi, mitihani ya darasa la saba tumejitahidi, wanafunzi wetu wengi wanafaulu angalau tuongeze zaidi asilimia 61 siyo kubwa. Lakini utazame mtihani wa darasa la nne nguvu bado haijakua wanafunzi wana feli wengi. Kwa hiyo, naomba hilo mtazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana Sekondari na tumeweka ahadi ya kila kata iwe na sekondari, ziwe sekondari zenye kutoa elimu ya kweli siyo sekondari madarasa. Unakuta hizo sekondari nyingi kuna madarasa manne hamna *library,* hakuna maabara na kadhalika, mwisho tutamaliza *form four* watoto hawa watakuwa hawana elimu. Kwa hilo, nilikuwa nataka tulizungumzia.

Mheshimiwa Spika, tulizungumzia suala la ajira na kwenye elimu ikitolewa elimu ya kweli vijana wetu watakuwa na *profession* ya kweli na watapata ajira ya kweli na kwa maana ya kuajiriwa. Inapofika ajira ya kujiajiri naomba nitoe ushauri, vijana wengi ninaozungumzia mimi sasa hivi ni wale wanaokimbia, wamachinga, wauza magazeti, wauza korosho, wauza maji, hawa tusipowafanyia mikakati tutawaacha nyuma, tunapozungumza *SACCOS* watakuja watoto wa akina Dr. Gama na kadhalika hawa ambao kila siku wanakimbiakimbia tuwafanyie mikakati ili waweze kuingia katika *SACCOS* na wakishaingia katika *SACCOS* vikundi vyao na biashara wanazozijua tuwaingize katika mradi unaoitwa MUKEJA.

Mradi huu wa MUKEJA ni mzuri sana unamchukua mtu unampa elimu ya kile anachokishughulika mwenyewe kujipatia ajira. Unamtoa hapa unampeleka pale. Lakini katika MUKEJA tuweke wanapofundishwa elimu ya utalaam wao wafundishwe na elimu ya darasa. Kwa hiyo, wale vijana walioishia darasa la saba ambao wazazi wao hawakuwa na hela wakiingia katika vikundi hivi watafundishwa. Nimeambiwa mwaka mmoja atafundishwa *form one, form two,* mwaka wa pili *form three, form four,* mwaka wa tatu *form five* na *form six*. Mtoto huyu aliyekata tamaa kwa mpango huu utamfikisha mahali pazuri. Huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, kushirikisha wananchi. Mimi nasema hili jambo ni zuri sana lakini ombi langu tunahitaji kuhakikisha taarifa zote, sheria zote na mambo muhimu yawafikie. Mimi nilikuwa nazunguka kuwashukuru wananchi, hawajui suala la MKUKUTA mpaka sasa wananiita mama MKUKUTA. Mambo sijui ya *MDG* hawajui. Kwa hiyo, mimi nasema tuwafikishie ili waweze na wao kuelewa.

Mheshimiwa Spika, juzi Bunge lililopita wenzangu mlivyoondoka mimi nikaingia katika kila *pigeon hole* ambayo nilikuwa nakuta kuna karatasi muhimu nikakusanya nikawapelekea Madiwani wangu wametumia hiyo, kwa hiyo, ilinisaidia sana.

Mheshimiwa Spika, nyongeza Ofisi ya Mbunge, najua mimi ni Mbunge mgeni, Ofisi ya Mbunge, bado yangu na bahati mbaya niko na Mbunge mwenyeji ambaye kwa kuwa amekaa muda mrefu ameandaliwa pole pole ofisi mpaka alipofikia hilo mimi sina lalamiko nalo. Lakini inatia aibu ukifungua mlango wa mwenyeji ukija kwa Mbunge mgeni ni vichekesho, mlango hauna cha kufungia, viti kingine cha rangi nyekundu huku kocha, lakini ukienda kwenye kabati wadudu wametafuna ungaunga unatoka. Nimemuuliza *RAS* amesema Bunge ndiyo wanaoshughulikia lakini najua siyo Bunge ni *RAS*. Kwa hiyo, mimi naomba wapange bajeti, kama waliweza Mbunge mwingine mgeni wakamshughulikia naomba na mimi wanisaidie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *tender board*, naomba itazamwe vizuri sheria ya mwaka 2001 ilimruhusu Mkurugenzi kuwa Mwenyekiti, sheria ya mwaka 2004 hairuhusu, lakini mpaka leo baadhi ya *tender board* Mwenyekiti bado ni Mkurugenzi, tuiangalie vizuri na sheria hii tazameni vizuri sana kwa sababu hapa ndiyo kwenye makulaji, manunuzi na *tender*. *(Makofi)*

Lakini la mwisho kwa sababu nimesikia hawa wanaohusika na masuala ya *tender* wako hapo tukubaliane tupewe *register* ya kuonyesha *list* ya watu wote ma-*engineer* wa utalaam mbalimbali ili wanapopitisha ifikie hatua na sisi tutazame kweli huyu amekuwa *registered*. Inasikitisha Mwenyekiti wa Halmashauri hahusiki kwenye *tender board,* lakini ikishapitishwa anaambiwa saini, anasaini kitu gani anachokijua?

Lakini lingine naomba nizungumzie Shirika la Elimu Kibaha, kwa maana ya Hospitali. Ninyi wote mnatambua sehemu kubwa ya ajali, 30% inafikia Hospitali ya Shirika la Elimu Kibaha. Kwa masikitiko haina vifaa, imefanya watalaam waliokuwa pale wanakata tamaa, naomba niwaambie *accident* mnaziona zikipatikana tunamaliza *first aid, next day* wote wako Muhimbili, hakuna vifaa. Naomba tupatiwe vifaa, inasikitisha *instance* imetokea watu wameumia wanataka kupewa damu watu wamejitokeza hamna hata mifuko ya kutilia damu. Wengine wanakufa kwa hiyo, mimi naomba ile Hospitali tuitazame kwa jicho la huruma kwa sababu sehemu kubwa ya 30% ya *accident* zinatokea huko.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Kibaha Mjini tuna matatizo, baada ya Dar es Salaam kuwa wanapima viwanja sasa hivi watu wote wanakimbia Kibaha Mjini na wao wanaifanya ni kijiji wanataka mashamba. Tumejaribu kuwaambia Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa hawasikii. Mimi nimeseme, Mkurugenzi kasema, *DC* kasema lakini mpaka sasa mashamba yanauzwa. Lakini sheria inasema ni eka tatu tu za mashamba, hawasikii tunaomba Serikali mtusaidie tufanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule, naomba shule za walemavu ikiwezekana tuweke katika kila Mkoa shule moja, ukiweka shule moja ya *primary* na sekondari utamsaidia huyu mlemavu akae *boarding* na utaweza kuweka walimu wa aina ya ulemavu katika shule hiyo kwa sababu sasa tunadanganyana haiwezekani watu wazazi wameandikisha watoto wao…

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivi naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wenzangu kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa uteuzi wake Mkuu alioupata hivi juzi pamoja na sekretarieti akiwemo ndugu yetu Mheshimiwa Aggrey Mwanri ambaye anastahili kuwa Katibu Mwenezi katika Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru wewe kwa namna unavyoliendesha Bunge kwa sayansi. Unaliendesha vile vile kama ulivyozungumza kwa *Standard and Speed*. Kwa hiyo, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu namfahamu sana kutokana na harakati zake kubwa za utendaji. Ni mtendaji mzuri, ni mfuatiliaji mzuri, tena anashaurika, ukimshauri anakubali. Kwa hiyo, huyu ndiye anayetufaa kabisa kuwa ndiye Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

Serikali ya Awamu ya Nne, anakwenda vile vile kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Lakini niwapongeze vile vile Mawaziri wote waliokuwa katika ofisi yake akiwemo rafiki yangu Mheshimiwa Mizengo Pinda na Waziri anayeshughulikia na Shughuli za Bunge, Makatibu Wakuu wote nawapongeza sana naamini kwamba Waziri Mkuu, watakusaidia sana hawa uliopewa, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianzie kwa kumpongeza ndugu yangu Msajili wa Vyama, ndugu John Tendwa pamoja na msaidizi wake ndugu Rajab Baraka, kwa kazi nzuri anayofanya katika kusimamia Vyama vya Siasa katika nchi hii. Lakini mimi nilikuwa na ushauri mmoja katika usajili wa Vyama vya Siasa ili upate usajili inabidi kila Mkoa upate wanachama 200. Lakini kwa sasa hivi jinsi wananchi wote wanaofahamu nini maana ya mfumo wa vyama vingi nafikiri sheria hii sasa hivi imepitwa na wakati. Iko haja sasa hivi hiki kiwango ambacho kilikuwa kimewekwa iko haja kukizidisha kabisa badala ya 200 sasa *at least* kidogo iwe 1,000 nina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana ya kuzungumza hivyo wakati wa mchakato wa uchaguzi vyama vyote vinaingia katika uchaguzi na kutuma ma-*candidate* wake katika majimbo. Lakini jambo la kushangaza kabisa kwa mfano katika jimbo langu la uchaguzi Jimbo la Amani, nilikuwa na ma-*candidate* ambao tuna nafasi ya kugombea ubunge vyama tisa. Lakini katika vyama tisa, vyama saba vyote kila chama kinapata kura moja/mbili, kinapata kura tatu. Mimi naona hii ina kasoro kidogo na hii inawapa shida hata wale wapiga kura wenyewe kumtafuta yule mtu wao ambaye wanamtaka, lakini *list* ya wale ni wengi mno ambao wakati ule ule wanachama wale katika jimbo lile kule hawapo.

Sasa mimi ningeshauri ni demokrasi kwamba vyama viingie katika *system* ya mchakato wa uchaguzi lakini kile chama kisione haya kwamba mimi katika jimbo hili wanachama sina. Sasa vurugu hii ya nini. Sasa mimi ningeshauri kabisa kile chama kilichokuwa hakina wanachama ndani ya Jimbo lile mimi nafikiri haina haja ya kuweka *candidate* kwa sababu ni vurugu, tena isitoshe ni gharama inazidi kabisa ambao wanachama wake hawapo pale. Sasa mimi ningeshauri sheria hii irekebishwe, itazamwe upya na iangaliwe upya kabisa ili tufanye shughuli zetu kwa utaratibu ambao unaokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchangia naanza na hifadhi ya mazingira. Mazingira ni uhai, mazingira ni uchumi, hivi karibuni tunafahamu Watanzania wote kutokana na uharibifu wa mazingira namna tatizo lililokutumba la njaa, njaa imetukumba Tanzania nzima, ikalazimika Serikali kutumia fedha nyingi kabisa kutafuta chakula kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni kwamba Serikali itenge fedha, naiomba tena Serikali, Waziri Mkuu nisikilize vizuri, naona unazungumza na Mheshimiwa Mizengo Pinda hapo, naiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kufanya *(nurseries)* vitalu nchi nzima. Hii isione taabu kwamba inatupa fedha, hapana, inatengeneza hali ya nchi, inatengeneza mazingira mazuri ndani ya nchi, itenge fedha

itengeneze *nursery* nchi nzima kila mwananchi agawiwe miche miwili ili apande na aiangalie. *(Makofi)*

Mimi nakubalia ushauri, miche kumi naomba kumi, maana nini? Mimi bahati nzuri ni mmoja wa mwanamazingira Makamu Mwenyekiti wa Bunge wa Kamati ya Mazingira, kila unapokwenda unapata risala miche iliyopandwa katika Mkoa lakini ukifuatilia miche ile haipo imekauka yote kwa sababu haina mwenyewe. Lakini tukiweka utaratibu mzuri, unaofaa, tukafanya *nursery* tukawaka wananchi bure, wakaitunza miti ile, naamini baada ya miaka miwili/mitatu hali ya Tanzania itakuwa ni nzuri na mvua zitanyesha kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri sana ushauri huo utiliwe maanani sana hasa kwa vile mazingira, miti namna ilivyokuwa imekatwa, mabwawa yamekauka, mvua hazinyeshi kikawaida hii ingesaidia sana hapo baadaye miaka ijayo, hata vijana wetu na watoto hawa walioko pale vijana wanaosoma itakuja kuwasaidia wakati mvua zinaponyesha kikawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya mazingira imekuwa ni ngumu sana, hivi sasa mabonde yote yamekauka, hata *Lake Victoria* kina cha maji kimepungua sana na nafikiri ni vizuri tukatumia *Lake Victoria* katika nchi zetu tatu hizi kwa ufanisi unaokubaliwa, kwa sababu nchi nyingine *Lake Victoria* maji yake yanatumika kwa wingi zaidi ukilinganisha na nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimwa Spika, sasa mimi ningelishauri sana katika kutumia maji ya *Lake Victoria* tutafute mbinu na tukubaliane namna ya kutumia maji yetu.

Mheshimiwa Spik,a lakini kina cha maji kikubwa kinapungua kutokana na uingiaji wa takataka kwa wingi sana katika *Lake Victoria* na kuingia kwa gugumaji katika Ziwa Victoria kwa hivyo, mbinu na utaratibu wa kutafuta njia ya kutatua tatizo la gugu maji ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nakwenda kwenye ajira na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kabisa kwa kupeleka shilingi milioni 500 na ninaamini Jimbo langu la Amani Zanzibar litanufaika. Naamini hivyo, najua hivyo na mimi Jimbo langu la Amani, Zanzibar litanufaika na shilingi milioni 500 hizi na kama hivyo, basi hivyo ni nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeliomba tu hizi shilingi milioni 500 zisiwe na urasimu, halafu riba yake ikubalike kwa sababu sasa hivi Watanzania wanajiweka vizuri sana, *SACCOS* si muhimu, lakini wanashindwa kukopa pesa mabenki kutokana na riba kubwa. Leo ukiweka wewe pesa unapata 7% riba, lakini wewe ukienda ukakopa pesa benki unapata riba 20%. Hii ni unyonyaji wa hali ya juu. Serikali hili suala ingawaje haidhuru tunasema ni soko huria lakini sasa hii imekuwa soko holela. Lazima Serikali iingilie kati kuangalia utaratibu huu. Haiwezekani kwamba wewe ukiweka asilimia ndogo sana ambayo hailingani, wewe ukichukua asilimia kubwa sana ambayo hata kiwango chake wewe huwezi kufahamu, sasa hiyo nafikiri Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye kupanda kwa bei ya mafuta. Mafuta ni nyeti sana. Mafuta ni moja katika nyanja za uchumi ndani ya nchi. Hivi sasa mafuta yanapanda bei holela sana. Lakini kupanda mafuta holela hivyo ni hasara kwa wananchi wetu huko vijijini, kwa sababu hao gharama zote zinazopanda walipaji ni wao. Leo nauli siku zote unasikia zimepanda, wakipakia mizigo kuleta kwenye soko bei kubwa. Gharama za uchukuzi ni kubwa, bei za vyakula ni kubwa. Sasa kila kitu kimepanda kutokana na upandaji wa mafuta holela. Ningeomba Serikali kwani Serikali haiwezi kuagizia mafuta yenyewe, hawa matajiri ikachukua mafuta Serikaini, itakuwa kuna tatizo na kasoro?

Mimi ningeshauri sana kuwe na utaratibu mzuri kabisa, Serikali iagizie mafuta kwa sababu upandaji wa mafuta bei hiyo yote haijui kwamba wanapandishwa kiasi gani, wanafahamu kwamba hii ni Serikali, kumbe Serikali kabisa haihusiki na habari hiyo. Sasa mimi ningeshauri kabisa ili kuwanusuru wananchi wetu wanyonge, basi kwa utaratibu Serikali iagazie mafuta halafu yale makampuni yachukue mafuta Serikalini na yasambaze yauze kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kitu kimoja ambacho ni kero kubwa na hii Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar wanalizungumzia sana kuhusu akinamama wanaopata taabu bandarini. Hili kwa kila anayekaa hapa hulizungumzia suala hili.

Mheshimiwa Spika, huu MKUKUTA una maana ndefu sana na MKUKUTA ni kuwawezesha wananchi hasa akinamama kujiajiri, kuondokana na umaskini na kiuchumi. Lakini sasa tatizo akinamama wanavyokwenda kuchukua bidhaa Zanzibar na kuja nazo Bara bado matatizo yako pale pale, hivi kuna nini Mheshimiwa Waziri Mkuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu leo tupe tamko rasmi na sisi tuelewe na wana Zanzibar wasikie, kuna nini? Waziri Mkuu hebu tueleze hiki kitu, kama kuna tatizo kubwa basi na sisi tuelewe hata sisi Wabunge unajua Waheshimiwa Wabunge kuna tatizo moja, mbili, tatu, nne, tano na sisi tukazungumze na wananchi wetu, tukawaeleze hali halisi. Lakini ninyi matatizo mmeweka mfukoni na sisi tunapiga kelele, mnatuona kama sisi tuna wazimu humu ndani. *(Makofi)*

Sasa utaratibu utakuwa si sahihi kabisa, tupate tamko Mheshimiwa Waziri Mkuu leo, ili kesho utakapokuwa una-*wind up* tujue tatizo ni nini, akinamama wasipate usumbufu, tunasahau kwamba hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi moja, Serikali mbili? Lakini mambo yetu yote yanakwenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili naomba rasmi, hizi kero hizi ziondoke. Loo! Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini mimi leo naomba nianze na kutoa pole kwa wananchi wa Shinyanga na hasa wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Shinyanga na hususan Wilaya ya Bariadi. Kijana wetu mmoja alikuwepo katika Mkutano Mkuu huu wa juzi bahati

mbaya wakati wanarudi wamepata ajali, Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi amevunjika mbavu na wengine mikono, lakini kijana wetu huyu ndugu yetu alikuwa anaitwa Ndugu Makaranga amezikwa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni Mbunge wa Mkoa ule natoa pole sana nasema Mungu alitoa na sasa ametwaa, jina lake libarikiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi nichukue nafasi kwanza kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kupata nafasi nyingine ya kuwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Ndugu yetu, Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mbunge wetu, mwenzetu na sekretarieti yake kwa kupata nafasi hii. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nichukue nafasi hii tena nimpongeze sana Waziri Mkuu, Waheshimiwa wote Mawaziri na Naibu Mawaziri, lakini wewe binafsi nakushukuru, unavyoweka kwa kweli kama unavyosema mwenyewe viwango na kasi, Naibu Spika safi, lakini bado kwa Wasaidizi Wenyeviti bado umeweka mwanamke na mwanaume na kusema kweli asilimia 50 sasa itaendelea kuwepo kwa ajili yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa niingilie moja kwa moja kwenye suala la kilimo. Nataka nizungumzie kuhusu kutosheleza kwa chakula. Mkoa wetu wa Shinyanga kwa kweli ndiyo ilikuwa kati ya janga la njaa ulikuwa ndiyo Mkoa wetu wa kwanza. Lakini nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mkuu alifika mwenyewe Shinyanga, pamoja na Mikoa yote lakini kwetu alifika, alitembea karibu Wilaya zote na akatoa misaada ya kutosha. Mkuu wangu wa Mkoa wa Shinyanga yuko hapa na ananisikiliza na kweli wananchi wa Shinyanga wanasema ahsante sana na Mungu akujalie kwa hili. *(Makofi)*

Pamoja na hilo labda mimi niseme lifuatalo, katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, umesema kuhusu hifadhi ya chakula kwa Taifa kwamba ziimarishwe na ili kuwezesha kuwepo na akiba ya chakula cha kutosha. Lakini labda niongezee mimi naona nayo Mikoa iwe na akiba ya chakula chake. Kwa mfano Shinyanga kuna *SGR* pale, lakini kama ingekuwa ni ya kwetu na bado ya Taifa ipo, Mkuu wa Mkoa angeweza kutoa chakula chake kwanza wakati Taifa linaendelea kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda mimi niseme juu ya kilimo cha umwagiliaji maji. Mkoa wetu kwa kweli una hali mbaya kama unavyojua, chakula, njaa. Lakini tuna mabonde mazuri. Basi ni vuziri Idara hiyo ije ili itusaidie ili na sisi tuweke kilimo cha umwagiliaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu jengo hili zuri, lakini wananchi wetu tukisema wana njaa, watu wanaweza wakashangaa kidogo. Lakini sasa naomba niende kwenye suala la maji. Mimi naomba nitoe shukrani kwa niaba ya Mkoa wa Shinyanga kwa kweli tumelalamika muda mrefu lakini sasa kilio chetu kimeanza kuisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabomba yale ukiyaona mimi mwenyewe mzima mzima naweza nikaingia na ningekuwa maji ningeweza kunywewa. Mabomba ni makubwa, kwa kweli tunashukuru na wanawake wa Shinyanga wamenituma wanasema Serikali ahsante sana na kwamba mmezingatia kuona Mkoa wetu ni jangwa lakini ni maji ni wanawake na wanawake ni maji. Wanasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hii mimi nimshukuru Waziri Mkuu, kwanza alikuwa Waziri wa Maji ndiyo aliyeanzisha hii Awamu ya Tatu. Namshukuru Rais lakini Waziri wa Maji, lakini alivyoondoka yeye akatazama nani achukue nafasi yake. Nashukuru kwa kumpa Mheshimiwa Stephen Wasira. Mheshimiwa Stephen Wasira, anatosha na Naibu wake anatosha na mimi nataka niseme kwamba pamoja na kwamba vijiji 54 tu ndiyo vitapimwa Mwanza na Shinyanga, lakini sisi tuna vijiji zaidi ya 80 lakini namjua Mheshimiwa Stephen Wasira alivyo, ataweka maneno tutapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu zile ambazo ni pembezoni zaidi, basi atusaidie angalau visima virefu na vifupi ili tuendelee kuwa na maji ya kutosha. Aendelee na juhudi hizo ili ziwe endelevu. Namwaminia Mheshimiwa Stephen Wasira. *(Makofi)*

Lakini vile vile niende kwenye miundombinu, leo mimi nashukuru tu. Wabunge wengine wanalalamika, mimi leo nashukuru. Tumelalamika sana lakini sasa Mkoa wa Shinyanga tuna haki ya kushukuru sasa. Miundombinu barabara Dodoma mpaka Mwanza, ukipanda basia Mwanza unaingia Shinyanga unapata raha tu. Unakwenda mpaka Igunga raha tu. Sasa unapofika tu Mkoa wetu wa Singida sielewi kulikoni. Tunaanza kuumia viuno mpaka tufika hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wakandarasi mmetupa, yule wa Singida ana tatizo gani? Kwa nini hachukuliwi hatua? Jamani Wasukuma tunasema ndiyo taabu hatuna shida, tupeni raha. Tufike mpaka Dar es Salaam siku moja. Hebu angalieni watu wa Shelui wana matatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kuzungumzia barabara ya *Old Shinyanga* kwenda Mwanza. Barabara ile inaimarisha sana uchumi wa Mkoa. Vijiji vile ni vya wakulima, wanalima pamba, mpunga, dengu na vile vile kuna mifugo. Lakini barabara ile wapiganaji wetu wako wengi wanajeshi kule na njia ile ni fupi zaidi kuliko hii ya Maganzo na mkitupa njia hizo mbili mambo yatakuwa safi. Mabasi yanaenda mengine Maganzo, mengine yanapitia *Old Shinyanga,* wananchi wote tunakuwa safi. Naomba utusaidie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie habari ya afya. Afya mafanikio yapo lakini lengo kila kijiji kuwe na zahanati na kila kijiji na kila kata kuwe na kituo cha afya. Mpango wa Serikali ni mzuri basi uwe wazi. Uharakishwe basi maana yake watu kule wanahangaika. Lakini wananchi washirikishwe, wameshazoea sasa kushirikishwa na *TASAF*. Mheshimiwa Aziza Sleyum jana alisema *TASAF* ipo na wananchi wanaelewa.

Lakini lingine Halmashauri ya Wilaya na vijiji basi izingatie kutenga maeneo kuanzia sasa, waagizwe watenge maeneo. Katika hotuba ya Waziri Mkuu ilizungumzia kuhusu magari 22 ambayo yatanunuliwa kipindi hiki na kwamba watapeleka kwenye

Wilaya mpya. Mkoa wa Shinyanga tuna Wilaya mpya ya Kishapu, naomba gari hilo lifike moja. Lakini bado tuna Wilaya ambayo iko pembezoni na haina hospitali. Wilaya ya Bukombe tunaomba tukipata hiyo tutashukuru zaidi. Watu ni wengi zahanati kwa kweli ni kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la elimu. Mimi nimshukuru sana Waziri Mkuu katika mikoa yote Shinyanga kwa kweli Waziri Mkuu alitushangaa. Watoto wengi wamefaulu kwenda Sekondari lakini nafasi hakuna. Pamoja na njaa tuliyokuwa nayo, tumejenga shule 39. Lakini yote hayo ni kwa sababu ya msukumo wa Waziri Mkuu. Mimi nasema Mama Lowassa, kama ananisikia, mtunze Mheshimiwa edward Lowassa, mpe ugali ashibe, atufanyie kazi. Ndio maana sikutaka kumsifia mwanzo, nilitaka nimsifie katikati. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Edward Lowassa anafanya kazi na mimi nasema kwa kweli Waziri Mkuu huyu sasa tumepata. Watu wanasema upele umepata mkunaji, sasa huyu ndiyo mwenyewe. Lakini pamoja na yeye Waziri mliyetupa naye mambo siyo mabaya, siyo mabaya Mama Sitta. Mama Sitta amekuja kutembelea Mkoa wetu, anasema darasa hili bomoweni halina ubora wa viwango. Mama wa viwango. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana na najua ataendelea. Lakini sisi tunasema kwamba mambo haya yanawezekana, tunaomba mtuletee walimu sasa shule zipo, watoto nao wapate raha. Wapate raha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za uchaguzi, mimi nichukue nafasi hii kushukuru sana kutoka asilimia 20 mpaka asilimia 30, leo nipo hapa. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Shinyanga kwa kunipa nafasi kuwa Mbunge, nami leo nazunguka katika kiti hiki na mimi nawaambia Mkoa wa Shinyanga kwamba sitawaangusha kama anavyosema Rais wetu wa nchi. *(Makofi)*

Kuhusu ajira na uwezeshaji wa wananchi kwa maana ya kiuchumi. Mimi nichuikue nafasi hii kushukuru sana hizi shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa na nasema mimi nilikuwa nahangaika Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, yupo hapa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, nilimwita, nikasema hapa ukisema *SACCOS* watu hawaelewi. Ukisema sijui MKUKUTA hawajui. Tukasema tuanzishe kitu kinaitwa Vikoba. Nikaenda kwa ndugu yangu Mheshimiwa Devota Likokola, nikamwambia hebu niambie huko Songea mnafanya vitu gani? Nimeweka Waziri ameviona na nashukuru kwa kuviona yeye Naibu wake wakaingia kwenye Vikoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri kile kiburi chako sasa kina shilingi milioni moja na laki mbili na nusu. Sasa kwa hela hizo zilizokuja mimi zimenipa nguvu mtakapofika kwamba hela zipo lakini mimi naomba niseme ombi, hizi hela zigawanywe kwa kila wilaya ili tujue kila Wilaya inafanya kazi gani.

Mheshimiwa Spika, sasa nichukue nafasi hii niseme Serikali imekusudia kuunda Bodi kusimamia mikopo hiyo na Waheshimiwa Wabunge watashirikishwa na sisi tunashukuru. Kwa sababu kila unapokwenda wanasema Rais alisema hapa

mtatuwezesha.  Tuwezesheni, hii mikutano tunashindwa ndugu zangu.  Fanyeni mambo haraka ili tukienda kule tuweke mikutano tuwe na majibu barabara.  *(Makofi)*

Naomba nimalizie na suala la mifugo.  Kuna machinjio manne ya  sasa tumeambiwa, yako Dodoma, Pwani, Rukwa, Morogoro katika Wilaya ya  Mvomero.  Mimi najiuliza Shinyanga je?  Maji yapo, tunaomba, kuna ng'ombe, tunaomba mtuletee machinjio na huko na kiwanda chetu kifanye kazi, sasa kimekuwa kibovu tu.  Lakini nisemee kuhusu wafugaji wale wanaoambiwa warudi kwao.  Naomba niweke angalizo.  Sasa tunaweza tukaita rushwa, maana ukipita hapa na pale unaambiwa wewe si una ng'ombe, kama unataka kupita hapa weka ng'ombe watatu hapa.  Lakini naweka angalizo. Naomba mlitazame.  *(Makofi)*

Mwisho, mimi nichukue nafasi hii kushukuru Mawaziri na Manaibu Waziri wanawake, kwa kweli wanafanyakazi.  Ukiona wanafanyakazi waangalie wengi wamekata nywele, hawana nafasi ya kwenda *salon* kama sisi.  Wanachapa kazi, waangalieni wakati wanajibu hoja Bungeni.  Nasema wanawake wanafanyakazi na mimi nawatakia kila la kheri na nasema wanawake tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeni Mama Zakia Meghji imekwenda moja kwa moja asilimia mia. Nani kama siyo Mama Zakia Meghji?  Wanawake tunaweza.  *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba mwisho nitoe shukrani kubwa sana kwa wanawake wa Mkoa wa Shinyanga, nasema mimi niko na najua mnaniona nasema nitawafanyia kazi kwa nguvu zangu zote na ari yote kwa kasi mpya.  Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, nasema naunga mkono hoja asilimia mia moja na thelathini. Ahsanteni.sana. *(Makofi)*

**SPIKA:**  Ahsante.  Waheshimiwa Wabunge, kweli wanawake wanaweza. *(Makofi)*

**MHE. JANETH M. MASSABURI:**  Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu na mimi nichangie hoja hii.  *(Makofi)*

Kwanza kabisa naanza ibada ndogo, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyeniwezesha niwe miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  Namshukuru sana Mwenyezi Mungu.  Namwomba aendelee kunipa nguvu na hekima.

Mheshimiwa Spika, bado namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia kiongozi mwema, hodari, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye mimi namfananisha na Nabii ambaye ametumwa na Mwenyezi Mungu kuja kutusaidia sisi Watanzania ambao wengi wao ni wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani, samahani bado nashukuru. Napenda kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao wao wamenionyesha imani

kubwa na heshima kwa kuniruhusu au kunichagua niingie katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili niwe mwakilishi wao. Nawashukru sana wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam na mimi nawaahidi sitawaangusha, niko nao siku zote kama Mungu atakavyonijaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizi napenda nitoe pongezi. Kwanza katika pongezi nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi wa Tanzania pamoja na wapinzani kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili nampongeza kwa dhati Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar, pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vile vile nampongeza kwa jitihada zake kubwa na uhodari alionao na uchapakazi anaofanya katika kutatua matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Naibu Spika, Mama Anne Makinda. Nawapongeza Mawaziri wote na Manaibu wao katika nyadhifa walizo nazo. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Vile vile nawapongeza wjumbe wote wapya wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja na arobaini, kama alivyosema mwenzangu naongeza kumi. Napenda sasa nichangie hoja hii ya hotuba ya Waziri Mkuu katika maeneo yafuatayo:-

Moja eneo la ulinzi na usalama, mbiundombinu, utawala bora na ushirika. Nikianza na ulinzi na usalama, majeshi yetu ya ulinzi na usalama yameonyesha nidhamu ya hali ya juu si kwa kuwa na utayari wa kivita bali pia hata palipotokea dharura na maafa kwa jamii kama vile mafuriko ya Lindi/Mtwara, ajali ya *MV Bukoba*, ajali ya treni hapa Dodoma, ujenzi wa madaraja kama vile daraja la Msata na mengineyo mengi, wanajeshi wetu walishiriki kikamilifu na hata madaktari wa Hospitali ya Taifa Muhimbili walipogoma, madaktari wa kijeshi waliwatumikia wananchi bila kusita. Kwa kweli mimi nawapa pongezi na wanastahili sifa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ufanisi katika vyombo hivi vya ulinzi na usalama, naiomba Serikali ivipatie vyombo hivi mahitaji ya vitendea kazi vya kisasa vinavyoendana na sayansi na teknolojia kama vile magari, boti za doria, meli za doria

ambazo zitakwenda kwenye kina kirefu, pikipiki, mafunzo ya kijeshi ya mara kwa mara ndani na nje ya nchi.

Kuhusu ujenzi wa nyumba za maaskari kwa mtindo wa magorofa pia pawepo na bajeti ya matengenezo madogo madogo ya nyumba zao sambamba na mafuta kwa ajili ya operesheni. Kuna tetesi tumesikia kuna baadhi ya askari waliostaafu wameajiriwa katika majeshi ya nchi jirani. Kama habari hizi ni za kweli, tunaziomba zifanyiwe utafiti wa kina kwa sababu kuna uwezekano wa kuvuja kwa siri za nchi. Kwa hiyo, wahusika tunaomba wafuatilie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri, Waziri wa Usalama wa Rais na Naibu wake pamoja na wasaidizi wake akiwamo *IGP* Said Mwema na jeshi lote la polisi kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya kwani matunda yameanza kuonekana hasa katika suala la kupambana na uhalifu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi kwa jeshi letu la polisi lakini Idara ya Usalama Barabarani bado dawa haijapatikana na hii inatokana na kutokusimamia vizuri kwa sheria za usalama barabarani kwani kuna baadhi ya matrafiki ambao wanaitia dosari Idara hii kutokana na matrafiki hawa kuwa na mahusiano ya karibu na madereva wa daladala ambapo hali hii inapelekea madereva kuwa na dharau na kiburi dhidi ya abiria na wanafunzi. Maana suala la unyanyasaji wanafunzi limekuwa kama wimbo na hatua hatuzioni kama zinachukuliwa kwa hiyo, hawa madereva wa daladala waelewe wazi kuwa hawa wanafunzi ndiyo viongozi wa baadaye. *(Makofi)*

Natoa mfano wa Rais wa Kongo, Mheshimiwa Joseph Kabila alipofanya ziara hapa nchini aliwahi kusema kwamba aliteremshwa na dereva wa basi katika maeneo ya Mikumi. Sasa je, mnyama angemla huyu Mheshimiwa Rais hivi kule wangekuwa na Rais. Kwa hiyo, tuwaheshimu wanadamu, huwezi kujua huyu unayemtupa na kumtukana atakuwa nani hapo baadaye? Hivi naomba niulize hawa wenye daladala au madereva hivi hawazai? Hawana watoto nyumbani na kama hawana, hawana watoto hata wa shangazi zao? Tunaomba wawaheshimu wanafunzi pamoja na abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia na Idara husika ianzishe sheria kali dhidi ya madereva wetu ili Tanzania iweze kuishi kwa amani. Kutokana na udhaifu huo ndiyo maana ajali hazipungui kwa mfano utakuta gari halina breki lakini linatembea barabarani bila wasi wasi. Vile vile magari mengine yanatembea taa moja nyakati za usiku wakati mwingine watu hudhani ni pikipiki, matokeo yake ni ajali, unasikia watu 50 wamekufa. Hawa ni binadamu siyo kuku. Tunaomba eneo hili kwa kweli lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara ya Usalama wa Raia kuhakikisha Idara ya Usalama Barabarani inachukua hatua za makusudi na za haraka ili kurekebisha dosari hizo lakini pia iongeze adhabu kali kama nilivyosema hapo awali, dhidi ya madereva wazembe, kwani roho za binadamu haziuzwi dukani. Vile vile naishauri Serikali kupitia Idara ya Wizara ya Usalama wa Raia iongeze vizuizi vya barabara zenye vifaa za kisasa na hasa kamera na pia umbali wa kutoka kizuizi hadi kingine upangwe upya ili kuimarisha zaidi usalama barabarani lakini pia kuwepo na ile miiba ya nondo kama wanavyofanya wenzetu wa nchi jirani kama Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika miundombinu, katika kuimarisha na kuboresha miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, barabara zifuatazo naomba zifanyiwe matengenezo ya haraka ili ziweze kutatua tatizo la msongamano wa magari. Kwanza naomba barabara ya Buruguni - Uhuru hadi *Clock Tower*, pili, Ubungo Maziwa hadi *Mama Land Mabibo External*, tatu Kitunda kupitia Mwanagati hadi Tandika Azimio, nne Barakuda kupitia Vingunguti hadi *Nyerere Road*, tano Kigogo kupitia Tabata Dampo hadi *Mandela Road*, sita Segerea hadi Majumba Sita kupitia *Segerea Seminary*, saba Kagera, Mburahati hadi Kigogo darajani na maeneo mengine ambayo yako katika Kata ya Gerezani, Mchikichini na Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwezi Septemba, 2006 Serikali itaanza rasmi kutekeleza mpango wake wa kuweka *speed meter* katika *taxi* zote, naiomba Serikali iharakishe ukarabati wa barabara kwa sababu hiyo endapo kutakuwa na mita hizo kabla ya ukarabati huo kuna hatari ya kuwasababishia gharama kubwa abiria wa *taxi, waiting charges* kutokana na foleni za barabara ambazo zinasabasihwa na ubovu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja katika Utawala Bora, baadhi ya maofisa watendaji kata hawasimamii ipasavyo maafisa walio chini yao. Kwa mfano, Afisa Afya wanashindwa kuwajibika katika utendaji wa shughuli zao za kila siku na ndio maana uchafu umekithiri sana katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, maafisa hawa wa afya wanao wajibu wa kuwatembelea kila kaya au kila mtaa, wananchi na kuwaelimisha kanuni za afya, lakini wengi wao hawafanyi hivyo. Mimi naamini kuwa iwapo maafisa afya watasimamia suala zima la usafi ipasavyo, kwa kila kaya kwa kuwapa vipeperushi na kuwaelimisha sheria na kanuni za afya, wananchi wataelimika na suala zima la usafi litakuwa ni historia katika Mkoa wetu.

Pia naishauri Serikali na hasa Halmashauri za miji zitafute makampuni yenye uwezo wa kuzoa taka hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwani utakuta magari yameoza, lakini yanatembea, wakati mlango mmoja nao unaanguka basi yote, gari limebeba takataka na lenyewe linaonekana kama ni takataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naingia katika ushirika yaani *SACCOS*, sisi Wabunge tumeanza kwa kasi mpya kama walivyotangulia wenzangu kuhamasisha vyama vya akiba na mikopo. Ombi langu kwa Wizara husika naiomba iandae programu maalum ya kutoa elimu ya namna ya kuanzisha *SACCOS* na faida zake kwa wananchi kupitia vyombo vya habari kama vile *TV*, *Radio*, vijarida, vipeperushi, kutoa semina mbalimbali maana wengi wao hawajui. *(Makofi)*

Pia naishauri Serikali itumie zile *mobile cinemas* kama ilivyokuwa miaka ya 1970 katika kuwahamasisha wananchi kuhusu elimu ya afya, namna ya utunzaji wa mzingira, ukulima wa kisasa, matumizi ya mbolea, ufugaji wa kisasa, malezi bora, elimu ya

mazingira kama nilivyosema ujenzi wa nyumba bora na kuwatunza watoto yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na arobaini kama nilivyosema awali. Naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Matemwe, natoa shukrani kwa kunipa nafasi leo hii kuwa nami mmoja kati ya wachangiaji katika hoja iliyo mbele yetu. Lakini kwanza wacha kwa ruhusa yako nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika vile vile niwapongeze wananchi wa Jimbo la Matemwe, kwanza kwa heshima kubwa waliyonipa kunileta hapa na vile vile niwapongeze kwa heshima kubwa waliyokipa Chama cha Mapinduzi ushindi wa kishindo kwenye Jimbo la Matemwe, lakini niwapongeze vile Watanzania wote kwa kujua uwezo wa Chama cha Mapinduzi kukipa ushindi katika nchi hii, nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi za Rais na Mwenyekiti wa CCM kwa kura nyingi na za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema nawashukuru ndugu zangu wa Jimbo la Matemwe kwa kunichagua, lakini kwa heshima kubwa waliyonipa, nasema kwamba sitowaangusha, ninachoomba waendelee kunisaidia kama vile miaka mitano ya nyuma waliyokuwa wamenisaidia katika kuhuisha Jimbo lile na kufikia hali ya kwamba tumeweza kuibua shule tisa katika Jimbo la Matemwe na kuibua mahala ambamo hamna shule kiasi ambacho sasa hivi Jimbo la Matemwe, mtoto hawezi kutembea zaidi ya kilometa sita hajakuta shule. Lakini nichukue nafasi hii vile vile niishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanziabar na vile vile nimshukuru Mheshimiwa Waziri Haruna, kwa ushirikiano aliokuwa ametusaidia kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa kama manvyoelewa mimi ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, lakini naelewa vile vile kama mnavyoelewa mimi ninayezungumzia Matemwe Wizara ya Elimu ambayo kwa bahati mbaya sana uwanja huu haugusi sawa sawa. Lakini nadhani kuzungumza kwangu salaam hizi napongezi hizi zitafika, labda niseme kwamba tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ahadi waliyokuwa wameweka lakini zaidi kwa kazi ambayo wanayoifanya na kuitekeleza. Hivi sasa hivi kumejengwa njia kutoka Pongwe kuipeleka Matemwe.

Mheshimiwa Spika, njia hii kwa sehemu kubwa sana inapita katika jimbo langu. Lakini zaidi hivyo vile vile niishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwamba kuweza kutujengea njia au ahadi waliyotoa kujenga njia kutoka Mishelishelini kwenda pale Mchangani. Njia hizi mbili zimefumbua tatizo kubwa la mawasiliano na kuondoa umaskini tatizo ambalo katika jimbo la Matemwe lilikuwa likitufika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo mimi nasema vipi hii nchi ni moja, Serikali mbili Katiba inasema hii ni nchi moja, Serikali mbili na kwa kweli tunahisi wakati mwingine kama choyo au tunahisi kama uzito, kwamba Wabunge wa Jamhuri la Muungano, wanasimama na wanazungumza kwa nguvu moja na kutetea hoja ambazo zina manufaa katika majimbo yao. Sisi hapa tunasikiliza hoja hizo na kwa bahati mbaya

kama utasimama basi huwezi ukazungumza Zanzibar kwa maana ya Jimbo, na tutazungumza Zanzibar kwa maana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hii ni nchi moja, Mheshimiwa Waziri Mkuu anachapa kazi sawasawa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunachomuomba kwamba atafute kipengele katika nchi hii ya kuona kwamba tunasaidiwa moja kwa moja katika majimbo bila kufikiria suala la Serikali kwamba ya Muungano ama sio Muungano. Hivi sasa nakukaribisha katika Jimbo la Matemwe, lakini Matemwe tupo karibu sana sisi na Jimbo la Kitope, kwa maana ya Kiwingwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja hivi karibuni na tunamshukuru sana na namwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kule watu walijipanga pembeni zile nyendo zake zote kuingia na kutoka zote vijana walikuwa wanaziratibu na kutaka hata kukuona. Walitamani wamuone kwamba angalau azungumze nao, lakini sijui naye alifungwa vile vile kwa sababu ni Waziri wa Serikali ya Muungano ama kwa maana ya kwamba labda pale hawezi kuzungumza. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba, utakapokuja kule kama ulivyo, njoo kifua wazi wanasema vijana mwendo mdundo, tunakutaka kule uje Mheshimiwa uje kutusaidia *later on,* suala hili la kwamba kuna Serikali mbili, hii nchi moja bwana na kule sasa hivi tunapovyozungumza umewakuta ndugu zetu pale wa kimasai wanalinda, wanalinda nini mbona hawajaenda Kenya kwenda kulinda. Naambiwa kule wako lakini si Watanzania, wale si wa Kenya, wamasai wa Kenya hawapo pale. Pale kuna sehemu wanaita Kibanda Ugali yaani ni mahali ambapo utakuta wafanyakazi wote au karibu *90 percent* wametoka Bara, nchi ni moja tusaidie bwana, mfano hizi shilingi milioni 500 zinazotoka katika kila Mkoa kwa nini basi wekeni shilingi milioni 500 mseme kwa Zanzibar zima sisi tuna Mikoa mitano kila mmoja shilingi milioni 100. Watu wanasema kuna usemi wa watu wazima kima akikosa mwitu, nafikiri kima anatembea katika msitu mara nyingi. Sasa ile mbuga yote mkiifyeka atakuja mabegani bwana, kwa sababu anataka lazima arukie mahali. Kwa hivyo, sisi kule kote tutakuja mabegani tusaidie bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitabu hiki cha hotuba yako ukurasa wa 28 utawala bora, iko sehemu inasema: "Serikali itaendelea kutekeleza majukumu ya kusimamia utoaji wa haki kwa wananchi na kuhakikisha taratibu zinafuatwa katika masuala ya mikataba na kisheria."

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kusema hapa aidha, Serikali itawawezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake ili kupunguza mlimbikano wa kesi, nataka kudunda katika nukta hii. Hilo asubuhi kulikuja swali linauliza uhalali uliokuwepo wa kwamba watu wanachukua sheria mikononi mwao, wezi wakitokezea raia wana waua au raia wanawachoma moto. Jibu limetolewa hapa kulikuwa vile vile kuna jibu la nyongeza, lakini zaidi ni kwamba hapa hawa askari watafanya kazi mpaka watoke upara kama nilivyotoka mimi hivi. Lakini kama mahakama, katika vyombo vya mahakama havikutekeleza, mahakimu hawakutekeleza kazi zao zinavyotakiwa, hatuwezi hata siku moja kusimama. Ni kweli kabisa muhalifu anapelekwa polisi akifika kule yule muharifu anafika nyumbani mapema zaidi kuliko yule aliyempeleka. Lakini zaidi ya hivyo ni

kwamba yule aliyekuwa anampeleka ana wasiwasi kwamba mimi maisha yangu kesho na kesho kutwa yatakuwaje.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza vipi, katika hili ni kwamba lazima tuone mahakama wanachukua wajibu wao ipasavyo, sio hivyo, utawala bora hakuna, sio hivyo, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu atafanya juu chini, chini, juu hawezi nchi ikatulia. Kwa hiyo, mahakama lazima ichukue nafasi yao, lakini kuna wakati mwingine najiuliza katika hii mihimili mitatu muhimili wa Rais au *Executive* au Rais mwenyewe ni *answerable* kwenye Bunge, sisi ni *answerable* kwa wananchi, mahakama ina *answerable* wapi kwa Waziri, ikiwa hakimu anacheleweshа kesi ama kwa makusudi, ama ana utashi fulani yeye hakimu anawajibika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba hili tupate jibu baadaye, hakimu yeye anawajibika wapi au wakati mwingine inawezekana hakimu tu akasema au akahukumu anavyotaka tu kwa mujibu wa utashi wake, yeye anawajibika wapi, kuna siku ambayo kuna chombo kinamwajibisha kuna chombo kinamuuliza.

Kwa mfano, taasisi fulani inawezekana ikapitia mjadala wote ule na kesi zote halafu ikaonekana huyu kafanya sivyo au hakufanya sivyo, hatuwezi kwenda tumsaidie Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, tuisaidie Serikali hii na tuone kwamba mahakama, mahakimu wanashughulikia kesi kwa wakati na wanatoa *judgement* ambayo inastahili. Tunazungumza habari ya walioko magerezani, hivi sasa tatizo kubwa ni mahakimu, ukiona kesi haijakamilika, vipi hii kesi itakaa miezi sita haijakamilika, mtu kaua aliyeuawa anajulikana, waliouwa mashahidi wapo, sasa ushahidi gani unaotaka? Au ule ushahidi wa kuwa mnatafuta ushahidi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri na hili nalo limefahamika, kwa haya machache naomba kwamba tuzingatie hayo na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuzungumza kuhusu hoja ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa awali ya yote niombe kutoa pongezi kwa Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vile vile kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM. *(Makofi)*

Vile vile napenda kutoa pongezi kwa wale wote waliochaguliwa kuwa kwenye sekretarieti ya CCM, vile vile napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu, vile vile natoa pongezi kwa Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mawaziri wote kwa kuteuliwa katika nyadhifa zao, Manaibu Mawaziri kwa kuteuliwa katika nyadhifa hizo na Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu. Naiunga mkono hoja kwa sababu ina matumaini ya kutuletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia niwashukuru wananchi wa Ngara walioniwezesha kufika hapa, nawashukuru kwa sababu wamenipa asilimia 74 ya kura zote zilizopigwa katika Wilaya ya Ngara. Nalisema hili kwa sababu wakati wa mchakato mzima kulikuwa na *rumours* nyingi sana ya kwamba jimbo la Ngara linaenda upinzani. Sasa nataka kuwahakikishia wale waliopeleka *rumours* ya kwamba haikuwezekana na CCM ndio chama tawala katika jimbo la Ngara. *(Makofi)*

Vile vile kuhusiana na hilo nataka kutangaza ya kwamba jimbo la Ngara limempa Mheshimiwa Rais JAkaya Mrisho Kikwete asilimia 93 ya kura zote zilizopigwa na limekuwa jimbo la kwanza katika Mkoa wa Kagera kutoa kura nyingi kwa Rais Jakaya Kikwete. Kwa hapo nawapongeza nawashukuru sana wananchi wangu wa Ngara kwa kutoa kura nyingi kwa Chama cha Mapinduzi. Vilevile nawashukuru wananchi wa Ngara kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi katika ngazi ya udiwani, madiwani wote 17 walichaguliwa katika Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kuhusiana na hiyo nawashukuru sana wananchi wa Ngara, kwa sababu wameonyesha kwamba wanakipenda Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Katika kuchangia hoja hii nitalishughulikia sana sana jimbo la Ngara na wakati Mawaziri tofauti watakapotoa hoja nitachangia Kitaifa. Tuanze na suala zima la Ulinzi na Usalama. Ndugu zangu Waheshimiwa kuna tatizo la usalama katika Jimbo la Ngara na hili tatizo linatokana na wakimbizi. Huwezi kutoka Ngara ukaenda Bukoba bila kuwa na *escort* ya polisi, huwezi kutoka Ngara ukaenda Mwanza bila kuwa na *escort* na saa nyingine ni kitu cha hatari hata kusafiri ndani ya jimbo lenyewe.

Kwa mfano, nilipokuwa niko kwenye harakati za kutafuta kura za maoni, naenda Murusagamba, nilikoswa risasi na majambazi na juzi juzi hapa nilipokuwa kwenye likizo katikati hapa, gari ya *Immigration* ilikoswa risasi na ikapinduka, hali ni mbaya sana ya usalama. Tunachoomba, wananchi wa Ngara wanachoomba, tuongezewe ulinzi katika jimbo la Ngara. Kusema ukweli *grade* ya polisi sasa hivi nadhani sio kwa kiwango cha wakati huu labda tuwafanyie *upgrading*, tuwape silaha na labda tuwape sijui *training* ya aina gani ili wakabaliane na ujambazi katika Wilaya ya Ngara. Ni kitu cha hatari sana kwenda Ngara. Magari yanatekwa, makubwa kwa madogo, vifaa vinatekwa, malori yanatekwa, ingawa utawala wa Mkoa umejaribu kukusanya bunduki ambazo zipo katika mikono ya majambazi.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kuzikusanya bunduki zote kwa sababu nyingi zinakuja na askari kutoka nchi za jirani ambao hawajavaa *uniform* na kwa sababu wanazungumza lugha hiyo hiyo ya Kihangaza au Kishubi inakuwa ni vigumu sana kuwa *ditect*. Kwa hiyo, nacho waomba Serikali iweke mkakati maalum wa kukaribiana na ujambazi na kitu kikubwa kushinda yote ni kuwarudisha makwao wahamiaji wote ambao wametoka nchi za jirani na wanajipenyeza katika Wilaya ya Ngara. Nitashukuru sana kama hii ikizingatiwa. Kuhusu hilo wananchi wa Ngara wanasema hivi angalau tupewe fidia kwa wale ambao wanauawa na majambazi kutoka nchi za jirani. Hawazungumzi ya kwamba wapewe fidia ya kipesa, ila wajengewe miundombinu, *infrastructure* iwe bora zaidi, kwa mfano, tukijengewa barabara, ujambazi utapungua kwa sababu hizo barabara

zitatumika kwa wingi zaidi. *Frequency* ya magari kupita itaongezeka na majambazi watakuwa wanakamatwa kwa kirahisi zaidi.

Vile vile hizo sehemu ambazo zimeathirika zaidi basi wajengewe zahanati ili waweze kutibiwa ukikoswa risasi au ukiumizwa. Ukipata matatizo ukiwa Murusagamba inabidi uje mpaka Benako kutibiwa. Murusagamba hakuna simu, Murusagamba hakuna barabara ya uhakika. Kwa hiyo, inachukua siku nzima hata polisi kujua kama kuna tatizo au hakuna tatizo, kwa hiyo, tukipewa simu, umeme, mazingira kama ya Murusagamba tutakuwa tumepunguza matatizo ya ujambazi.

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hilo niangalie kilimo. Kilimo Ngara, kusema kweli kinaendeshwa kizamani, mimi tangu nizaliwe Ngara hakuna aina yoyote ya pembejeo inayokuja, ni jembe sijaona mbolea. Wakati natembelea kata nilijaribu kuzungumzia hili suala, kwanini watu wa Ngara hawatumii mbolea, ng'ombe wapo lakini mbolea haitumiki, tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo ni kwamba *extension officers* au maafisa ugani kusema ukweli hawahamasiki kuwaelekeza wakulima kutumia mbolea. Udongo umeanza kuchoka, haiwezekani kuboresha kilimo Ngara bila kutumia mbolea na itabidi tufanye msukumo wa makusudi kuboresha uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, mpaka miaka kumi iliyopita Ngara ilikuwa haitokei njaa, hata kama ikiwa kuna upungufu wa mvua Ngara ilikuwa haitokei njaa kwa sababu kama kuna ukame watu wanaenda mabondeni. Ngara ina milima na mabonde, kwa hiyo, huko kwenye mabonde, tunalima wakati wa kiangazi. Sasa hivi ni kama udongo umechoka, kwa hiyo, inabidi tuongeze bidii ya kuzalisha chakula na *critical factor* ni hawa maofisa ugani. Tatizo lake ni kwamba hawana usafiri hata kidogo, kwa hiyo, naomba kilimo kiboreshwe kwa kupewa pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nachoomba lishughulikiwe ni afya. Ngara kuna hospitali moja tu ambayo ni *Dis-ignited Government Hospital (DGH)*, ni ya *mission* haina madaktari, haina manesi, tunaomba Serikali itusaidie madaktari ili tuweze kuboresha maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, kingine napenda kuzungumzia kuhusu elimu. Ngara madarasa yamejengwa sawa, mimi sina tatizo na hilo, lakini tatizo ni kwamba hakuna walimu, shule nyingi hazina walimu na hata walimu waliopo wangefaidika na *refresher courses* kusema ukweli wanahitaji mafunzo ya ziada ili vijana waweze kupasi mitihani.

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari zimejengwa lakini hazina walimu, sekondari zimejengwa tisa, lakini hakuna walimu wa kutosha, Waziri Mkuu alikuja Benako, wakati amekuja. Benako ile sekondari ni mpya, ina mwalimu mmoja na walimu watatu wa kujitolea ambao hawapo kwenye *payroll*.

Mheshimiwa Spika, sasa tufikiri tumeboresha majengo, tunakosa walimu hatuwezi kuboresha elimu bila walimu na hapa nizungumzie kwamba labda kulikuwa na

uzorotaji katika ku-*train* walimu, *we were not serious,* katika ku-*train* walimu, ndio sasa tuna matatizo makubwa sana ya walimu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuweke mkazo, tuweke jitihada za ku-*train* walimu, *to allocate more resource*, *financial resources* katika *training* ya walimu wa rika zote tangu shule ya msingi, shule ya sekondari, hata vyuo vikuu. Kwa sababu matatizo ya walimu, yako *across the board* mpaka vyuo vikuu kuna *shortage* ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalozungumzia ni umeme. Ngara tumefaidika na umeme, *head quarter* ya Wilaya ina umeme. Lakini umeme haujafika Kabanga, tunaomba Serikali iweke pesa ya kuiruhusu *TANESCO* ipeleke umeme mpaka Kabanga, mpaka Rulenge, mpaka Murusagamba. Kwa sababu wanahitaji umeme ili walete maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nanichoomba ni miundombinu ya barabara, tuna barabara mbili, moja ya kwenda Rwanda na nyingine ya kwenda Burundi, tunashukuru Serikali imejitahidi. Lakini barabara kutoka Murugarama kwenda Kenza mpaka Nyakaula, ni barabara ya udongo na tungependa iwekwe lami. Itatusaidia katika kukomaza ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Ngara Mjini kuna maji lakini Rulenge hakuna maji ya bomba, tunaomba Serikali iweke jitihada ya kuleta maji katika Mji wa Rulenge kwa sababu wanalalamika ya kwamba Wahangaza ambao wanakaa kwenye sehemu za milima wana maji lakini sehemu za Bushubi hawana maji angalau na wao wapate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa ni nafasi ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na nadhani kuna nafasi kuna Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kunifikisha hapa kwa afya njema na kuijalia familia yangu afya njema, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Namtumbo kwa kunipa imani yao mimi kuja kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu, naomba kuwahakikishia wana Namtumbo wote kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kuchaguliwa kwake kuwa Katibu Mkuu wa Chama chetu cha Mapinduzi na wajumbe wote wa sekretarieti yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti nzuri, aliyoitoa kwa umahiri mkubwa na umakini mkubwa, bajeti hii ndiyo kiini na msingi wa kufanikisha malengo yetu tuliyojiwekea kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM na vile vile katika MKUKUTA kwa miaka mitano ijayo hivyo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake alisema naomba nimnukuu katika ukurasa wa 9 *paragraph* ya 12 mstari wa 10: "Viongozi na Watendaji wa Serikali wanategemewa kuelewa ahadi na mikakati hiyo na kuhakikisha kuwa fedha zinaelekezwa kwenye maeneo yaliyoainishwa kwenye mpango wa maendeleo, Serikali katika ngazi zote inahitaji umakini na umahiri katika utekelezaji wa mipango yake hivyo haitakubali vikwazo vya aina yoyote visivyo vya lazima, viongozi na watendaji wote wa Serikali wanao wajibu na kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji na kila mara kutoa taarifa za utekelezaji kwa mamlaka husika," mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu na hatuna budi kushirikiana ili kufikia malengo na mabadiliko ya maendeleo tunayoyakusudia. Watendaji ndiyo usukani wa gurudumu hili, hivyo hawana budi kuwajibika kweli kweli kushirikiana na viongozi wa siasa kwani miaka mitano si mingi hasa tukizingatia tunapigana vita dhidi ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifikapo mwaka 2010 tuje kuwaonyesha wananchi wapi tulipofikia malengo yetu kama vile Serikali kufikia malengo ya kutoa huduma muhimu kwa wananchi na kuongeza uwezo wa kugharamia uendeshaji wa Serikali, hayo yote yanategemea watendaji wazuri wenye moyo wa kizalendo hivyo watendaji wote naomba kwa dhati kabisa kwa dhati ya mioyo yetu tuelewe kuwa tunahitaji kwelikweli kuondoa umaskini wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara yangu ya Ubunge ya kushukuru katika mikutano yangu mzee mmoja alisimama akasema kwa nini tunampigia kura Diwani? Kwa nini tunampigia kura Mbunge? Nikashtuka khee na mimi pia? Kwa nini tunampigia kura Rais na kwa nini tusimpigie kura Hakimu, Mwalimu na Afisa Mtendaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali lake nilimuelimisha aina tofauti ya watu hao na kwa nini watu hao wanapigiwa kura, lakini mzee yule alikuwa na maana ya kwamba wana imani sana na viongozi wa kuchaguliwa wa siasa kuliko watendaji.

Mheshimiwa Spika, naomba watendaji wasitufikishe hapo kwa wananchi kwamba wao wasiaminike sana sisi Wabunge tukaaminika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie bajeti hii kupitia Halmashauri yetu ya Namtumbo ambayo ndiyo bajeti yake ya kwanza toka Halmashauri yetu ianzishwe, kwa upya wa Halmashauri yetu inakabiliwa na changamoto nyingi za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya wananchi wa Namtumbo kwa mujibu wa Ilani ya uchaguzi ya CCM na MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ya mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Namtumbo katika ukurasa wa 14 jedwali ambalo tumeambatanishiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 206/2007 Halmashauri ya Namtumbo imeidhinishiwa shilingi 394 milioni kwa ajili ya *OC* na kiasi cha shilingi 4,373,936,400/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, kwa watumishi waliopo 956 wa kada mbalimbali kabla ya *salary adjustment* yaani marekebisho ya mishahara halisi ni shilingi bilioni 1,808,736,446.4 hivyo kufanya ziada ya mishahara iliyotengwa kuwa shilingi bilioni 2,565,201,953.60, kiasi hicho cha fedha ni ziada kubwa mno hata ukifanya marekebisho ya mishahara kuongeza ajira mwaka 2006/2007, labda Serikali iamue kuajiri watumishi wasiopungua 700 kwa kipindi hiki cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, upungufu umeathiri *OCs* yaani matumizi mengineyo hasa katika Idara ya Maji, Kilimo, Afya na Ujenzi. Sekta ya Maji imeidhinishwa *OC* kwa mwaka shilingi milioni 5, sekta hii ni muhimu sana na Idara ya Maji ina jukumu kubwa sana ya kuhakikisha upatikanaji wa Maji Safi na Salama kwa wananchi wa Namtumbo moja ya kipaumbele kikubwa ni maji kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa maji katika Jimbo la Namtumbo pia katika ziara zangu nililala katika kijiji kimoja Kata ya Magazi, asubuhi nilipoamka akina mama walikwenda kuteka maji kwa ajili ya kuoga Mheshimiwa Mbunge na wageni wake na kwa ajili ya kutengenezea chai na wananchi waliopo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akinamama wale walipokuwa wanakwenda kuteka maji kisimani, mtoni wakati wanashuka wakakutana na simba anakunywa maji katika kisima kile, akinamama wale wakasita, wakasimama juu wakawa wanabishana wengine wanasema simba yule ni wa safari anakunywa maji anakwenda zake, wengine wakasema simba yule amekula nyama sasa anakunywa maji, hiyo ndiyo hali halisi ya Jimbo langu la Namtumbo. Akinamama wanavyo-*risk* kwenda kutafuta maji na maji hayo maana yake anakunywa simba,tembo, fisi, Mbunge na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Namtumbo ina mpango wa kutekeleza vipaumbele vya wananchi hususan maji lakini bajeti ya *OC* shilingi milioni 5 kwa idara ya maji kwa mwaka haitoshi tunaomba marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya kilimo na mifugo, Halmashauri imetengewa shilingi milioni 12 kwa sekta hizi mbili ambazo ni sawa na shilingi 500,000 katika kila idara kwa mwezi, kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na mipango tuliyojiwekea na

Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2006/2007 kama ilivyojieleza katika kitabu chake ukurasa wa 39 na 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanikisha yote katika kilimo katika Wilaya yenye *square kilometres 20,375* ukitaka kwenda Kusini kijiji cha mwisho unahitaji kusafiri kilometa 264, ukitaka kwenda Kaskazini unasafiri kilometa 130 kutoka Makao Makuu ya Wilaya yenye watu 98% ni wakulima, nashauri bajeti ya Halmashauri ya Namtumbo irekebishwe kwenye ziada ya mishahara baada ya marekebisho yake ya mishahara kufanyiwa na kupata namba za kada ya watumishi watakaoajiriwa katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kufuta ushuru wa mazao ya kugharamia bodi za mazao, kama ushuru wa bodi hasa ya Tumbaku na sasa Serikali itagharamia bodi hizo 100%.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa maana mkulima alikuwa anabebeshwa mzigo mkubwa sana hasa wa Tumbaku katika kugharamia bodi hizo. Kwa hiyo, hatuna budi kuishukuru Serikali na ninawaambia watu wa Namtumbo mwaka huu hakuna tena zile kodi za bodi.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna vitu vinavyomnyongesha mkulima wa tumbaku, nilizungumzia katika hotuba yangu ya kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais kwamba unapofika ununuzi wa tumbaku pale wanunuzi wa tumbaku wanamwondoa mkulima wa tumbaku nje ili wao wafanye kazi yao ya kupanga *grade* ya tumbaku, hii si sahihi.

Mheshimiwa Spika, leo hii huwezi kwenda dukani kwa mtu kununua kiberiti, ukifika pale ukamwambia mwenye duka kwamba mimi nataka kununua kiberiti toka nje nichague kiberiti kitakachonifaa mimi, huyo mtu atachukua kweli kiberiti? Au atachukua na kingine? Hiyo ndiyo hali halisi kwenye tumbaku, tunaomba Serikali nayo isimamie hili kuondoa kabisa lile suala la kumuondoa mkulima wakati ma-*least man* na ma-*classifiers* wanapopanga *grade*. Mkulima atatambuaje kwamba kwa nini amepata *grade* ile ikiwa anaondolewa nje? Tunaomba Serikali iangalie hili mkulima naye ashirikishwe kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mbolea ya ruzuku limeelezewa vizuri sana na Mheshimiwa Mbunge, Mwenyekiti wetu wa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma, lakini naomba nisisitize suala moja. Naiomba Serikali itoe mbolea ya ruzuku wakati wa mavuno, wakati wananchi wanauza mazao yao ndiyo wakati ule mbolea ya ruzuku nayo Serikali itoe, kwani Serikali inagharamia ile mbolea ya ruzuku baada ya wale wauzaji kurejesha *returns* zao kwenye Serikali ndiyo inalipia zile gharama. Kwa hiyo, itakuwa ni vyema na busara kwa mkulima akipewa mbolea ya ruzuku kwa wakati huu anapouza mazao yake ndiyo pale aweze kununua mbolea na kuihifadhi ndani lakini mbole ya ruzuku ikianza kutoka mwezi wa 12 mkulima anakuwa hana pesa anaanza kubabaika. Naomba Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia vipimo vya kununulia mazao kwetu kule sijui Serikali au Bunge lilipitisha lini suala hili, naamini haijafanya hivyo la kutumia makopo kupimia mazao au mtu anakuja anasema mimi nitanunua lumbesa gunia kubwa kule tunaita mbanganda, mimi mara mbili anasema nijazie mahindi au mpunga nakupa shilingi 10,000/=, kipimo cha wapi hiki?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kabla sijaanza kuchangia naomba nami niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura zote 99.999% kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza pia Wabunge wenzangu walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimabli, Mheshimiwa Yusuf Makamba kuwa Katibu Mkuu, Mheshimiwa Rostam Azizi kuwa Mweka Hazina, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kuwa Katibu Mwenezi na Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa Kupambana na UKIMWI Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe kuwa Mkurugenzi wa Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuteua wanawake wengi katika Baraza la Mawaziri na kuweka *record* ya nchi yetu kuwa mojawapo ya nchi duniani yenye Mawaziri wengi wanawake, tunamshukuru sana kwa imani aliyotupa. *(Makofi)*

Namshukuru pia kwa kuwateua Wakuu wa Mikoa wanawake, ma-*RAS* na pia Balozi mwanamke ambaye kwa muda mrefu tulikuwa hatujapata Balozi mwanamke.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii pia kuleta salaam na shukrani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoka kwa wananchi wa Wilaya ya Makete na Mkoa wa Iringa kwa ujumla kwa jinsi alivyolishughulikia tatizo lililojitokeza katika hospitali ya Bulongwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Iringa aliahidi kwamba atalishughulikia tatizo hili kwa haraka iwezekanavyo hata kama kwa kumtuma Waziri kwa kukodi ndege, napenda kutoa taarifa kwamba alifanya hivyo kwa kukodi ndege kwa kumtuma Waziri wa Afya kwenda kuangalia tatizo katika hospitali ya Bulongwa na tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kukupongeza kwamba Waziri uliyemtuma alifanya kazi nzuri sana mpaka usiku na tatizo hilo sasa limekwisha. Pongezi hizi ni pamoja na kwa watu waishio na Virusi vya UKIMWI wanashukuru na mashine sasa imenunuliwa ya kwenda kuhudumia wananchi kule, tunaomba tukupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kukushukuru.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kuzungumzia suala la afya. Napongeza juhudi zinazofanywa na Serikali kuboresha huduma za afya lakini bado tunahitaji kufanya zaidi. Sasa hivi tulivyokaa hapa toka asubuhi kila dakika inayopita mwanamke mmoja au msichana anafariki hapa nchini kwa tatizo la huduma za afya hasa wakati wa

kujifungua, wanawake kama taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inavyosema wanawake 578 kati ya wanawake 100,000 wa Tanzania wanakufa kila mwaka kwa tatizo la uzazi hii ni sawa na kusema kwamba karibu kila saa moja inayokwenda hapa nchini mwanamke mmoja au msichana aliyezaa katika umri mdogo anafariki kwa matatizo ya ujauzito au wakati wa kujifungua au anapata kilema cha kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia hili ina maana kwamba tunahitaji kufanya la ziada, sasa hivi ningeshauri Serikali iangalie uwezekano wa kujenga *ward* nyingi za wanawake kujingojelea hasa wale wanawake wenye matatizo katika kila Hospitali ya Mkoa na Hospitali ya Wilaya na katika Hospitali zilizoko pembezoni au Wilaya zilizoko pembezoni na Vituo vya Afya pia viwe na maeneo ambapo wakina Mama wajawazito wanaweza kukaa wale wenye matatizo. Tunaelewa kwamba wanapohudhuria kliniki kadi zao zinawekwa alama kwa akina Mama wale wote wenye matatizo sasa tusingoje mpaka dakika ile wanakwenda kujifungua ndiyo wapelekwe hospitalini tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka *ward* ambazo akina Mama hawa wakati wakingoja siku zao za kujifungua kufika.

Lakini pia tunaomba hospitali ambazo ziko pembezoni ziangaliwe kupewa *ward* za akinamama za kujifungulia, narudia kusema na niliwahi kusema na ninaomba nirudie kusema *ward* za wazazi Hospitali ya Wilaya ya Ludewa leo ni mwaka wa tatu *ward* hii haijaanza kutoa huduma. Wanawake wa Wilaya ya Ludewa wanajifungulia kwenye chumba kidogo, kitanda kimoja tufikirie kama wanawake watano wanaumwa uchungu wanahitaji kujifungua kwa wakati mmoja watajifungulia wapi? Kama siyo kuongeza vifo vya akinamama wajawazito. Mimi naomba hospitali ijengwe.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Mizengo Pinda, amekuwa mstari wa mbele kuangalia suala hili na ninamshukuru na kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa kuweza kuchangia pia ujenzi wa *ward* ile, naomba uharakishwe na baada ya hapo tuweze pia kupata *Ambulance* ambayo inaweza kutumika na iwe ni gari ambayo inamudu mazingira ya Wilaya zinazohusika na ninafikiri gari kama *hardtop* likiwekwa vifaa vyote linaweza kusaidia kuweza kuhudumia akinamama wale wanaoweza kujifungua na wenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nashukuru jitihada kubwa zinazofanywa za kuweza kuboresha Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake, lakini tunahitaji kufanya ziada, tunazungumzia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ili waweze kuondokana na umaskini na kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania, tunaelewa kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii ndiyo yenye wataalam wale waliofundishwa mbinu za kuhamasisha jamii kama hatutawezesha Wizara hii hayo tunayoyazungumza wananchi huko vijijini hawataweza kuelewa kama Maafisa Maendeleo ya Jamii hawatakuwepo katika kila Kata ya nchi hii kwa hiyo tuongeze jitihada za kuhakikisha kwamba Maafisa Maendeleo wanapatikana kwenye haya maeneo na pia kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii niliwahi kuzungumzia suala la kuwa na idara maalum inayoshughulikia watoto, naipongeza Serikali kwa sababu iliunda Wizara hii lakini Wizara hii bado inahitaji kuboresha kitengo hiki, kwa maoni yangu naishauri

Serikali sasa ni wakati umefika wa kuunda kamisheni maalum ya kushughulikia masuala ya watoto nchini. Kama  tulivyounda tume nyingine tume za kushughulikia Haki za Binadamu, Tume ya Kushughulikia Dawa za Kulevya na Tume mbalimbali.  *(Makofi)*

Sasa  namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie uwezekano wa kuunda Tume ya kushughulikia masuala ya watoto. Tuna watoto ambao sasa kwa matatizo mengine wapo Wizara ya Afya, wengine wako Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana  na wengine Wizara mbalimbali.

Sasa mimi nafikiri kwamba kama tutaunda tume, kamisheni itatengenezwa ambayo itashughulikia masuala ya watoto kwa  hiyo, watoto wote watakuwa katika idara moja na Wizara moja ambayo uratibu huu utakuwa chini ya Wizara mama,  Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa hiyo watoto wenye ulemavu wataangaliwa, watoto waishio kwenye mazingira magumu, watoto walioko kwenye magereza yaani mama zao wako magerezani na watoto pia wataweza kuangaliwa na watoto ambao wako shuleni wataweza pia kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kilimo. Naipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali zinazofanywa ili kuboresha kilimo, lakini tunahitaji kufanya zaidi katika suala la kuboresha kilimo wataalam wa kilimo na  ugani wanahitaji kupata nyenzo ili waweze kufanya kazi. Wanafanya kazi katika mazingira magumu Wilayani na Vijijini, ili waweze kuwa kweli wataalam ambao wanaweza kutoa utalaam vizuri kwa wananchi tunaomba tuboreshe mazingira yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba Serikali iangalie uwezekano wa kupandisha Chuo cha Kilimo Uyole ili kiweze kutumika kutoa wataalam wa ngazi za juu ikiwemo wataalam wanaoweza kupata *degree* pamoja na *diploma* za juu ili tuwe na wataalam wengi wa kilimo wenye elimu iliyo bora zaidi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la UKIMWI. Naipongeza Serikali yangu kwa juhudi kubwa inayofanya na hasa kuhakikisha kwamba wale wagonjwa ambao wako kwenye kupatiwa dawa wanapata dawa za kurefusha maisha ili kuhakikisha kwamba tunapunguza idadi ya watoto yatima lakini pia kupunguza wafanyakazi wengi kufa na kama watapewa dawa wataishi muda mrefu.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri sasa ni wakati wa sisi viongozi hasa Wabunge wenzangu nawaomba tuungane na Serikali katika kuhakikisha kwamba tunapambana na tatizo la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kwa juhudi ambayo amezifanya kuanzisha kampeni mahsusi ya kusaidia vijana  na kwa maudhui yanayosema Mtoto wa Mwenzako ni Mwanao Mkinge Dhidi ya UKIMWI. Sisi wote tuangalie hili na ninaomba tusizungumzie mjadala wa silaha zinazotumika katika mapambano haya.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonyesha nchi mbalimbali zilizofanikiwa katika masuala ya UKIMWI wametumia silaha mbalimbali kwa  hiyo naomba wote tuungane na

tushirikiane katika kutatua tatizo hili na ninaomba Tume ya Kudhibiti UKIMWI ipewe ofisi kubwa ili iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba *Social Action Trust Fund* ambayo ni *NGO* ya Kitaifa iliyoweza kuhudumia watoto 135,000 katika miaka sita imetumia shilingi bilioni 1.4 kusaidia watoto yatima iweze kupewa nafasi ya watu mbalimbali wanaochangia mfuko huu au *NGO* hii wapunguziwe kodi kama vile wale wanaochangia yatima wapunguziwe kodi kama vile ambavyo tunapunguza kodi kwenye masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nizungumzie suala la miundombinu kwamba ili tuboreshe kilimo tunahitaji kuwa na barabara ambazo zinapitika vizuri na tunapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali.

Kuhusiana na fedha zilizotengwashilingi milioni 500 kila Mkoa ninashauri kwamba fedha hizi pia ziangaliwe kuwafikia wanawake ili waweze kupata mitaji na ninapongeza wanawake wa Mkoa wa Iringa ambao wameanzisha *SACCOS* zao na sasa hivi wameanza kukopeshana na nina hakika kwamba fedha hizi pia zitaanza kuwafikia na zigawiwe kwa Wilaya pia mwaka kesho tuangalie pia ukubwa wa mkoa tusiangalie tu kila mkoa kupata milioni 5 tuangalie ziko wilaya ngapi katika ule mkoa ili tupate mgao sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la elimu, sasa hivi Serikali imetangaza ajira kwa walimu, naomba pia tuangalie uwiano wa wale watakaokwenda kwenye vyuo hivi ili tuhakikishe zile ajira zinapatikana kwa kila Mkoa kama vile na Polisi, Magereza wanavyofanya kutenga nafasi kwa kila Wilaya tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mama Margaret Sitta, mama yetu aangalie uwezekano wa kila Wilaya kutengewa hizo nafasi ili tuhakikishe kwamba tunapata uwiano wa hizi nafasi.

Mheshimiwa Spika, watoto yatima waliomaliza shule za sekondari waangalie kupewa hii nafasi tusizingatie tu kwamba waliopata *Division I* au *II* watoto hawa wanasoma katika mazingira magumu tuwaangalie kwamba wale waliofaulu hata kama wana *Division IV* basi na wenyewe waangaliwe kupewa nafasi za mafunzo katika vyuo mbalimbali vilivyopo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wenzangu wa Bara la Afrika walioniamini na kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kwanza wa Umoja wa Wabunge wa Bara la Afrika wa Kupambana na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ambayo umekuwa ukinipa na kunisaidia na nina uhakika Ofisi ya Waziri Mkuu itanipa ushirikiano mkubwa kwa sababu ni heshima ya nchi yetu kuwa nchi ya kwanza katika Bara la Afrika kuweza kushika nafasi hii kubwa na Mkutano wa kwanza wa Wabunge wa Bara la Afrika wa kupambana na UKIMWI utakuwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, tunaendelea kukupongeza kwa nafasi yako hiyo, kama mwanaharakati wa kupambana na UKIMWI. Sasa umetambuliwa na Afrika nzima na tunatazamia utatambuliwa na Dunia nzima. Namwita sasa Mheshimiwa Felix Kijiko, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Clemence Lyamba. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, ili nami niweze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ambao wameweza kuchangia hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni hotuba ambayo kusema kweli imejieleza, haina haja kujadiliwa kwa sababu kilichoandikwa mle ndani, kinaeleweka na bahati nzuri, watu waliopewa hiyo hotuba waisome na kupitia ni Waheshimiwa Wabunge, ambao wana uwezo wa kutosha wa kusoma na kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa alioupata majuzi, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama Tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa ushindi alioupata kwa sababu safari iliyopita sikupata nafasi ya kumpongeza. Lakini leo nachukua nafasi hii, kumpongeza kwamba, ulikuwa pia ni ushindi wa kishindo na hiyo inajidhihirisha wazi kwa jinsi anavyotuongoza. Humu ndani tunakwenda vizuri, kwa *speed* inayotakiwa na wewe Spika ukiwa pale pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sikumtendea haki, Naibu Spika wako, Mheshimiwa Mama Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na uwezo unaotuonyesha kwamba, kweli akinamama nao, wana uwezo wa kusimamia Bunge humu ndani na likaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa hotuba aliyoitoa. Kweli ile bajeti ilikuwa kubwa kabisa inayojieleza na aliileta kwetu na sisi tukaipitisha, sidhani kama kuna kitu kingine kitajitokeza kukwamisha bajeti ile na huo ndio mwelekeo wa Serikali tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, labda nitakacho kizungumza sasa ni salamu kutoka kwa wale wana-Kibondo, wana-Muhambwe na wana-Buyungu, walichonituma kuja kukizungumza katika Bunge hili. Wana-Kibondo walinituma nifikishe salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu baada ya ajali iliyotokea ya gari kugongana na lori, wananchi 12 walipoteza maisha yao na Serikali haikuwa nyuma kwa kwenda kuwahani wafiwa. Mimi Mbunge nilitumwa kwenda

kufanya hiyo kazi kwa niaba ya Serikali na nilipokelewa vizuri sana. Wanatoa shukrani sana wale Waha wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, sasa nirudi tu moja kwa moja kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wilaya ya Kibondo ni Wilaya ambayo iko mpakani Mkoani Kigoma kule na ni Wilaya ambayo inapakana na nchi ya Burundi. Tunapakana kwa sababu ukiangalia ule mpaka ambao unatenganisha Wilaya ya Kibondo na Wilaya ya Burundi, ambayo iko jirani sana na Kibondo ni mto, kwa hiyo, tuko mpakani sana. Lakini ni Wilaya ambayo imekuwa na wakimbizi wengi. Kibondo inayo makambi manane na ni makambi ambayo yanahudumia wakimbizi. Lakini wana-Kibondo wanafaidika na huo utaratibu wa kuhudumia hao wakimbizi, kwa sababu huduma nyingi ambazo zinatolewa kule Kibondo zinawagusa pia wananchi wa Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo ambayo yapo nikija kwenye Huduma ya Afya ni kwamba, Wilaya ya Kibondo inafaidika sana kutokana na kuhudumia wakimbizi ambao wanalazwa kwenye hospitali ya Wilaya. Wananchi wa Wilaya ya Kibondo wanafaidika kutokana na huduma ambayo inatolewa na Shirika la *UNHCR.*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatendea haki kama sikulipongeza Shirika linalohudumia wakimbizi la *UNHCR.* Kule Kibondo mambo mengi ambayo kusema kweli wananchi wanafaidika nayo yanatokana na hilo Shirika la Umoja wa Mataifa na wanafaidika kwa sababu nia na madhumuni ya Shirika hilo huwa ni kuhudumia wakimbizi. Lakini wale Waha wenzangu wanajikuta kwamba, wanaangukia humo kwa kupata ama kufaidika na huduma hizo zinazotolewa. Kwa hiyo, napenda kulishukuru sana Shirika la Umoja la Mataifa kwa huduma zinazotolewa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna kipengele kinachoeleza kuhusu kujenga maslahi na mahitaji ya makundi maalum katika jamii. Mimi naungana kabisa na hilo na vikundi vimeelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini labda ningetoa ushauri kidogo kuboresha hicho kipengele.

Mheshimiwa Spika, hayo makundi ni makubwa kiasi kwamba, sasa kitu ambacho kingeweza kusaidia sana ili kuwahakikishia wananchi kwamba kweli nia ya Serikali ni kusaidia hayo makundi, basi ilikuwa ni kupata wahamasishaji. Serikali kwa makusudi mazima, iandae wahamasishaji ambao watakwenda huko kuanzia ngazi ya Wilaya mpaka ngazi ya Mkoa ili kuhakikisha kwamba, hayo makundi maalum ambayo yanatakiwa kuhudumiwa na Serikali, yanapata huduma hiyo. Wapate elimu ya kutosha ya kuweza kujua kwamba, Serikali sasa imetangaza vita kuwasaidia kuhusu maendeleo ambayo yanaweza kuwasaidia kama makundi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye kipengele cha barabara, ni kama nilivyosema kweli kwamba, Wilaya ya Kibondo ni Wilaya ambayo iko mpakani. Ni Wilaya ambayo napenda kusema kwa masikitiko makubwa kwamba, ni Wilaya ambayo ilikuwa imesahaulika sana. Ninashukuru sana kwa hatua ambazo Serikali ya Awamu ya Nne

imezichukua kuhakikisha kwamba, mpaka wa Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake tatu, utafunguliwa sasa. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa sababu mpango wa Serikali sasa ni kuwapatia wananchi wa Mkoa wa Kigoma barabara ya lami, ambayo itatoka Kigoma kwenda mpaka Nyakanazi, ikipitia Kasulu mpaka kule Kibondo. Kwa hiyo, wananchi wa maeneo hayo watafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia habari ya barabara ya lami kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma, afadhali Kigoma Mjini angalau wamewahi kuwa na barabara ya lami, lakini imekwisha haribika kutokana na kuwa ya muda mrefu. Lakini ukienda Kasulu mpaka Kibondo, ukamwambia mwananchi akueleze lami ni kitu gain, atashangaa. Nakumbuka katika miaka ya nyuma kuna watu walikuja kujenga daraja linaitwa Daraja ya Mto Malangarasi, wakaweka lami kama mita 50 hivi, wananchi walikuwa wanatembea kwa miguu maili 40 kwenda kuangalia hiyo lami nyeusi ambayo imewekwa pale na magari yanapita ilikuwa lami ya namna gani, lakini ilikuwa ni lami!

Sasa tunapozungumzia barabara ya lami itajengwa kutoka Kigoma kwenda mpaka Nyakanazi, nadhani ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi wa kule Kibondo. Hiyo ni hatua ambayo Serikali itaichukua. Kwa hiyo, tunaishukuru sana na mimi ninaishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wa kule Kibondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nije sasa kwenye barabara za Vijijini. Barabara za Vijijini ni kwamba, hakuna. Lakini katika Wilaya ya Kibondo au Mkoa mzima wa Kigoma kwa ujumla ni miongoni mwa Mikoa ambayo haikutetereka kutokana na baa la njaa, ambalo lilijitokeza mwaka 2005 na ambapo mpaka sasa ni kitendawili kikubwa sana. Ina maana wananchi wake ni wenye moyo na kupenda maendeleo ya kilimo. Sasa tatizo ambalo linawakabili wananchi ni kuboreshewa barabara zao ili waweze kusafirisha mazao yao kutoka Vijijini na kufikishwa Mjini. Mahali ambapo mkulima akiyafikisha mazao yake ataweza kuuza na kuweza kupata uwezo wa kununua mafuta ya taa ama sukari. Lakini ukienda Vijijini ni kwamba, barabara ni mbovu, hakuna madaraja na barabara ambazo zipo hazipitiki, lakini hizo ni barabara ambazo zinajitegemea kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitapenda nitaje barabara ambazo kusema kweli zimekuwa ni kero kubwa sana, lakini ni barabara zinazounganisha vijiji ambavyo vinajiendesha kwa kilimo na ni wakulima wakubwa sana. Kuna barabara ya kutoka Kifula-Kichanagana-Mabamba haipitiki, lakini wananchi wa kule wanalima sana na wamekwama na mazao huko. Kuna barabara ya kutoka Mgunzu-Katanga-Kasongati mpaka Kinonko kule kuna mazao mengi lakini wananchi wanashindwa kusafirisha hayo mazao kule vijijini na kuyafikisha kwenye soko. Kuna barabara ya kutoka Kibondo Mjini kwenda Makao Makuu ya Kata inayoitwa Murungu hadi Kumbanga, hii barabara inakwenda mpaka kwenye Hifadhi, lakini haipitiki na wananchi wa kule ni wakulima. Wananchi wa kule wana asali nyingi sana, wanatakiwa wasafirishe hiyo asali kutoka porini kuileta huku Mjini, lakini barabara haipitiki. Kuna barabara ya kutoka Kifula-Nyaruyoba hadi Kigogo ambayo inasikitisha kwa kutokupitika kabisa.

Mheshimiwa Spika, hizi barabara zina umbali mrefu; barabara ya kwanza ina kilomita 48, barabara nyingine ina kilomita 54 na barabara ya tatu ina kilomita 33. Hii barabara niliyoitaja ina kilomita 28 na barabara ya mwisho inayotoka Kabale kwenda Rumashi hadi Nyabibuye ina kilomita 22. Kwa masitikiko nasema kwamba, hizi barabara uwezo wa Halmashauri hauwezi kuzitengeneza isipokuwa kilomita 40 tu. Lakini ukijumlisha kilomita za barabara hizo ni nyingi zaidi ya uwezo wa Halmashauri. Sasa mimi nilikuwa naomba kwamba, kusema kweli hizi barabara zingeweza kuboreshwa kwa kuiongezea nguvu Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ili wakulima waweze kufaidika kwa kusafirisha hayo mazao kutoka mashambani na kuyafikisha kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la umeme. Kuhusu suala la umeme pia napenda kuipongeza Serikali kwa hatua ambazo zimechukuliwa. Lakini pongezi za pekee zimfikie Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kazi ambayo ameifanya, ni kubwa sana na nina hakika kama atafunga safari kwenda kule Kigoma, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, atabebwa na wale Waha kule. Kwa sababu wamefurahi sana kwa hatua ambazo umezionyesha za kutaka kumkomboa huyo mwana-Kigoma. Naishukuru sana Serikali, kwa sababu najua kuna mkono wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la maji katika Wilaya ya Kibondo na limetajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kubwa sana na hili tatizo nimelikuta mimi na nimeingia kwenye siasa juzi tu. Lakini wakati napita vijijini kwenda kuzungumza na wananchi nikiwaomba kura, nimeweza kuwakosa baadhi ya akinamama kwa sababu walikuwa wanaamka saa tisa usiku kwenda kuchota maji umbali wa maili kumi ndiyo waje kuwahi mkutano wangu, lakini walishindwa kuhudhuria baadhi ya mikutano yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala la maji linalozungumziwa, sijasikia mahali panazungumzwa kwamba, mwana-Kibondo au mwana-Kigoma naye ana matatizo ya maji. Mimi nina tatizo hilo kubwa sana, maji kwangu mimi ni kitendawili, hata pale Mjini tu mahali ambapo kuna Mashirika mengi, wageni wanafikia hapo, lakini tatizo la maji lipo. Tunakosa maji kwa muda wa wiki mbili Mjini, lakini tatizo hilo lingeweza kutatulika kama Serikali itaamua kutusaidia katika hilo. Kwa jitihada zangu, nimejaribu kuwaomba Wahisani, Shirika la Kimataifa linalohudumia Wakimbizi, waweze kutusaidia kwa kutumia kigezo kwamba, kuna wakimbizi ambao wanakuja kulazwa hapo katika hospitali ya Wilaya, wanajitahidi lakini katika kujitahidi walikuwa wanataka waone nguvu ya Serikali nayo inalitatua hilo namna gain, kuliko kutegemea kuomba omba kwa hayo Mashirika makubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo tatizo la maji nimelizungumza hivyo kusema kweli limekuwa ni kero kubwa sana katika Wilaya Kibondo na ninakumbuka hata wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais wetu, akiwa ni mgombea, alikwenda kule akashangaa alipoambiwa Makao Makuu ya Wilaya hayana maji. Sasa kwa sababu aliambiwa na ninaamini kabisa kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, naomba anisaidie sina maji kule, wale Waha watanimaliza, nisaidie nipata maji. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati ukiwa Waziri wa Maji na Maendeleoya Mifugo, ulionyesha jitihada za

kuwapatia maji kutoka Mwanza kuja mpaka Shinyanga, kwa nini maji yale yasiende mpaka kule Kibondo na yale maji ya Ziwa Victoria hayatakwisha?

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Hifadhi. Kibondo imezungumzwa ina Hifadhi na kweli watu ambao waliwahi kule wana *plot* kubwa na wanafaidi sana. Lakini mwana-Kibondo hafaidi kitu kutokana na mbuga hizo. Hafaidi kitu kwa sababu hata mtu wa kufyeka majani anakuja na mtu aliyepewa *plot*. Yule mtu wa kawaida wa Kibondo ambaye angeweza kwenda kufyeka majani akalipwa hela ili aweze kununua chumvi, hapewi nafasi hiyo. Nilikuwa naomba utaratibu huu ubadilishwe.

Mheshimiwa Spika, lakini mbaya zaidi, nina kijiji kimoja kinaitwa Kubanga, kina mto mkubwa sana ambao umo ndani ya Hifadhi na huo mto una chumvi. Hao watu tangu enzi na enzi, hawajahi kwenda kununua chumvi ambayo inatoka mahali pengine, wanatumia chumvi inayotoka kwenye mto huo. Lakini kwa sababu huo mto upo kwenye *plot* ya mtu, basi kuna ulinzi mkali sana kiasi kwamba, wananchi kwenda pale wanashindwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa asilimia mia moja na kumi. *(Makofi)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nami niungane na wasemaji wote walionitangulia ili niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru nawe pia kwa kuniweka kitinda mimba kwa mchana huu kuwa msemaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi za pekee kwa hotuba nzuri iliyosheheni maelekezo yanayoendana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyoiwasilisha hapa Bungeni. Ni dhahiri natambua kutakuwa na nafasi nzuri zaidi wakati wa *presentations* ya hotuba za kila Wizara, kuchangia kwa masuala mbalimbali niliyonayo. Lakini leo nitayazungumza kwa ujumla kwa vile ni vyema yakasikika tangu mwanzo, halafu yakafuatiliwa baadaye na wananchi wa Jimbo la Mikumi wana hamu sana na shauku, kusikia yale waliyonituma ninayatamka tangu awali.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kutoa pongezi kwa Mawaziri waliotangulia, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa hotuba nzuri za utangulizi na ambazo zimeoana kabisa na maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amedhihirisha tena kweli kwamba, wanawake wanaweza na tuwape nafasi. Kwa hakika kama ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi, naamini tumeshawapa nafasi. Lakini kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya, wanayoonyesha kwenda nayo akinamama, si ajabu katika muda mfupi watakuwa asilimia 70, basi watukumbuke akinababa kutupa viti maalum huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, pamoja na viongozi wote wa Sekretarieti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi kwa *Cabinet* nzima, kwa jinsi walivyokuwa machachari kufuatilia kero ambazo wananchi kwa kweli zinawagusa lakini wanashiba tayari kwa yale ambayo wanayatekeleza kuondoa kero zao.

Mheshimiwa Spika, shukrani pia ziende kwa wale walioandaa Ilani ya Uchaguzi, kwa sababu ni kwa sababu hiyo wametufanya sisi wengi tuweze kuwa katika Bunge hili. Bila kumsahau msanii maarufu Mheshimiwa Capt. John Komba, ambaye alihamasisha sana umma kwa nyimbo zake, kutufanya wote tuweze kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati, kwa wapiga kura wa Jimbo la Mikumi, ambao pasipo wao na imani yao kwangu, nisingefanikiwa kuwa Bungeni katika Serikali ya Awamu ya Nne, yenye ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze katika masuala yote yanayohusu kero, lakini kwa bahati nzuri yameainishwa katika Ilani ya Uchaguzi. La kwanza kabisa, ni barabara. Barabara kati ya Mikumi na Kilosa kupitia Handeni/Dumila na hadi Korogwe. Tunaishukuru Serikali na wananchi wa Jimbo la Mikumi, wanatoa pongezi sana kwa Serikali kuona umuhimu wa barabara hiyo. Barabara hii italeta changamoto na kufufua kilimo katika Ukanda mzima kutoka Mikumi hadi Kilosa. Kwa maana kwamba, wakulima ni wengi wanaolima mpunga, sehemu nyingine mara mbili kwa mwaka, wanalima mahindi mara mbili na sehemu nyingine hadi mara tatu kwa mwaka. Kwa hiyo, barabara hii itakuwa kwao ni ukombozi kwa kusafirisha mazao yao ya biashara.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kati ya Mikumi na Kilosa katika Kata za Ulaya na Zombo, pamoja na Masanze kuna mto Miyombo na mto Zombo ambayo inaambaa, pungufu ya robo kilomita kutoka mahali ambapo barabara ya lami itakapokuwa imejengwa. Ili mazao yaweze kuja katika barabara hii na kuyasafirisha, inabidi madaraja ambayo ni sugu na magumu kuyajenga kwa sababu ya mafuriko ya kila mwaka, yanahitajika. Tunaiomba Serikali, iingize gharama za ujenzi wa madaraja hayo muhimu ili tuweze kuhakikisha kwamba, mazao yanayolimwa na wakulima yanafika barabarani na kusafirishwa kupelekwa katika maeneo ya biashara. Haya ni katika Mto Nyameni, pamoja na Mto Kisuru, ambapo panaitwa barabara ya Nyameni kwenda kwa Wangoni, kuna Wangoni wamekaa watupu pale, kuna kisiwa cha Wangoni.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna daraja la Mto Zombo, nalo ni muhimu sana katika suala hili. Sababu ya kuomba fedha maalum zitengwe kwa ajili hiyo kutoka Serikali Kuu ni kwa ajili ya ugumu wa ujenzi au *complexity* ya ujenzi wa madaraja yale. Kwa sababu ya mafuriko makubwa ya kila mwaka Halmashauri haitamudu kuwa na fedha za kutosha kuyajengwa madaraja hayo.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu barabara hiyo tunaomba Serikali itupe ratiba kwa *section* kutoka Mikumi mpaka Kilosa, Kilosa mpaka Dumila, Dumila mpaka

Handeni na Handeni mpaka Korogwe. Ratiba yake ya ujenzi na usanifu na kadhalika itakwenda vipi? Ili iwe rahisi sisi kufuatilia na kuona jinsi maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo inavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ombi wakati wa usanifu, nafikiri umekwishaanza na upembuzi yakinifu ingekuwa ni jambo la busara iwapo Serikali itakubali kuyashirikisha Mabaraza ya Maendeleo ya Kata katika *centres* za vijiji inapopita barabara hiyo ili waweze kutoa mapendekezo na hasa wanapokaribia Mji wa Kilosa, kuepuka kukwepa vijiji ambako kuna *centres* za biashara ambapo ingerahisishia wakulima kuwasafirisha mazao yao katika barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikizungumza kuhusu barabara licha ya barabara hii ya lami ambayo tunaishukuru Serikali kuipanga, napenda nizungumzie kuhusu Kata mbili ambazo kwa hakika katika Jimbo la Mikumi ni kama yatima. Hii ni Kata ya Vidunda na hasa hasa Kata ya Uleling'ombe. Kama ilivyosemwa katika Taifa kuna Majimbo au Mikoa ambayo ipo pembezoni, Kata hizi mbili ya Uleling'ombe na Vidunda, zipo milimani juu kabisa kama Milima ya Upare vile. Kwa kiasi fulani inaelekea Serikali imewasahau wananchi katika maeneo hayo, tatizo kubwa ni barabara. Niliwahi kuzungumza wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa kweli Serikali Kuu tunaomba itupie jicho wananchi wa Uleling'ombe, wameachwa pekee yao, huduma za jamii hazifiki haraka.

Kutoka Mikumi inabidi uende kilomita 150, ukifika Malolo inabidi upande milima mirefu kwa kilomita 25, itakuchukua saa nne na nusu na sehemu nyingine barabara ni mawe matupu na majabari. Hali kadhalika kwa kiasi kifupi kidogo zaidi, Vidunda. Uleling'ombe nikizungumzia juu ya huduma finyu wako watu 4,000. Katika Kata ya Uleling'ombe, zipo shule tatu, mbili zina mikondo mitatu' wanafunzi 570 na ile shule moja wanafunzi 320 mkondo mmoja. Mahitaji ya walimu ni 25, pungufu walimu 18, watu hawana hamu kwenda Uleling'ombe, wanaokwenda hawakai. Naomba Serikali itupie jicho Uleling'ombe na Vidunda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongezea kwa sababu ya upweke wa maeneo haya yaliyotengwa, nimeanza majadiliano na viongozi wa *VODACOM* na *Celtel*. Lakini tunaomba kwa sababu mawasiliano ni mbaya mno, angalau basi *improvement* katika *communication*, kupeana taarifa, masuala mengi yanakwenda kwa *communicatio*n.

Naomba Serikali isaidie kusukuma viongozi wa taasisi hizi za mawasiliano ili tuweze kupata *attention* haraka iwezekanavyo. Kwa sababu wako milimani na maeneo yale ya milima yana *overlook* kata nyingine zote. Ukiwekwa mnara mmoja kule juu, utatawanya mawasiliano katika sehemu zote. Usiku wa jana Diwani wa Uleling'ombe alinipigia simu akiwa katika milima ya Ukwivya, amepanda kule ili apate mawasiliano. Ina maana ukiwekwa mnara kule wananchi wale wameokoka.

Mheshimiwa Spika, sikujua kama muda unakimbia kiasi hiki, nije kwenye mazingira. Mazingira ni suala muhimu katika nchi yetu na athari zake wote tunazijua. Mji wa Mikumi au Mji Mdogo wa Mikumi, wakazi wake hawana sehemu ya kulima kwa

sababu wamepakana na milima karibu pande zote isipokuwa upande wa *National Park*. Hivi karibuni katika zoezi la kutaka kurekebisha mipaka, viongozi wa *National Park* walianza kupima mipaka tofauti na maagizo yaliyomo katika *Government Notice* Namba 121 ya tarehe 13 Juni, 1975.

Mheshimiwa Spika, ombi, Serikali isaidie watakapokuja kurekebisha mipaka, kipaumbele kitolewe kuwawezesha wananchi wa Mikumi kupewa nafasi angalau kiasi fulani kusogea ili waweze kupata maeneo ya kujiendeleza kiuchumi, pamoja na MKUKUTA. Hiyo inagusa maeneo ya Ruhembe, Kidodi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kushauri kama inawezekana Serikali iandae Mkakati Maalum na wa kipekee wa kuanzisha au kueneza nishati mbadala ya jua kwa vijiji. Wanavijiji wote wanategemea kwa kweli kuni na mkaa, angalau basi nishati mbadala ya mionzi ya jua kwa majiko tu yanayoweza kutumika kwa kupikia yasambazwe katika vijiji ili kuepuka ukataji wa miti na shauku ya kutumia mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fungu la barabara kwa Halmashauri ya Kilosa, naomba liongezwe kwa sababu eneo lote la Bonde la Kilosa na mpaka Mikumi ni bonde ambalo maji yake yanatiririka kutoka milimani katika milima hiyo ya Udzungwa, Usagara na Ukwivya. Tunashukuru wakati wa mafuriko Ruaha, Mheshimiwa Makamu wa Rais, alitutembelea na kutoa pole kwa wananchi na kutoa *offer* ya shilingi milioni nane kuwasaidia wananchi walioumia. Tunashukuru kwa hilo, nami niko mbioni kuzifuatilia hizo fedha kwa sababu huu ndiyo wakati wa kufanya *repairs. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya mafuriko ya kila mwaka, kama yale yaliyotokea ya *El-Nino* na kuvunja daraja pale Kilosa na ambalo mpaka hivi leo halijatengenezwa na sasa hivi Kilosa magari yanapita kwenye daraja ambalo treni inapita na watu wanapita hapo hapo, treni inapita hapo hapo na mifugo inapita hapo hapo, ni hatari. Tangu wakati wa *El-Nino* mpaka sasa, hakuna kilichofanyika, tunaomba Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafuriko yanayoenea katika Kata za Mabwelebwele, Kilangali, Muungano, Zombo, kote kule kunahitajika kwa kweli tupate vifaa vya uhakika. Naomba Serikali itoe angalau *excavators* mbili kwa Halmashauri ya Kilosa na greda moja kwa sababu mafuriko haya yanarudi kila mwaka. Kwa sababu *system* ya *drainage* imeshaharibiwa na mazingira, kwa hiyo, maji yanakwenda yanatapakaa na kuvunja nyumba za watu. Njia pekee ya kurekebisha hali hii ni *river training* na *drainage* katika maeneo hayo ili maji yafuate mkondo unaostahili na kuepusha kuvunja nyumba na kuleta vifo wakati wa mafuriko.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mikumi una matatizo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, anakumbuka pengine kilichotokea Mikumi, bado kinaendelea na kwa sababu na mimi ni mgeni, hata naona Wilaya imeshindwa kupata ufumbuzi wa tatizo lile. Naomba msaada maalum ili tulete ari ya wananchi kukubali uongozi utakaowekwa madarakani, kwani uliopo haukubaliki na

hauko na watu, haujasoma mapato na matumizi na unajifanyia vitu unavyotaka wenyewe. Naomba msaada huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakulima wa miwa, ndugu yangu Mheshimiwa Castor Ligallama, alilizungumzia. Lakini ni muhimu nitamke kitu alichosahau kutamka kwamba, *TRA* imekuwa inawa-*charge* au inawatoza kodi wakulima wa miwa, *on gross revenue*, siyo *on net of expenses*, gharama za uzalishaji. Ni kitu ambacho kwa kweli ni kama kuwaonea wakulima na kuwavunja moyo, pia *TRA* inabagua. Wakulima wadogo wakiwa na vifaa vyao vya kupakia miwa na kusomba wanatozwa *VAT*, kampuni ikipakia yenyewe au wakulima wakubwa wakipakia miwa wenyewe, hawatozwi *VAT*. Kwa hiyo, hili kwa kweli inabidi litazamwe kwa undani zaidi ili kuondoa adha hii inayowasibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho, ombi maalum, tulipata semina Waheshimiwa Wabunge, tulizoshiriki katika maboresho. Ninaomba yale majumuisho yatakayokuwa yanafanywa au kama yameshafanywa, tupewe Waheshimiwa Wabunge *draft* ya majumuisho yale ili tuweze kuona yale tuliyoyaeleza kama ni kero, kama kweli yamekaa katika ile hali ambayo tuliona kwamba, inafaa ili kuondoa adha na kuleta ufanisi. Kwa mfano, tulipendekeza Waheshimiwa Wabunge, tuwemo katika *Board* ya *Tender* za Halmashauri kwa sababu kiutaratibu kwa sasa tunaambiwa hatustahili kuwemo, lakini mambo yanavurugwa kule.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache. Kwanza, wale Waheshimiwa Wabunge, ambao wana mazungumzo na Kampuni ya *Toyota Tanzania Limited*, wanaombwa na viongozi wao Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Vita Kawawa, wakutane katika ile sebule ambapo huwa tunachukulia barua. La pili, ninayo orodha ya wachangiaji 17. Lakini nitakaoweza kuwapa nafasi kwa leo ni Waheshimiwa Wabunge 11 na kesho Waheshimiwa Wabunge wanne, kwa sababu uchangiaji hoja nitaifunga saa tano kamili asubuhi ili kutoa nafasi kwa yote yaliyosemwa, wiki nzima hii, kuweza kupata majibu kutoka kwa Serikali.

Sasa ili Waheshimiwa Wabunge, mjipange vizuri, naomba niwataje, saa 11.00 jioni tutaanza na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, afuatiwa na Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Anna Komu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Anastazia Wambura na atamalizia Mheshimiwa Eliatta Switi. Kwa hiyo, kesho asubuhi tutaanza na Mheshimiwa Fatma Mikidadi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Mkapa, halafu Mheshimiwa Savelina Mwijage na atakayemalizia mjadala huo wa hoja ya Mheshimiwa Waziri ni Mheshimiwa John Shibuda.

Sasa baada ya hapo, mpangilio wa Serikali ni kama ufuatavyo, kama tulivyokubaliana na Serikali. Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, kesho saa

tano atatoa majumuisho, kwa yale ambayo yeye ameandaa na yanayomhusu kwa dakika 30. Atafuatiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Celina Kombani, dakika 15. Baada ya hapo atakuja Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Juma Akukweti kwa dakika 30 na atamalizia bosi wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa dakika 45, ambaye anasimamia moja kwa moja. Kwa hiyo, nitasitisha Shughuli za Bunge saa 7.00 mchana.

Kwa hiyo, saa 11.00 jioni nitamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ataendelea nadhani kiasi cha saa moja. Saa 12.00 jioni basi nitawaita Waheshimiwa Wabunge tuingie katika Kamati ya Matumizi ili tupitishe kifungu kwa kifungu na mkumbuke vifungu ni vingi vinavyosimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika bajeti hii. Kwa hiyo, nawakumbusha tena vitabu, tukiwa na vitabu vyetu saa 11.00 jioni itarahisisha rejea ili tumalize vizuri. Nashukuru sana kwa uvumilivu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa kuwa muda umefika basi nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa chama chetu cha CCM. Lakini naomba niwapongeze wale wengine wote, waliopata nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama cha Mapinduzi na ambao wanaongozwa na Mwana-CCM wa siku nyingi, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, iliyotanguliwa na zile hotuba za Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji. Nawapongeza sana kwa hotuba zao nzuri, lakini pia ninaipongeza Serikali nzima ya Awamu ya Nne, kwa kufanya kazi nzuri. Mwanzo tumeona ni mzuri, tunakwenda vizuri na mimi nafikiri *there is some light in the channel*. Hotuba ya Waziri Mkuu, ukiiangalia inaonyesha kwamba, inayo dira sahihi kabisa, dira ambayo inatupeleka kwenye maendeleo. Mimi nampongeza kwa sababu sehemu nyingi ambazo amezigusia, zinatamka wazi wazi yale ambayo Serikali ya Awamu ya Nne, inakusudia kufanya. Kwa hiyo, ni hotuba yenye *vision for National Development*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie kilimo. Nchi hii mipango yetu ya kilimo imekuwa aidha ni ya zimamoto au ni ya majaribio. Lakini tunajua kwamba, kilimo cha nchi hii ndiyo mkombozi wa walio wengi katika Taifa hili, maana zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wanakitegemea kilimo na haiwezekani tukaendelea kufanya majaribio katika kilimo. Tunayo mabonde mengi, tunayo mito mingi, hii mito inastahili tuitumie vizuri ili tuondokane na baa la njaa.

Mheshimiwa Spika, tuna mipango ya kilimo cha umwagiliaji sehemu mbalimbali. Lakini hii miradi mingine ni midogo midogo sana, haikidhi haja ya kuzalisha kikamilifu vile tunavyotakiwa tuzalishe katika Taifa letu. Lazima sasa tuanze kufikiria kwa makini zaidi ni namna gani tunaweza kuanzisha miradi mikubwa mikubwa ya kilimo. Kule Kigoma tuna bonde la Mto Luiche, ni *very fertile*. Tuna bonde la Mto Malagarasi ni *very fertile*. Hayo mabonde yakitumika, yataweza kulisha hata nusu ya nchi hii. Kule hakuna uhaba wa mvua, bahati nzuri Mungu ametujalia, mvua tunapata, tunamshukuru Mungu. Tukiyatumia vizuri na tukipanga hata yale mabonde mengine yalioko huko Rufiji na sehemu nyingine, nchi hii itaweza kujitosheleza kwa chakula, hatutafika mahali tuanze kuombaomba chakula.

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili kwa sababu ni tatizo kubwa. Tumekuwa tukisema kilimo ni uti wa mgongo, lakini *without proper investment* inayowekwa ndani ya sekta hii na ukiangalia *investment* ambayo inakuwa inawekwa kwenye sekta ya kilimo, kubwa zaidi imekuwa ni maneno tu kuliko matendo. Kwa hiyo, naomba tuwekeze katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mikoa yote ya pembezoni ina faida kubwa kwa Taifa hili. Maana inatuunganisha na nchi za jirani. Barabara ya kutoka Dodoma kwenda Manyoni mpaka Tabora kwenda Kigoma ni barabara ya muhimu sana, ambayo ilitakiwa iwe imejengwa miaka 20 au 30 iliyopita. Bahati mbaya barabara ile ilikuwa haipo na imetunyima mengi. Mazao mengi yanayozalishwa kutoka mikoa kama Kigoma au asali ya Tabora, haiwezi kusafirishwa kirahisi rahisi mpaka kufikia Dar es Salaam. Sasa ni wakati muafaka maana tumezungumza hivi ni wakati muafaka kipaumbele kitolewe tujenge barabara hizi, barabara zinazotuunganisha na nchi za jirani ili tufanye biashara tunahitaji barabara zile zijengwe.

Barabara ya kutoka Kigoma kwenda Burundi ijengwe, maana itatuunganisha na wale jamaa wa Burundi. Wao wanapenda sisi tujenge barabara, maana sisi wanaona tunawacheleweshа. Wanapenda mizigo yao ipite pale maana ni karibu. Hata wangeweza kama bandari haitakuwa na uwezo wa kuichukulia ile mizigo yao pale, mizigo yao mingine ibebwe ipelekwe labda Manyovu ikifika Manyovu pale pawepo na bandari kavu. Wao wanaleta mizigo yao inafikia Manyovu. Kutoka Manyovu mizigo inachukuliwa inaletwa Kigoma inasafirishwa, inaondoka pale inakuja Dar es Salaam na kusafirishwa huko kunakotakiwa kwenda, hii ingeweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Kigoma kwenda Sumbawanga ni muhimu sana. Juzi Rais alipokuwa anazungumza alisema, uko mpango mahsusi unafanyiwa kazi kuhakikisha kwamba, barabara hii inajengwa, itatusaidia sana nayo kurahisisha maana kuna wengine wanaotaka kusafiri kwenda hadi Zambia lakini inabidi wazunguke waje hadi Dar es Salaam kisha waende Zambia. Tunaishukuru Serikali, yako mazungumzo sasa kwamba, barabara ya kutoka Kigoma kwenda Nyakanazi kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa ya Kagera na Shinyanga iko njiani. Tunaishukuru Serikali kwa mpango mzuri huu. Kama barabara hizo zitajengwa, nina imani watu wa Mkoa ule

watafarijika sana kwa tendo hili na tendo hili litakuwa tendo la kuleta maendeleo zaidi na kupeleka maendeleo kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba ya Waziri wa Fedha, bahati mbaya alipowasilisha sikuwepo, lakini nilichokielewa liko suala la mafuta ya kupikia ambayo yamekuwa yanazungumzwa humu ndani. Mimi ni Mbunge niliyeteuliwa mwaka 2005 kwenda Malaysia, kujifunza swali hili kisha niishauri Serikali. Nilikwenda Malaysia nikatembelea zile nchi kisha nikaenda India, nikaona wenzetu wanachofanya ili kuweza kuisaidia Serikali yao na Serikali iweze kupata mapato zaidi. Lakini kabla ya hapo, nilikuwa nazo taarifa kwamba, *exporters* wengi wa kule walikuwa wamefahamu kwamba, watu wetu wanao-*import* mafuta kutoka Asia, wanasema wanachukua *crude oil* kutoka kule. Napenda niwaeleze kwamba, hakuna hata mfanyabiashara mmoja kati ya hao wanaojiita wafanyabiashara wakubwa wa mafuta, anayeingiza ndani ya nchi *crude oil*. Nasema hivyo kwa sababu zifuatazo: *Crude oil* inayotoka Malaysia inakwenda kwenye nchi ambazo wana *joint venture partnership,* hakuna *crude oil* inayokwenda kwenye nchi nyingine nyingine na ni nchi chache tu.

Mheshimiwa Spika, *crude oil* ya kutoka Malaysia ukiinunua kuna kodi ya asilimia 30, ambayo imekuwa *imposed* ili kulinda hadhi zao kule ndani ya Malaysia. Hawawezi kukupa mafuta yaliyosafishwa. Kwa hiyo, hawa wengine wanaoleta mafuta wanakwenda kuyaleta sehemu kama Indonesia. Wanaleta kitu kinaitwa *cocktail cooking oil* kutoka Malaysia na Hongkong. Haya mafuta ni asilimia 95 *refined*, lakini wamekuwa wanayaita *crude oil* na wanapata msamaha wa kodi asilimia 100. Ni makosa wamekuwa wakiibia Serikali kwa kiwango kikubwa, mabilioni ya fedha wamekuwa wanaiba. Tunahitaji kuwasaidia watu wetu ndani ya nchi ili uchumi uonekane ukifanya kazi. Tutakachokipata hapa ni kwamba, Taifa letu sasa litawa-*encourage* wafanyabiashara wetu wanaolima mbegu za mafuta ili waweze kuziuza humu nchini na hivi viwanda visafishe mafuta yanayotokana na mbegu zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kodi ya mafuta iko katika *categories* tatu. *Categories* tatu hizi ndizo zinawachanganya watu wetu kule Dar es Salaam. Lakini tumeandika ripoti, iko Hazina ni juu ya Hazina kuitumia. Ninasikia kuna watu wanasema wanataka kuwasaidia hawa wafanyabiashara ili ile asilimia 10 iliyokuwa *imposed* iweze kufutwa. Ninashauri hii kodi isifutwe iendelee, hakuna nchi Afrika nzima inayoleta mafuta hapa, nchi hii itakuwa inaendelea kupoteza kodi bila ya sababu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anazungumzia habari ya kupeleka shilingi 500 milioni kila mkoa ili kuwasaidia vijana na wengine kujiendeleza katika uzalishaji mbalimbali. Hii itakuwa katika *form* ya *Microfinance. Microfinance* yenyewe *has a discipline, is an extremely interesting discipline.* Lakini ni *discipline* ambayo inataka utaalamu zaidi, sio ambayo kila mmoja anaweza akaingia kisha akafanya kazi ya ku-*manage Microfinance business*. Ukiwauliza wale wanaoendesha *Microfinance* huko waliko, wanakwambia *Microfinance* ni biashara ya kitaalamu zaidi na lazima ifanyike kitaalamu. Ukiwaendea Mabenki, *formal financial institutions,* wanakwambia sisi hatuingii kwenye biashara hii, *because Microfinance* ni ya watu

maskini. *Formal financial institutions are not instutions of the poor,* ndivyo wanavyokwambia. Sasa tunahitaji utaalam, ukizipeleka shilingi milioni 500, uzipe Halmashauri, hizi fedha zitapotea. Ushauri wangu ni kwamba, ni lazima tutafute wataalamu na wataalamu tunao hapa hapa nchini, waweze kutusaidia ku-*manage* hii *microfinance programme. (Makofi)*

Tunayo *Pride,* wamejenga uwezo, wamejenga nidhamu ya kuendesha kazi yao vizuri zaidi. *Repayment rate* ndani ya *Pride* ni kubwa sana na ni nzuri sana, *it is almost hundred percent,* huwezi kupata wataalamu zaidi ya hawa. Kwanza, Bodi yenyewe utakayoichagua inahitaji ifundishwe maana ya *Microfinance*, hiyo Bodi utakayoichagua. Lakini pili hawa wengine wanaokuja kufanya kazi ndani ya *Microfinance*, wanahitaji wafundishwe. *So you either appoint an organisation,* ambayo itafundisha hii *Microfinance* kama biashara yenyewe ili waweze kuifanya vizuri zaidi na Taifa hili liweze kunufaika na wale walengwa wanufaike zaidi, *otherwise* fedha zitapotea. Lazima tujifunze kutokana na *culture* ya Watanzania. Akipata fedha anataka akimbie akaoe mke wa pili, anataka akimbie akanywe pombe, anataka akimbie akafanye lolote lile, hii ndiyo *culture* yetu. Sasa lazima tujifunze kutokana na *culture*.

Ukipeleka bilioni watu watazichukua kweli na watakwambia wanakwenda kufanyia biashara. Ukitaka michanganuo watakuletea lakini fedha zitapotea. *Pride* ipo tuitumie iweze kutusaidia kuwafundisha watu wetu na *even* kwenda *further*. Hata ikiwezekana wa-*manage* fedha hizi, maana uwezo wanao. Wamejenga nidhamu kubwa, wana uwezo mkubwa, tunaweza kuwaamini wakafanya kazi yao. Kile chombo kinaendeshwa na Watanzania halisi, wote ni wazawa wa humu humu ndani, wanaweza kukiendesha kile chombo na waka-*manage* hizi fedha zetu vizuri zaidi na sisi tukafurahi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye mashule tatizo kubwa ni Walimu, kwenye mashule tatizo kubwa ni *infrastructure* nzima, *it is incomplete*. Shule inakaa miaka saba, nane, tisa, kumi, haina *laboratory,* lakini wanasema tunafundisha sayansi. Tunazalisha Mwanasayansi wa namna gain, ambaye hawezi hata kufanya *experiment* ya aina yoyote! Tujitahidi pia tuweze kujenga uwezo wa shule hizi za Sekondari. Hizi shule tuzipe uwezo, hakuna nchi iliyoendelea bila kuwa na utaalamu wa namna hiyo. Mashule yawepo, watu wasome, watu wakishasoma tutapata nafasi ya kuendelea. China imefanya hivyo, *South Korea* imefanya hivyo na nchi nyingine zote za Asia, ambazo zimepata nafasi ya kuendelea, ambazo tulikuwa kwenye *level* moja ya maendeleo, wamefanya hivyo na wamefanikiwa kuendelea kwa kujali sana mashule yao.

Mheshimiwa Spika, ili kushughulikia umaskini vizuri zaidi ni lazima afya za watu wetu nazo ziwe nzuri. Hali ya afya ya watu wetu huko vijijini sio nzuri. Hospitali hazina madawa, watu wamejenga *dispensaries* nyingi, mimi nikienda jimboni ninaulizwa umetuhamasisha tumejenga sasa tumejenga madawa yako wapi, tunaambiwa tena tuchangie tununue madawa, hivi Serikali hii ya kwetu inatusaidiaje? Tunahitaji madawa Mheshimiwa Mbunge. Sasa mimi maelezo ya kutoa ninawaambia tu Serikali bado inajiandaa, inatuletea Waganga, madawa na tutafaidika na mpango maalum unaokuja wa Serikali. Tutengenezeeni utaratibu wa kupeleka madawa kwenye hizi *dispensaries,*

vinginevyo tutaua moyo wa kujitolea, wananchi wetu ambao tumekuwa tunawaomba wajitolee kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru wewe kwa nafasi nzuri ambayo umenipa na ninaomba nimpongeze sana Waziri Mkuu na timu yake, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Nakushukuru sana, naunga hoja mkono mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wengine, wamekuwa na shauku ya kujua baadhi ya wageni wetu, kwa hiyo, naomba kutangaza ifuatavyo:-

Katika *Speaker's Gallery* pale naomba nimtambue Mama Mary Johnson, yeye ni Mkuu wa Idara ya Uchumi na Siasa katika Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam. *We are glad to have you Mama Johnson in your first visits to this chamber. Thank you very much. (Makofi)*

Upande wangu wa kulia kuna vijana, naona kama ni vijana hawa, ambao wana sare wengine nyeupe, wengine njano, hawa ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa *The Tanzania Muslim Students' Association (TAMSA),* Chama cha Wanafunzi Waislamu wa Tanzania. Naomba msimame ili Wabunge waweze kuwaona. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda nimpongeze Waziri Mkuu na timu yake yote, kwa ajili ya kuweza kutengeneza hotuba hii, ambayo inaendana na wakati. Ninachomwombea kwa Mwenyezi Mungu, ampe watendaji ambao wakipiga huo mdundo anaouzungumza, wacheze pamoja.

Pia nampongeza Rais wetu, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa kura nyingi, hiyo moja isiwasumbue. Namwombea dua Mwenyezi Mungu, ampe umri mrefu, afya njema, hekima na busara na pia Mwenyezi Mungu, amsaidie kumpa kifua cha uvumulivu. Pia nawapongeza wale wote ambao wamechaguliwa kumsaidia katika jahazi hili zito, nikiwaomba tafadhalini muendane na Rais wetu ili tulete mustakabali wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijapoteza muda, naomba pia niwapongeze wale waliopata nafasi ya kuwa Mabalozi wa nchi za nje. Hawa wanakwenda kuitambua au kuiwakilisha nchi yetu kule wanakokwenda. Nawaomba sana katika pongezi zangu hizo, wajue kwamba, wanakwenda kule kuitangaza Tanzania, kwani inasikitisha unapofika nchi za wenzetu, unatoka wapi unasema *East Africa*, kitu cha kwanza unaulizwa ni Nairobi? Unaposema Tanzania, watu wanaanza kutafuta *atlas* waiangalie Tanzania! Kwa hiyo, naiomba Serikali iwasaidie kwa mbinu zote na hali zote, ili waweze kwenda kuitangaza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi leo naanza kwa kuchangia kwanza hotuba ya Waziri wa Fedha. Hotuba ya Waziri wa Fedha, imetenga fedha nyingi sana kwa ajili ya mishahara ya Watanzania. Nilivyoisoma na nilivyoisikiliza kuna na ajira mpya za Wauguzi, Walimu na kadhalika. Ninachokiomba, mchanganuo wa kugawana hizi fedha za mishahara utakapokuwa unatoka, tuwakumbuke wale ambao tayari wako kwenye ajira. Wafanyakazi wa Tanzania wana kipindi kirefu kilichopita bila ya kuongezewa mshahara. Kati ya kipindi hiki, bidhaa zimepanda kwa kiwango cha maradufu, shilingi 60,000 kwa mwezi kwa Mtanzania si chochote. Kwa hiyo, kama tunasema tunataka kuwapa Watanzania maisha bora, kwanza tuangalie wakati wa kugawa hii asilimia ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, shilingi 60,000 kwa mwezi, ina maana tunazungumza shilingi 2,000 kwa siku. Basi kama ndiyo tunaanza au ndiyo tunataka kuwaweka vizuri hawa, basi angalau ni shilingi 5,000 kwa siku ili na wao wakipata hizo shilingi l50,000 labda wanaweza wakasogeasogea. Kama tunafikiria kuwapelekea shilingi milioni 500 kwenye mikoa kwa ajili ya mikopo ya maendeleo ya wanawake na vijana, mikoani maendeleo haya wanapewa hizi fedha ili wafanye biashara, waweze kumudu kurudisha huu mkopo. Sasa hivi biashara watakazofanya ili warudishe mkopo, mnunuzi ni nani? Kweli kama ninalipwa shilingi 60,000 au mtaniongezea nipate shilingi 100,000, nitamudu kununua vitu vya sanaa ambavyo vitatengenezwa na akinamama; nitamudu kununua maua na vinyago nipambe nyumbani ambavyo vinatengenezwa na vijana au nitaangalia jinsi ya kuigawa ile shilingi 100,000?

Mheshimiwa Spika, hizi shilingi milioni 500 tunazozingumza, zinazopelekwa kwenye mikoa sasa hivi, kama hatutaziangalia, tayari kuna watu wameshafungua midomo wanazisubiri. Mengi yameshapita tumeyaona, hatuna haja ya hadithi, sasa tunapeleka tena MKUKUTA, MKURABITA, tunapeleka tena vitu vingine, tuangalie na tupate somo la kule tulikotoka. Mikopo inatolewa kwenye Halmashauri lakini ninaweza kusema kwamba, kutoka sasa hivi niende kwenye Kata fulani niulize vikundi vya akinamama walivyopata huo mkopo uliotolewa kwenye Halmashauri, Mheshimiwa Spika, tukienda mimi na wewe, tutakuta katika kumi labda mmoja, lakini zimepelekwa kwenye Halmashauri. Sasa ninachokiomba, tunapojadili kuongeza mishahara ya wananchi wa Tanzania ili tuweze kubadilisha maisha yao, tupeleke na shilingi 500 milioni mikoani ili tuweze kubadilisha maisha ya wananchi hao hao, lakini tuangalie tena upya tunafanyaje kabla hatujapeleka fedha hiyo. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, mishahara hiyo hiyo kuna ongezeko la kodi linaongezwa asubuhi na jioni. Kila tunapokaa kwenye bajeti, tangu akina Anna hatujaja Bungeni mpaka leo, kinachoongezwa ni vinywaji baridi na sigara. Lakini hapo hapo tunapiga vita UKIMWI, madawa ya kulevya, unapoongeza bei ya vinywaji baridi, ina maana unamwambia kijana wa Tanzania aendelee na gongo. Sidhani kama atakuwa na uwezo wa kununua bia ya shilingi 1,000 wala sidhani kwamba atakuwa na uwezo wa kununua soda ya shilingi 300 au 400. Kwa hiyo, tunawaambia warudi tena waendelee na gongo, mataputapu na bhangi. Tuangalie tena kitu kingine kipi ambacho kitaweza kuongeza mapato ya Serikali tuachane na vinywaji baridi kwa muda.

Mheshimiwa Spika, janga la UKIMWI lipo, atakayesema hakuna janga la UKIMWI, huyo labda sijui nimwite nani. Kama hujafiwa wewe, amefiwa jirani yako, ndugu yako. Wengine tumepoteza mpaka vijana kumi ndani ya majumba kwa ajili ya UKIMWI. Tumepeleka Maprofesa UKIMWI, tumepeleka watu wenye visomo vikubwa vikubwa UKIMWI. Lakini kila siku tunakuwa tunajadili kwenye Mabunge, *NGOs*, tunajadili UKIMWI, UKIMWI. Kama tuliweza kuzungumza hapa kuhusu majambazi, tukawakabidhi wenzetu hawa walioshika usalama wa raia kazi na wakamudu kuweza kushika shina la ujambazi katika nchi hii, nina hakika tutakapokusudia kufanya kazi, basi tutauweza UKIMWI na tutawaweza vijana wetu wanaomalizika kwa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, siamini mnaponiambia haeleweki nani analeta dawa za kulevya katika nchi hii. Wafanyabiashara wanatangaza ana biashara yake anauza labda viatu vya kandambili, maplastiki na vitu vya ajabu, lakini anapofika mwisho wa mwezi analipa *TRA.* Asilimia 20 ya *TRA* anayolipa, tukitaka kujua tutaangalia amefanya biashara ya shilingi ngapi kwa mwezi. Mfanyabiashara huyu huyu tunamwangalia anauza kandambili na madishi ya plastiki lakini anajenga maghorofa kumi Kariakoo, anapata wapi hizi fedha kama hajihusishi kwenye biashara ambazo sio za halali katika nchi hii; tunatafuta mchawi wapi?

Mheshimiwa Spika, nawaomba ndugu zangu wanaoshughulika na mambo ya biashara na UKIMWI na madawa ya kulevya, kama tulivyofanya kazi kwa muda wa miezi sita nchi hii tukaweza kujua shina la ujambazi, basi naomba tufanye kazi kwa miezi sita hii iliyobaki, tujue shina la madawa ya kulevya na nini tufanye kuhusu UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ninazungumza kuhusu Halmashauri zetu. Hatuwezi tukatoka hapa Bungeni wote tukasema tunakwenda kwenye Halmashauri fulani leo ili tukashughulikie kule wananchi wapate maendeleo. Kule kuna Madiwani, nao ni chaguo la wananchi. Diwani kama anataka kurudi kwenye Kata awe Diwani tena lazima ahakikishe anapeleka maendeleo kwenye Kata yake, akishirikiana na Mbunge na kama Wabunge tunataka turudi tena kwenye majimbo. Diwani anapokwenda kule ana Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji hawa wote wanataka kurudi tena katika mamlaka hayo ya kuwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji wa Mitaa. Lakini utakuta vitu vinavyofanyika katika hali hiyo ni vitu vya ajabu. Leo tunaambiwa, Halmashauri kadhaa zimepata hati ya kutambulika. Lakini kuna Halmashauri 14 kama sikosei hapa, ambazo wamepewa cheti cha kufeli.

Naomba nijulishwe hao ambao hawakutimiza wajibu wao, wamechukuliwa hatua gani, ili tuweze kuwaambia wale wengine ambao hawatafanya vizuri hii ndio hatua ya Serikali leo. Sio kuandika tu kwamba, kuna Halmashauri ambazo hazijafanya vizuri. Halafu tumewaacha, tunawaogopa nini. Hii ni nchi yetu na tunachotaka kufanya ni kubadilisha maisha ya Watanzania. Tukitaka kubadilisha maisha ya Watanzania, tunaanza katika vijiji, mitaa tunakuja kwenye Halmashauri ndio Mheshimiwa Mbunge anapata pa kuanzia. Tusiwaache anayekwenda nyuma ya mdundo kama alivyosema Waziri Mkuu hadharani, awekwe na wengine wapate mfano wajue kwamba sasa hivi hii sio Serikali ya mchezo na Wabunge waliopo pale Bungeni sio Wabunge wa kuchezea

tena. Tunataka mifano hai tuione wanaochezea mali za umma kwenye Halmashauri wachukuliwe hatua muhimu tena haraka tukiona.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na afya njema katika Bunge lako Tukufu leo hii. Pili, ni kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkoani, kwa kunipa kura nyingi na nikaweza kuwa Mbunge wa Jimbo lao na ninawasihi kuwa sitawaangusha. Tatu, nikushukuru wewe kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake safi, ambayo ameitoa katika Bunge hili na vilevile nimshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kweli hotuba yake ni makini na inahitaji kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia hotuba ya Waziri Mkuu ni vyema nijikite katika hotuba za Wasemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwa sababu kuna mawazo kuwa Wapinzani ni watu wanaopinga tu, Wapinzani pengine hawaitakii mema nchi hii, Wapinzani ni wakorofi. Kwa kweli sisi ni Watanzania na tuliomo ndani ya Bunge hili, hakuna hata mmoja ambaye haitakii mema nchi hii. Sisi kama tunakosoa, basi tunakosoa kwa nia kwamba, Serikali iende vizuri. Sambamba na hilo ni kwamba, ukiangalia hotuba za Wasemaji Wakuu katika Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, utagundua kuna hekima kubwa ya Wapinzani, wamedhihirisha mle. Hawakukosoa tu na ni vyema nitoe mafano kwa sababu Upinzani ulio mzuri ni ule ambao unapongeza panapostahili kupongezwa, unakosoa pale panapostahili kukosolewa na unashauri pale ambapo panatakiwa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukizisoma hotuba mbili za Wasemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ukiachana na tofauti ambayo ilizuka, suala la *lift* ya ndege na suala la ujenzi wa nyumba za Afrika Kusini, bado hotuba zile zina hekima kubwa. Zina nini hotuba hizo? Zina hekima kubwa. Kwanza, Serikali imepongezwa kwa sababu nasema Upinzani si kupinga kila kitu. Serikali imepongezwa kwanza, kwa kupitia Mawaziri waliowasilisha hotuba zao pamoja na Manaibu Mawaziri na wamepongezwa watendaji. Hii ni kuonyesha kuwa, kazi yao tunaithamini. Pili, katika hotuba hizo za Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani. Wamezipongeza *SACCOS*, hii ni kuonyesha kwamba, *SACCOS* ni utaratibu mzuri, ipo haja ya kufuatwa. Zimepongezwa *SACCOS* za Kibaigwa, Gairo na sehemu nyingine. Hii ndiyo kazi mojawapo ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika hotuba hizo, imepongezwa Serikali kwa kuongeza fedha katika elimu kutoka asilimia 16.1 mpaka asilimia 19. Hili ni jambo zuri, lakini vilevile katika kupongeza utendaji wa Mfuko wa *TASAF*, ukiziangalia hotuba hizi Wapinzani wanapongeza kuwa Mfuko wa *TASAF* unafanyakazi vizuri. Kwa hiyo,

Wapinzani nasisitiza tena si kama ni wapingaji tu, lakini kile kinachostahili kupingwa kinapingwa, kukosolewa kinakosolewa na kupongezwa kinapongezwa.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la mshahara, hakuna hata mmoja atakayesema kuwa kuongezwa mshahara ni jambo baya. Kwa hiyo, nalo hilo vilevile utalikuta kwenye hotuba za Wasemaji Wakuu wa Upinzani wamelidhihirisha hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuhusu MKUKUTA, ni mpango mzuri, ambao umeshirikisha wananchi kuanzia chini kabisa. Kwa hiyo, sisi Wapinzani katika hilo tunaipongeza Serikali. Lakini katika upande wa pili wa shilingi vilevile tumekuwa na mashaka na baadhi ya mambo na wenzetu, yafaa tufahamu hatuna nia mbaya na nchi hii. Kwa mfano, kuna upotevu wa fedha, ukiangalia mwaka 2004/2005, katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Fedha, kaelezea upotevu wa fedha na alitaka maelezo kwa kweli kutoka Serikalini. Vipi waliopoteza fedha hizi watashughulikiwa? *(Makofi)*

Mfano, Hazina kuna upotevu wa pesa shilingi bilioni 1.8, kwa mujibu wa hotuba hiyo. *Police Force* ni shilingi milioni 132, Kilimo shilingi milioni 122 na Maliasili shilingi milioni 155. Sasa tunaposema haya tusionekane kuwa ni wakorofi, lakini tunajaribu kuieleza Serikali kuwa Bajeti yetu ni tegemezi kwa asilimia 39. Huku kuna fedha zinazochumwa na Serikali zinavuja. Kwa hiyo, si vyema sisi tunyamaze kimya na kwa hili tutaendelea kulieleza kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la *TANESCO*. *TANESCO* ni shirika la kibiashara, sasa leo shirika la kibiashara linapofika mahali kila wakati linapata ruzuku kutoka Serikalini, kwa kweli pana mtihani hapo. Kwa hiyo, kuwa na wasiwasi ni haki yetu na wala hakuna anayesema kuwa nishati ya umeme si muhimu na sisi Wapinzani hatujasema hilo. Sisi tulichokitaka kwa sababu tayari *TANESCO* imeshailipa *IPTL* na *Songas* dola za Kimarekani milioni 60 na sisi tunadaiwa dola za Kimarekani milioni 40 na katika bajeti hii Serikali imeshatoa idhini kuwa *TANESCO* wapewe ruzuku ya dola milioni 200. Upinzani ulichotaka katika jambo hili ni kuelezwa; je, hizi dola za Kimarekani milioni 200 zitatosheleza katika kuhakikisha tunapata umeme? Wala Upinzani haukupinga kwamba, wasipewe fedha hizi, lakini tulikana maelezo, kwa sababu ufafanuzi ulikuwa ni mfupi, kwa hiyo, ikabidi tuombe maelezo kutoka Serikalini ambayo hayakutoka.

Mheshimiwa Spika, kuna mgao wa fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambao ni kwa muda mrefu kinatumika kigezo cha 4.5. Zanzibar ni nchi na ina Wizara, ambazo zinaoangoza kada mbalimbali. Kuna Wizara ya Afya, Kilimo na Mawasiliano. Haipendezi kuwa misaada itoke nje halafu kiwango hiki ni cha muda mrefu. Ukiangalia katika hotuba za Wasemaji wa Kambi ya Upinzani, ni kwamba, Bunge hili liliahidiwa itakuja *formula* mpya ya kugawa, lakini mpaka leo tunaambiwa tusuburi. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya mambo ambayo Wapinzani waliyaona katika hutoba zile mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mchango wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika suala la Utawala Bora. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, maelezo hayo unayapata katika ukurasa wa 28 na 29. Nizungumzie kipengele kimoja tu cha Utawala Bora, vyombo vinavyohusiana na Utawala Bora, kimojawapo nina

kitabu hiki, naomba ruhusa yako kukisoma. Kwenye kitabu hiki kuna taarifa ya mwaka 2002/2003 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Ripoti hii ni ya mwaka 2002/2003 imeletwa Bungeni 2006. Hili ni tatizo na chombo hiki ndicho kinachosimamia Utawala Bora. Sasa chombo kinachosimamia Utawala Bora, utendaji wake ni huu, hawa wengine watakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu zaidi kwamba, katika Sheria ambayo imeunda Tume hii ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sheria Namba 7 ya mwaka 2001, ilitakiwa ikishatoa taarifa ipeleke kwa Waziri mhusika, ambaye ni Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Tume imekitayarisha Kitabu kwa mwaka 2002/2003, wao Tume wamekipeleka Wizarani terehe 31 Desemba, 2004. Sisi tumekipata 2006 na ni chombo muhimu mno katika suala la Utawala Bora na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, barua yenyewe naomba unipe ruhusa niisome kidogo, hii ni taarifa ya mwaka 2002/2003 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Inasema: "Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu (Mb), Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, S.L.P. 9050, Dar es Salaam. Tunawasilisha kwako kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 131(3)(a) na (b) na Sheria Namba 7 ya mwaka 2001 kifungu 33(a), (b) na (c)."

Mheshimiwa Spika, tuone sasa Ibara hiyo inasema nini. Ibara ya 131(3)(a) na (b) inasema: "Kila mwaka wa fedha, Tume itatayarisha na kuwasilisha taarifa kwa Waziri anayesimamia haki za binadamu kuhusu; (a) Shughuli za Tume katika mwaka uliotangulia; (b) Hali ya utekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri atawasilisha mbele ya Bunge, kila taarifa iliyowasilisha kwake na Tume mapema iwezekanavyo baada ya kuipokea."

Sheria inasema kuwa, kifungu cha 33(1)(a), (b) na (c) cha Sheria Namba 7 ya mwaka 2001, inasema: "Katika kipindi cha miezi sita, kila baada ya mwisho wa mwaka wa fedha, Tume itaandaa na kuwasilisha Bungeni kupitia Waziri mwenye dhamana, taarifa ya mwaka unaohusika pamoja na ..."

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2002, Bunge lako linaipata taarifa 2006. Huu si Utawala Bora na ni suala la Kikatiba na sheria, si matakwa. Kwa hiyo, kwa nini kukatokea haya? Nadhani ni vyema tuje tuelezwe, kwa sababu hiki ni chombo kizito na kinahitaji kupewa nafasi yake, kwa sababu sheria imetaja Bunge. Waziri alipelekewa tangu mwaka 2004 na mwaka 2006 ndio inafika Bungeni!

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la Muungano. Tunaposikia sikia Zanzibar ina hali ngumu kwa kweli tunapata mashaka kidogo na inahitaji kusaidiwa. Kwa sababu Zanzibar haikuwa hivyo. Tunapata taarifa kuwa mwaka 1974, Zanzibar iliwahi kuisadia Tanzania Bara hapa. Sasa wako wengi wamechangia namna gani ya kuisaidia Zanzibar na njia nzuri si kutoa fedha.

Mheshimiwa Spika asante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpange mambo vizuri, sasa hapa Mheshimiwa Ali Khamis Seif, mchango wake ulipokuwa unakolea, ndiyo muda umepita. Basi inaharibu kila kitu, nakushukuru sana tena sasa. Namwita Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, atafuata Mheshimiwa Anna Lupembe na baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa Kanali Saleh Ali Farrah.

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii ya awali kabisa, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwaka 2005. Naomba pia kwa huzuni kubwa niseme tu, tulipoachana hapa mchana nilipokea simu ya kuondokewa na rafiki yangu wa karibu, mfadhili wa chama chetu, aliyekuwa akiendesha gari lake kutoka Mererani kueleka Arusha, gari lake lilipinduka na yeye akafariki dunia. Ni kiongozi mwenzetu, namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

**SPIKA:** Hukumtaja kwa jina Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninafahamu juu ya umuhimu wa kutaja jina hilo, amefariki saa moja na nusu iliyopita. Bado familia yake haijaambiwa. Kwa hiyo, naomba kwa heshima na taadhima, niache kulitaja jina hilo kwa sasa. Nasema hivyo kwa sababu yeye mwenyewe aliponipigia simu asubuhi ya leo, aliniomba kwamba, nitakapochangia leo nizungumzie baadhi ya mambo. Najua kwamba, familia yake inanitazama sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii na hasa kwa kujua kwamba, ni mara yangu ya kwanza, kuzungumza mbele ya Bunge lako Tukufu, nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura zote. Mimi nilikufahamu wakati nilipokuwa mwanafunzi, kama vijana wale walioko pale juu. Nilipokuwa Rais wa Serikali ya Ushirika wa Kikristo wa Wanafunzi Tanzania (UKWATA), nilikualika kutufungulia Mkutano wetu Mkuu wa Taifa, uliofanyika katika Shule ya Sekondari Mazengo. Ulikuja ukatoa hotuba nzuri na baadaye mada yako ambayo ilitushawishi na kutufanya tukukumbuke na kusema kwamba, pengine Mwenyezi Mungu, bado ana mpango mzuri na nchi hii, kwa kukupa nafasi nzuri ya kulitumikia Taifa letu. Nina hakika maombi ya vijana wale, Mwenyezi Mungu ameyasikia, kwani maandiko matakatifu yanasema, kitakachofunguliwa duniani na mbinguni kimefunguliwa na Walatini wanasema, sauti ya watu ni sauti ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba basi kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, nikuombe uendelee kikikalia Kiti chako, kwa kasi na viwango kama ulivyotuahidi na sisi Wabunge wenzako tuko nyuma yako, kukupa ushirikiano wa kutosha. Baada ya kusema hayo, nataka nichukue nafasi hii, kukishukuru chama changu cha CCM na kupitia Mkutano Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro. Walinipa kura nyingi za kishindo na hivyo kuiwezesha Halmashauri Kuu ya Taifa kuteua jina langu kuwa Mgombea pekee wa Ubunge wa Jimbo Simanjiro, kwa tiketi ya CCM. Kipekee nataka niwashukuru wananchi wa Simanjiro si kwa kunichagua mimi tu, kwa kura nyingi na kuwa Mbunge wao, lakini kwa kumpa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kura za

kishindo na kuwachagua Madiwani wote wa Kata zote 15 wanaotokana na chama changu cha CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi hao walionichagua na kwa kuwa Waswahili wanasema, chanda chema huvishwa pete na si stahiki kwa kichwa cha jogoo kuvishwa kilemba, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yao, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mambo makubwa matatu. La kwanza, nampongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kura za kishindo. Sababu yangu ya pili ya kumpongeza Mheshimiwa Rais ni kwa ushindi wa kishindo cha kimbunga cha *Tsunami*, alioupata juzi kwenye Mkutano Mkuu wa Chimwaga, kwa kupata kura karibu zote, isipokuwa moja, kuwa Mwenyekiti wetu wa Taifa wa Chama chetu cha CCM.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninaafiki kwamba, Mheshimiwa Rais, ametufanyia kazi nzuri ya kuunda safu ya uongozi na watendaji wa juu wa chama, kwa kumteua Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mheshimiwa Jaka Mwambi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, kuongoza safu ya sekretarieti ya chama chetu. Chama madhubuti huzaa Serikari madhubuti. Nawahakikishia kwamb, safu hiyo chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, imeshasafisha njia ya mwaka 2010, kwani Waswahili wanasema, kanzu ya Ijumaa hufuliwa Alhamisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kupitia Bunge lako Tukufu, nimpongeze kaka yangu na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, kwa nyadhifa hizo walizopewa. Ningependa nisiwe mchoyo wa fadhil, Tume ya Uchaguzi ya Tanzania na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, zilifanya kazi yake kwa umakini na kwa kiwango cha kupigiwa mfano. Nataka kusema kwamba, vyombo vya ulinzi na usalama, pamoja na vyombo vya habari, vilifanya kazi zao kwa kiwango cha kupigiwa mfano. Natoa ushauri wa bure kwa vyama vya siasa vilivyomakini na kwa wanasiasa waliomakini, uchaguzi umekwisha, Karume amepatikana, Kikwete amepatikana, kazi iliyobaki sasa ni wao wajipange kwa mwaka 2010, kwani baada ya uchaguzi mmoja ndiyo mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi unaofuata.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya yangu ya Simanjiro, wana matatizo mengi lakini naomba kupitia Bunge lako hili Tukufu, nizungumzie baadhi ya mambo ya msingi, ambayo yanawaguasa wananchi hao. Nilipokuwa napita kuwashukuru, niliwaambia wananchi wangu wa Simanjiro, nitatimiza wajibu wa mwanasiasa makini kwamba, nitawatetea na kuwasimamia mambo yenye maslahi kwao, bila kumwomba radhi mtu yeyote, lakini kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na maelekezo ya Chama changu cha CCM. Nimekuwa kimya kwa muda sio kwamba, nimesahau ahadi nyangu. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, niwaambie kwamba, kilichonifanya ninyamaze kwa muda huu ni kutokana na ushupavu, umakini, umahiri na uadilifu wa Serikali ya Awamu ya Nne, wa kushughulikia mambo ya msingi yanayowagusa wananchi hao wa Jimbo langu. Serikali ya Awamu ya Nne, imeanza kushughulikia utekelezaji wa Ilani katika Jimbo langu, kwa kuniahidi kwamba, katika Bajeti hii ya

mwaka huu, umeme kwa mara ya kwanza, utawashwa katika Makao Mkuu ya Wilaya ya Simanjiro, Orkesumet.

Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, amefanya kazi hiyo na kwenye Bajeti yake nimechungulia chungulia pale na kwenye Bajeti ya Mhesimiwa Zakia Meghji, nimechungulia chungulia pale, najua kwamba, umeme mwaka huu utakwenda Orkesumet na utawashwa katika Kata za Terrat, Orjora Namba Tano na sasa kazi iliyobaki ni kwa Kata nyingine kama Msitu wa Tembo na Kata ya Ngorika, karibu na Nyumba ya Mungu, ambako ndiko umeme unakotoka, lakini hauwashwi Simanjiro. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya Jemadari Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii, kuzungumzia suala la barabara. Mwaka 2002, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliugawa Mkoa wa Arusha na kuunda Mikoa miwili mipya; Mkoa wa Manyara na Mkoa wa sasa wa Arusha. Katika hotuba yake ya kuugawa Mkoa huo, Mheshimiwa Mkapa alisema, barabara itatengenezwa kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro kwenda Babati na kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kiteto ambayo ni Kibaya kwenda Babati.

Mwaka 2005, zilitengwa shilingi bilioni 1.1 na zilitengeneza kilometa 22 tu, mwaka huu zimetengwa shilingi milioni 870, kwa kasi hiyo maana yake barabara hiyo ambayo inahitaji zaidi ya shilingi bilioni 15, itachukua miaka 20 kukamilika. Ningependa kuiomba Serikali ya Awamu ya Nne, kwa ari ileile na nguvu ileile na kasi ileile, ielekeze nguvu zake kutafuta fedha katika vyazo vingeni ile barabara ya Orkesumet kupitia Naberera, Kimotorok kwenda Babati, ikamilike na barabara inayotoka Kibaya kwenda Mkao Makuu ya Wilaya ya Babati, nayo ikamilike.

Mheshimiwa Spika, ningepnda pia nichukue nafasi hii, kwa kweli nisiwe mwizi wa fadhila, kugusia tatizo la maji. Nilitaka kuwashukuru watu wawili sasa niende kwenye suala la maji. Simanjiro ina tatizo la maji, asilimia 80 ya Wilaya ya Simanjiro hatuna maji na kwa sababu hakuna maji, wafugaji wanahamahama kufuata malisho na maji na ukitaka kuwasaidia watu hawa ili wapate elimu waweze kumudu ushindani wa kisasa na waweze kufanya mambo yanayoendana na wakati huu. Ni vizuri kwanza, Serikali iwekeze katika kuwapatia maji, lakini pia iwekeze katika suala zima la kuwajengea mashule ya bweni. Nampongeza Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa ahadi yake aliyonipa kwamba, atahakikisha kwamba, walau tunapata shule kadhaa za bweni ili watoto wa wafugaji nao waweze kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa elimu, nyote mnajua. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema, uchu wa nguo ni mbaya lakini uchu wa akili ni mbaya zaidi na kwenye Hadithi za Mtume Muhammad *(S.A.W.),* kutafuta elimu ni faradhi kwa Waislam, wanaume na wanawake, tena anasema tafuteni elimu mpaka China. "*Twalbul-ilmi faltunal-muslimin-wal-muslimat.*" *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, kuiomba Serikali ielekeze nguvu, kuwasaidia wafugaji na hata wale

waliotolewa katika maeneo yale ambayo ni vyanzo vya maji, kwa sababu lengo letu wote ni kulinda mazingira. Lakini Serikali iwekeze katika kuwapatia maji, malisho, shule na hospitali, kwa ajili ya watoto wao ili tusiwe tunasikia tu kwamba, fedha zimetengwa za kuwaondoa. Tumesikia zimetengwa shilingi milioni 60 za kuwaondoa, ni za kuwapa tu askari posho ili walinde wale wafugaji wasirudi pale. Zitengwe pia fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji hao kupata makazi mapya.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii, kuiomba Serikali kwa upande wa ruzuku za Serikali Kuu, inazopeleka kwenye Halmashauri zetu kwamba, sasa vigezo vibadilishwe ili wananchi wasio na hatia, wasiadhibiwe kwa sababu tu ya udhaifu na upungufu wa watendaji ambao wameletwa pale. Ufungaji wa vitabu ni kazi ya Mweka Hazina wa Wilaya na Afisa Mhasibu, ambaye ni Mkurugenzi na wote hao ni watendaji. Udhaifu wao na mapungufu yao yasitumike kuwaadhibu wananchi wasio na hatia katika Halmashauri zetu. Ikitumika kama kigezo, tutakosa ruzuku na wananchi hao wataendelea na mateso.

Mheshimiwa Spika nataka sasa nichukue nafasi hii ya mwisho, kuiomba Serikali isaidie katika suala la maji na hasa katika maeneo yale ambayo wananchi wameshachimba visima, wapatiwe pampu na mibirika ya maji na *cattle troughs* katika vijiji vya Narakao, Rwebosiret, Emboret, Kimotorok, Orjohonori, Langai. Kwa kufanya hivyo, wananchi hatutawakatisha tamaa kutokana na jitihada walizokwisha zifanya za kuchimba visima vya kina kirefu kwa gharama zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ili kengele isije ikanigongea tena, maana naona inakaribia, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Lakini nataka kumtambua na kumpongeza Mheshimiwa Kanali Tarimo, Mkuu wangu wa Mkoa, kwa kuteuliwa. Pia napenda kumpongeza kaka yangu, Mheshimiwa Kone, kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, ambaye alikuwa Mbunge wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Ni dhahiri katika Bunge hili tunapata elimu ya kila namna, wapi unaweza kushuhudia Mmasai anayeitwa Christopher ananukuu *Quran* Tukufu. Mheshimiwa Anna Lupembe, atafuata Mheshimiwa Kanali Saleh Ali Farrah, wakati huohuo natumaini Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, atakuwa amekwisha rejea, ndiyo atakayefuata, ajiandae. Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenileta mahali hapa. Pili, nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Rukwa, walionipa kura za kunileta hapa. Tatu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Vile vile naomba niwapongeze watendaji wote waliochaguliwa kuwa Viongozi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie maendeleo vijijini. Ni kweli tunazungumzia maendeleo vijijini, lakini vijijini hakuna maendeleo. Unatembelea vijijini unakuta mapungufu mengi, unakuta watendaji hakuna, unakuta Mabibi Maendeleo

hawapo, unakuta Mabwana Shamba hawapo. Bwana Shamba na Bibi Maendeleo ndio watendaji wakubwa vijijini. Bibi Maendeleo kuweza kuwaelimisha wanawake na Bwana Shamba kuwafundisha wakulima jinsi gani ya kuweza kulima. Kila siku tutakuwa tunasema maendeleo vijijini hakuna kutokana na Mabwana Shamba, kutokuwepo vijijini, pamoja na Mabibi Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile naweza kusema Wakurugenzi hawafanyi ziara vijijini, kwenda kukagua kama Mabibi Maendeleo na Mabwana Shamba wapo au hawapo. Unakuta Mabwana Shamba na Mabibi Shamba, wanajifanyia shughuli zao wenyewe vijijini kwa sababu hakuna mtu anayekwenda kuwa-*monitor*. Tutakuwa tunasema kila siku hakuna maendeleo vijijini kutokana na utendaji ambao si mzuri Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukienda upande mwingine, ukienda Halmashauri, Mkurugenzi ndiye Mtendaji Mkuu. Ukifika pale unakuta Mkurugenzi hayupo, Bwana Mipango hayupo, Mweka Hazina hayupo. Ukiuliza wamekwenda wapi, unaambiwa safari. Mkurugenzi ameenda wapi, kwenye kikao Dar es salaam au Dodoma, Mweka Hazina ameenda wapi, ameenda Dar es salaam, Afisa Mipango amekwenda wapi, amekwenda Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, hatutafika. Hayo maendeleo vijijini hayawezi kwenda kwa sababu watendaji wadogo wadogo wakishaona Mkurugenzi au *DT* hayupo, hawafanyi kazi, bali wanafanya shughuli zao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja upande wa Afya. Vile vile unaenda vijijini unakuta kuna Zahanati au Vituo vya Afya, havina hata Mganga. Mimi nilitembelea kijiji fulani huko, nikakuta *Dispensary* haina Mganga. Niliuliza Mganga amekwenda wapi, wakasema Mganga anaumwa. Akina mama wanapata tabu. Kuna mama mwingine ameshikwa na uchungu, hakuna mtu wa kumsaidia, ikabidi mimi nimbebe. Tutakuwa tunasema vijijini hakuna maendeleo, sisi wenyewe hatufuatilii.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa Wizara ya Afya, ninashauri Zahanati, pamoja na Vituo vya Afya, ni bora Wizara ya Afya ivichukue, ivisimamie na moja kwa moja. Labda Wizara ya Afya inaweza ikaboresha, maana yake wao ni wajuzi zaidi, tukizingatia Waziri wetu ni Profesa, anaweza akaboresha huduma za hospitali vizuri zaidi kuliko Halmashauri. *(Makofi)*

Nakuja upande wa Wanawake na Watoto. Wanawake vijijini hawana maendeleo kutokana na kwamba, hawana uwezo. Vijijini unakuta mwanamke hana hata shilingi 1,000, tunategemea huyo mwanamke ajiunge katika kikundi cha *SACCOS!* Akina mama wengi tunawahamasisha kuwa watoe shilingi elfu kumi, ili waweze kupata mkopo. Mwanamke wa kijijini hana hata shilingi 1,000 mkononi; je, huyu mwanamke tutamfanyaje?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, amesema zitaenda shilingi milioni 500 kila Mkoa. Je, hizi shilingi milioni 500 zitafanywaje ili huyu mwanamke aweze kupata mkopo?

Mheshimiwa Spika, nakuja upande wa barabara. Wilaya yetu ya Mpanda, barabara kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda ni mbovu na haifai. Ukitoka Mpanda – Sikonge - Tabora, barabara haifai. Kutoka Mpanda – Uvinza – Kigoma, barabara haifai na kuja Mpanda – Kalema; hayo maendeleo tutayapataje bila barabara? Wilaya ya Mpanda inalima mazao mengi mno. Wilaya ya Mpanda inalima mazao hata watu wa Shinyanga wanakuja kuchukua mazao Mpanda. Watu wa Tabora wanakuja kuchukua mpunga Mpanda. Ninaomba barabara ya Mpanda – Sikonge – Tabora, itengenezwe. Barabara ya Mpanda – Uvinza – Kigoma itengenezwe, kwa sababu watu wa Kigoma wanakuja Mpanda kuchukua mpunga, mahindi ili waende kuuza katika Mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Elimu upande wa walimu, wengi wapo vijijini. Walimu wanapata shida kupita kiasi. Mwalimu wa kijijini akitoka kijijini kuja Wilayani, anakaa siku tano, sita, saba, akisubiri mshahara. Akifika Benki ni vurugu. Foleni inakuwa shida, vile vile anakaa *Guest*. Mshahara wake ule ule, anautumia kwa kulipia *Guest*. Akitoka pale, mwalimu hana senti tano, akirudi kijijini anaanza kukopa upya! Tutafika wapi? Vile vile wanaacha watoto kule hawana mwalimu yeyote. Mimi mwenyewe nimeshuhudia katika ziara yangu ya safari hii, nilikwenda shule fulani nikakuta haina mwalimu hata mmoja. Niliuliza walimu wamekwenda wapi, wakasema wamekwenda Wilayani kufuata mshahara. Wameenda Wilayani wamekaa siku 14, wanafunzi wale hawasomi! Naomba utaratibu wa mishahara ya walimu ubadilike. *(Makofi)*

Nakuja upande wa michezo. Serikali ya Awamu ya Nne imesema inataka kuboresha michezo. Kusema kweli, nchi yetu michezo iko nyuma sana sana, ninaomba michezo irudishwe mashuleni. Vile vile mashuleni kuna watoto wana vipaji vikubwa mno. Unakuta mara nyingine tunadharau vijijini. Namwomba Mheshimiwa Joel Bendera, atembelee mpaka Wilayani, afanyishe mechi ili atafute watoto wenye vipaji. Wilayani, kuna watoto wana vipaji, vijijini kuna watoto wana vipaji hawajui waende wapi. Naomba Wizara ya Michezo itembelee vijijini, Wilayani mpaka mikoani kutafuta vijana wenye vipaji.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimiwa Spika, sina budi kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kwa kunipa uwezo kwa jioni hii ya leo, angalau nikaweza kuzungumza ndani ya Bunge letu la Muungano.

Mheshimiwa Spika, pili, ninawashukuru wananchi wangu wote ndani ya chama changu, walionisaidia na kuweza kunifikisha hapa. Vile vile sitaweza kukisahau chama changu cha Mapinduzi. Nikimshukuru Mwenyekiti Mstaafu, Mzee Mkapa, pamoja na Kamati yake Kuu na Halmashauri yake Kuu, iliyoweza kunipitisha na kuwa mgombea ndani ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, vile vilile sina budi kumpongeza Rais wangu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa alioupata wa asilimia 80.28. Huo ulikuwa ni ushindi wa kishindo. Vile vile sina budi kumpongeza Rais wangu, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa ushindi mkubwa alioupata kwa asilimia 53. Sina budi vile vile kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais. Ninamkumbuka kwa sababu tulikuwa wanafunzi mahali pamoja. Tulikuwa darasa moja *Lumumba College*, tukikaa bega kwa bega. Vile vile sina budi kumshukuru Waziri Kiongozi na kumpongeza kwa kazi nzuri anayoweza kuifanya. Kwa kweli, siku ya leo vile vile ninataka nimpongeze Spika wa Bunge hili, Naibu Spika wa Bunge hili na vile vile sijawasahau Wabunge wenzangu 274, ambao wamepita ili tukae mahali pamoja tujadiliane mambo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sina fadhila kama sitowashukuru Wawakilishi wangu, hasa Mwakilishi mwenzangu, yeye akiwepo katika Jimbo langu, Mheshimiwa Kamal Bashah, Naibu Spika wa Zanzibar. Hatimaye nawashukuru Madiwani na siwezi kuzisahau Maskani zangu mbili, moja ya Kisonge na moja ya Kachorora, hii ndiyo ilikuwa uti wa mgongo nilioweza kupasua kifua au kichwa cha Mgana, mgombea mwenzangu. Mwisho, natoa shukrani za pekee kwa Mchawi wangu, Selemani Senga, aliyenihesabia kura wakati wa mizengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi vile vile kuwashukuru na kuwapongeza Mwenyekiti Mpya wa CCM, pamoja na safu yake mpya, akiwemo Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yusuf Makamba. Nasema hongera sana na kweli kiti kimepata mkaaji na tunasema ya kamba nyoka ni yule yule, lakini amejitoa ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ningeendelea kidogo niweze kuzungumzia yale machache, ambayo nimejaribu kuyatazama na kutokupoteza wakati, kuzungumzia juu ya yale ambayo wengine wameyazungumzia. Tokea siku ambayo Mheshimiwa Waziri Ngasongwa anatoa mipango yake na Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesoma bajeti yake, nikichanganya kwa sababu ndiyo nilipopata nafasi ya kuzungumza na Waziri Mkuu kutoa hotuba yake. Mimi nimejaribu kusoma kwa undani kabisa, kwa sababu ningali mpya, nimeona kuna kitu kimoja inabidi nizungumzie kwa makini sana, kwa sababu ni *sensitive issue*.

Katika mipango, kitabu hiki, Mheshimiwa Ngasongwa, sijamsikia amepanga nini kuhusu Muungano. Hotuba ya Waziri wa Fedha, kitabu hiki, nimekisoma chote mara mbili, sijamsikia isipokuwa ametaja tu vyombo vya Muungano. Lakini Muungano *per se* haujatajwa. Ninashukuru tu kwa Waziri Mkuu, kuna kipengele amekitaja cha Muungano na kulitaja neno Muungano *per se*. Sasa tukizungumzia Serikali mbili na tukizungumzia Muungano *per se* kama ni Muungano, hivi vitu mimi naviona viko tofauti. Haujazungumziwa Muungano, haujapangiwa Muungano; huu Muungano utakwenda namna gani? Hiki kitu ndiyo kitu nilichokuwa nimekaa nakifikiria, utakwenda vipi kama haujapangiwa au tunasitasita kuuzungumza?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha, ametaja kipengele kidogo sana tu cha mgawanyo wa fedha ule wa 4.5, ambazo ni karibu shilingi milioni 21.196,

kama nazikumbuka vizuri. Hapo ndiyo utakuta kidogo pamezungumzwa kitu, lakini kilichozungumzwa hiki sicho chenyewe hasa. Muungago wetu sasa hivi uko katika tabu sana na ninachotaka kusema ni kwamba, una upinzani. Una upinzani wa kina, umo nje ya nchi na ndani ya nchi. Sasa hivi tumefika mahali kiasi cha kuweza kuburuzwa au tumesikia kwamba, watu wanaupeleka Muungano Mahakamani. Sasa, nani ni *reponsible* wa kuweza kuukinga Muungano huu, ni sisi wenyewe. Tunafanya nini mpaka tunaukinga Muungano huu kama hatuupangii nini cha kufanya? Nini *vision* ya Muungano? Tumeanza huko nyuma na *Ministries* nne, sasa hivi tunakwenda na *items* karibu 22. Lakini, sasa *what is next*, hiki ndiyo kitu ambacho nimejaribu sana kupasua kichwa, sijakifahamu? Sijui tunakiogopa au tunaogopa kitu gani!

Mheshimiwa Spika, nataka kukuhakikishia ya kwamba, nimewahi kusema ya kwamba ni bora nife kwa kuukosa Muungano na nimeshapigana kwa ajili ya Muungano wetu. Sasa, ninaposikia kwamba, kuna watu wanauburuza Mahakamani Muungano, unataka kushtakiwa, mimi ninashangaa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najaribu kutoa rai katika kutaka kuyazungumza mambo ya Muungano, nilikuwa nahisi na ninaona ya kwamba, vyema ndani ya chama tukutane na tuweze kuzungumza *the way forward* ya Muungano. Kwa sababu nina hakika na ninasema nina hakika Vyama vya Upinzani, nao wakikaa huwa wanauzungumza Muungano huu na namna ya kuutegua. Sasa tunakwenda mpaka tunafika katika kero ya Muungano. Sidhani kama kuna mtu yeyote aliyetoka wakati wa Chama cha Tanganyika na Chama cha Afro Shiraz, mpaka sasa hivi tumekuwa watu wa CCM, anauzungumza vibaya Muungano, *unless upstairs is not alright*. Kwa hiyo, ninachojaribu kushauri ndani ya chama, tukae tuzungumzie Muungano, hiyo ndiyo itakuwa dawa. Bofu linapojaa, usingoje lipasuke, weka tundu ili u-*defuse* mambo utoe upepo. Kwa hiyo, yataendelea kuwepo mambo ndani na tunapata wakati wa kuzungumzia suala la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kushauri sana, suala la Muungano tujaribu kulipa kipaumbele. Rais wetu Kikwete, naona amejaribu sana kufikiria na akaona namna gani ataweza ku-*defuse* hii. Lakini siwezi kusema na siwezi kuona ya kwamba, kama Waziri Kiongozi, pamoja na Waziri Mkuu peke yao, watakaa chini wazungumze masuala ya Muungano, bila kutushirikisha sisi Wabunge na Wawakilishi ambao tunaweza kupokea kutoka kwa wananchi kero zile tunazozijua. Kwa hiyo, vikae vikao vya pamoja, Wabunge wa CCM, pamoja na Wawakilishi ili waweze kuzungumzia suala hili la Muungano.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimesitushwa na kubabaishwa sana kusikia kwamba, Bunge hili linatumia Lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza kabisa, Mwalimu alilihutubia Bunge hili nafikiri tarehe 12 Desemba 1963, mpaka leo tunasema ya kwamba, tunazungumza Kiswahili ndani ya Bunge, lakini Miswada inakuja kwa Kiingereza, halafu *Summary* yake inaandikwa kwa Kiswahili. *What are we doing? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki kitu kimenishangaza sana na mimi siwezi kushangaa kwa sababu hivi sasa ninavyozungumza, wananchi wanasikiliza Miswada ile ikisomwa,

inasomwa kizungu, sasa, wananchi kule wanafahamu kitu gani? Kwa ajili ya faida ya wengi na sisi tunaelewa ya kwamba, tuna wataalam wengi tu kabisa, kama labda Mawakili wanashindwa au Majaji wanashindwa, waende *University*, kuna chuo pale, kuna Walimu wamebobea, kuna Maprofesa pale, wajaribu kutafsiri. Bila kufanya hivyo, hatuwezi kufanya vitu vingine. Hili mimi ninaliomba lizingatiwe na katika Miswada yetu inayokuja, tujaribu kuiweka kwa Kiswahili, kwa sababu naweza nikasema bila kuona aibu ya kwamba, siyo wote humu ndani tunaweza tukaisoma lugha ile na tukaweza kuifahahamu. Lakini, ikiwa kwa Kiswahili na michango itabadilika itakuwa mingi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ninajaribu kutaka kuchangia tatizo moja lililokuwepo kwenye Majeshi yetu na hili linaniumiza kichwa kidogo. Nina hakika Waziri wa Fedha, anatoa fedha na kasma za Jeshi iko moja, *Vote* 38, nyingine *Vote* 39 kama sijakosea na *Vote* ya Wizara ni 59. Fedha zinatolewa za matumizi ya kawaida, tuseme chakula na mambo mengine. Lakini bado utakuta lile Jeshi kuna madeni. Haya madeni yanatoka wapi wakati wao wamepeleka kasma zile mbele na wamepewa fedha zinavyotakiwa? Hii inaleta bughudha wakati mwingine hasa inapofika wakati wa *ration*, ikiwa ni *ration* ya chakula ndani ya Jeshi. Inakuwa ni bughudha sana ukisikia wanajeshi wako wanakosa kitu fulani, kwa ajili ya upungufu wa fedha, lakini mie nasema siyo upungufu wa pesa, siyo kama pesa hazitoshi, isipokuwa tuwatazame watendaji.

Mheshimiwa Spika, nina Wazabuni hapa, hawa ni Wazabuni wa Zanzibari na karatasi hizi hapa ushahidi, wana jumla ya shilingi milioni 37 wanadai toka 1994. Maskini hawa wafanye nini? Wameona wamkimbilie Mbunge wao, wanasema wao wameshindwa. Sasa mimi ninachosema, kama hawa wanaonekana wezi, waburuzwe Mahakamani. Kama siyo wezi, basi wapewe haki yao! Hiki kimoja ndiyo nilichokuwa nakiomba. Kama ni wezi kwa sababu huwezi kusema ya kwamba, hawa watu ni wazuri, unakuja unawatetea hapa, halafu inakujulikana huko ni wezi wanapelekwa kwenye vyombo vya sheria. Lakini hawawezi kukaa tokea 1994 wanadai pesa na wao ni wafanyakazi au ni wafanyabiashara. Sasa watajikwamua namna gani? Kwa hiyo, suala hili, ninaomba lijaribu kutazamwa katika utendaji mzuri katika Majeshi yetu. Nina hakika pesa zinatolewa, lakini watendaji watazamwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka huko na ninaelewa huko, mimi nimejivua ile ngozi tu basi, lakini ni nyoka yule yule. Nikitakiwa tena, nafikiri naweza nikarudi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kengele isinigongee na mimi nijifanye mwenyeji ndani ya Bunge, ninasema ninaunga mkono hotuba hizi. Lakini kwa kipengele kile ambacho sijakiona sehemu zote isipokuwa kwa Waziri Mkuu, kipengele cha Muungano *per se,* naunga mkono kwa asilimia 99.998. Nashukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunivumilia na awali ya yote, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa karama zake, amenijalia nimesimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, mbele ya Waheshimiwa sana Wabunge wenzangu wa Bunge lako hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nisiache kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa kura nyingi sana. Katika hilo pia, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mheshimiwa Mzee Yusuf Makamba, Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kupewa nafasi nzito ndani ya Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama, amewapendekeza kutoka kwenye Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hiyo inaonyesha kwamba, ndani ya Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kuna hazina kubwa ya viongozi. Hivyo, napenda niwapongeze wao, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Edward Lowassa na wewe mwenyewe Spika wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa makadirio ya Ofisi yake na hotuba yake na pia niwapongeze Mheshimiwa Peter Pinda na Mzee wa Taratibu na Kanuni, Mheshimiwa Juma Akukweti, Mheshimiwa Celine Kombani na Mheshimiwa Siyame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ama kwa hakika pia kazi hii ambayo imewasilishwa kwetu ni kazi ya pamoja ya wafanyakazi wengi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ninaomba niwapongeze wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, nisiwasahau wananchi wa Mkuranga, walionichagua kwa kura nyingi. Ninawaahidi, *inshalah*, nitawatumikia kwa uwezo wangu na moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilikusudia kuchangia kwenye hoja ile ya Bajeti na Mpango wa Maendeleo, lakini Naibu Spika akaonya kwamba, wale watakaokuwa wamezungumza wiki iliyopita, hawatapa nafasi wiki hii. Sasa mimi mama yangu ni mtu wa Iringa na Naibu Spika, ni wakali sana nawafahamu. Akisema amesema, kwa hiyo, nikaona afadhali nitumie nafasi hii wiki hii, ile niiache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo naomba niwapongeze Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Watendaji wa Wizara zao, kwa kazi nzuri sana iliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niingie kwenye hoja. Wabunge wengi walionitangulia, wamechangia kwa mapana na kwa ufasaha mkubwa na wote tumeweka *reference* katika ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Hata Mbunge mmoja wa Upinzani, alikuwa anatafuta namna ya kutumia kauli mbiu hiyo, mwisho, akaishia kuitumia tu kwa sababu ana hakika kwamba, ndiyo njia sahihi ya awamu hii na mazingira ya kiuchumi na kijamii tuliyokuwa nayo. Sasa lakini hii ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ni nini; ni nani; ni lini; ni wapi na nini Ofisi ya Waziri Mkuu katika ari mpya na tafsiri nzima ya kiuchumi, kisiasa na kijamii? Kila mmoja wetu amesimama hapa, tumefanya *reference* katika kauli mbiu hiyo, lakini naomba niwahakikishie Wabunge kidhati kabisa, utekelezaji wa malengo haya ni kazi kubwa sana na ndiyo maana nikasema ni nani na ni nini? Kwa sababu ni nani, Waziri Mkuu anaposema ari mpya na

nguvu mpya au Rais anapolisema? Lazima sisi wote hapa tukubali kwamba, hiyo kazi kimsingi ni yetu wote, hakuna ambaye yuko *exempted* katika hilo. *(Makofi)*

Ili tupate utekelezaji wa uhakika katika hilo, basi lazima tukubali kwamba, kuna mambo ambayo tumekuwa tunayafanya *historically*, lazima tubadilike. Ari mpya, si kauli ya kuombea kura, ni wito wa kuwaambia Watanzania wote kwamba, sasa jamani tufunge mikanda, kazi inaanza.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kiuchumi ya kijamii ya Taifa hili, usimamizi wake sasa lazima tuanze kuutazama kama Menejimenti ya Kampuni binafsi. Nasema hivi kwa sababu, kimsingi hakuna maendeleo yanayokuja bila ya pesa, bila ya udhibiti wa mali, bila ya udhibiti wa rasilimali. Tuna kawaida ya kutazama fedha za umma kama fedha za mtu mwingine, tunasahau kwamba, sisi wenyewe ndiyo umma huo huo. Sasa tukilitazama hili kama Kampuni, basi tutasema Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ndiye Mwenyekiti wa Bodi, Mheshimiwa Edward Lowassa, ndiye Mkurugenzi Mtendaji, Mawaziri ndiyo Wakurugenzi wa Idara, halafu sisi wengine wote, tukawa wafanyakazi wa Kampuni hiyo, yaani wakulima, wafanyakazi na raia wengine.

Mheshimiwa Spika, nimeitambulisha Kampuni hii ambayo nimependa kuiita *Tanzania People's Development Company* ili niseme yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kusema kweli Tanzania haitafika popote mpaka tutambue kwamba kama ilivyo katika Kampuni ya mtu binafsi, hakuna mtu anayependa uharibifu wa mali, mipango mibovu, uwezekezaji mbovu na matumizi ya fedha yasiyokuwa na kichwa wala miguu. Sasa sisi humu Bungeni tunawaomba Watanzania wote, jamani ari mpya, uzalishaji; lakini tujiulize, je, tunawaandaa vya kutosha ili waweze kushiriki katika ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ili waweze kushiriki ipasavyo katika huu mtandao wa kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka kuhusu nia ya Watanzania wote walio nje ya nyumba hii kushiriki katika ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kwa sababu kwanza kabisa wana imani kubwa na Mwenyekiti wa Bodi, lakini pia wana imani kubwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo Mheshimiwa Edward Lowassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu kimsingi dakika 15 ni ndogo na mambo ya kusema ni mengi, naomba niseme yafuatayo: Mimi naomba nihimize Menejimenti ya Kampuni hii kwamba ari mpya na nguvu mpya inabidi ianze kwao, sisi tuwe tunafuatia nyuma, wao ndiyo wawe mfano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Naomba nitoe mifano katika sehemu tatu, Serikali za Mitaa, Kilimo na Miundombinu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika ukurasa wa 30 amezungumzia uboreshaji wa muundo wa Serikali za Mitaa katika kuboresha kitu kinaitwa Sekretarieti za Mikoa ili kiwe kinawajibika zaidi. Akaendelea kusema, tutaziimarisha Serikali za Mitaa ili ziwe vyombo shirikishi vya wananchi. Neno kubwa hapo ni "vyombo shirikishi vya wananchi, vinavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi

na uadilifu wa kiwango cha juu vinavyowajibika kikamilifu kwa wananchi wenyewe."

Mheshimiwa Waziri Mkuu akaendelea kusema kwamba: "Mikataba na matumizi ya mapato ya Halmashauri yanahitaji kusimamiwa kwa uadilifu mkubwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha." Baadaye akazungumzia mchango wa *Controller and Auditor General* na kimsingi, ameweka misingi mizuri mno ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali za Mitaa katika kuwajibika kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo, Waziri Mkuu, amezungumzia kwa uwazi kabisa, amesema kwamba tumejifunza kutokana na ukame uliotupata na kwamba sasa tunaandaa mazingira ya umwagiliaji maji, uvunaji wa maji ya mvua, mabwawa na kadhalika. Lakini naomba nirejee mchango wa Mheshimiwa Mbunge aliyenitangulia, aliyesema kwamba, katika hili lazima tujifunze kwa wenzetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie mfano wa miundombinu. Leo hii tulikuwa kwenye Kamati na tulikuwa tumezungumzia suala la ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Daraja la Kigamboni ni daraja lenye manufaa sana, tena sana kwa watu wa Mkuranga kwa sababu ya maendeleo yatakayotokana na daraja hilo. Kuna masuala ya *investment* itakayofanywa katika *satellite cities*, tutauza nyanya zetu, mchele na kadhalika kwa watu watakaohamia katika Kanda hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini daraja hilo limekwama kwa sababu wataalam baada ya kupokea maagizo ya Rais na ya Ilani, bado wanasubiri. Kwa kauli, nimesikia kwa masikio yangu kwamba Watalaam hawajaamua na kumshauri Waziri wa Miundombinu kuhusu mradi huo. Sasa hili ni agizo la Rais, ni agizo la Ilani ya Uchaguzi, watalaam wanalizuiaje?

Katika hilo, naomba niseme kwamba sisi Wazaramo tuna kauli moja, ukiishiwa halafu ukaanza kula kwa kaka yako, unakula siku ya kwanza, ya pili, ya tatu, wiki mbili, mtoto wa kaka yako akija akikwambia baba mdogo kama vile kaka yangu Vita mtoto wake akiniambia baba mdogo, hivi utaendelea kula hapa mpaka lini? Basi mimi sisemi yale maneno kasema yule mtoto, nitasema kasema Vita na mkewe. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nalisema hili kwa sababu watalaam hawana uwezo wala hawastahili kuyazuia yale ambayo Viongozi wetu Wakuu wameyatolea amri. Kwa hiyo, katika hilo nilitaka kusema kwamba hii Kampuni yetu ya *Tanzania People's Development Company* lazima tuhimize suala la nidhamu katika usimamizi wa fedha. Katika historia ya nchi yetu, kipindi cha mwaka 1983/1984 tulikuwa na vita dhidi ya wahujumu uchumi. Mwajiri wa Halmashauri ama wa Serikali anaanza kazi leo hata baiskeli hana. Baada ya miezi sita ana nyumba ana gari, huyo ni mhujumu uchumi, kazitoa wapi fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe kwamba mwaka 1984 kulikuwa na J. K. na Edward mmoja waliofanya kazi hii na mwaka 2006 tuna J.K. na Edward mwingine. Mimi nina imani kubwa kwamba watachukua mfano ule na watafanya kazi yao na hawatawaonea haya watu ambao wanaturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo yanasimamiwa juu lakini yanaelekezwa *(at base level)* pale chini kwa Watanzania wa kawaida, tusipofikia hatua ya wale wananchi wa kawaida kupendekezewa na kazi inayofanywa na Serikali yao na Bunge lao tutakuwa tunazunguka hapo, hapo na tutajikuta miaka kumi ya awamu ya nne imepita. Nasema miaka kumi kwa sababu nina uhakika *inshallah* mwaka 2010 tukiwa hai tutashinda tena. Nasema tutakuwa tunazunguka pale pale.

Kwa hiyo, naomba nimalize kwa kusema pia hii tabia ya kuwaondoa Watendaji kwenye Halmashauri moja, keshaharibu halafu tunampeleka Tandahimba au Namtumbo, sasa tunamwadhibu au tunamzawadia? Maana kule nako anakwenda kufanya uhalibifu mwingine.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa umefika wakati kwamba ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya haitakwenda isipokuwa tuwe tayari kuwakemea watu hata kama ni mkweo, lazima tuwe wakali. La sivyo, tutakuwa tunazunguka hapo, hapo. Hakuna uchumi duniani ambao umesimama bila watu kuwa wakali. Ni mfano wa Malaysia, Dr. Martin Mohamed amewafunga mpaka rafiki wa karibu kwa kuhujumu uchumi. Korea Kusini ni hivyo hivyo. Sasa mimi naamini kabisa kwamba, kama tukitaka kufikia maendeleo ya kweli na Tanzania tuna uwezo wa kufikia maendeleo ya kweli, tuwe wakali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kuna Mbunge mwenzangu alikuwa ananiambia, nchi za Kusini Msumbiji, Afrika Kusini,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupata taarifa kuhusu wageni, naona ni vizuri niwatambulishe. Kwenye *gallery* ya kushoto wapo viongozi wanawake 41 kutoka Vyama mbalimbali vya Siasa vya nchini kwetu, ambao wanahudhuria Semina, ni wageni kwa pamoja wa Waheshimiwa Anna Maulidah Komu wa Chadema na Mheshimiwa Monica Mbega wa CCM. Naomba akina mama msimame. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Nipongeze pia na Sekretarieti ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Rostam Azizi, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Ndugu Jaka Mwambi pamoja na Mheshimiwa Kidawa nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, nichukue nafasi hii ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo naweza kusema ni *self contained,* kwa maana kwamba imekamilika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitashukuru Bodi ya *ATEX* na *Quant Surveyors*, yaani Bodi ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majengo ambao waliendesha zoezi zima la kusaili Makampuni yaliyoleta michoro ya jengo hili. Ni kazi nzuri sana wamefanya, nawapongeza sana. Mimi kwa taarifa, nilikuwa Mwanasheria ya Bodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitaomba kwanza nigusie suala la ulinzi wa Taifa letu kwa ujumla. Suala la ulinzi tumelikabidhi kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano. Ni Serikali ambayo ina wajibu wa kulinda raia wake. Katika ulinzi, tumekuwa na Vyombo vya Polisi, tumekuwa na majeshi na hao ndio wamekabidhiwa jukumu la kulinda Taifa letu, wananchi pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka ya karibuni pametokea Makampuni mengi sana hasa katika Miji ya Dar es Salaam pamoja na Miji ya Arusha ambayo wamekabidhiwa shughuli za kulinda raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utakuta Makampuni haya yaliyo mengi yanazo silaha ya kisasa, yanafanya mazoezi ya nguvu sana kama ya Jeshi letu la Tanzania au la Polisi. Hawa watu wanazo radio, wanayo mawasiliano. Vile vile, haya Makampuni yanayo magari tena pengine mazuri kuliko magari ya Majeshi yetu sisi. Wanafanya shughuli za ulinzi wa raia wa Tanzania, lakini yakiwa ni Makampuni ya kigeni. Nadhani ufike wakati jambo hili tuliangalie kwa makini sana, kwa sababu itakuja kufika wakati tutajilaumu sana. Kama ni wawekezaji, basi wawe wawekezaji wa sehemu nyingine, lakini siyo katika suala la ulinzi wa nchi yetu pamoja na mali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imezungumzia sana kutoa ajira kwa vijana na hilo napenda kulipongeza na nashukuru sana. Sambamba na hilo, naomba nichangie kwenye ajira ya vyombo vyetu vya fedha, yaani hii Benki na hasa Benki ya Afrika Mashariki *(ADB)*. Juzi juzi, nilikuwa Uganda nikajaribu kudadisi ni watumishi wangapi ambao wanatoka Tanzania wako katika hiyo Benki ya *ADB* na hasa katika *level* ya *management.* Nilisikitika sana, nikagundua kwamba nchi yetu haiwakilishwi vizuri katika suala la *Senior Management* katika hiyo Benki.

Hali hii iliwahi kutokea Kenya hawakuwakilishwa kipindi fulani, walipiga kelele sana na baadaye hali ikarekebishwa. Nalisema hilo kwa sababu itakapokuja masuala ya uwekezaji (*investment), Senior Management* katika hiyo, ndiyo inayoamua masuala ya *investment*. Sasa tusipokuwa makini Tanzania tunaweza tukajikuta tunakuwa wasindikizaji katika Benki yetu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Aprili, 2006 kupitia Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, alitoa tamko la kuhusu mazingira na katika tamko lake yalikuwepo mambo mengi sana. Lakini mojawapo la muhimu ilikuwa ni kuwarudisha wafugaji waliotoka nchi za Rwanda na Uganda ambao wanafuga mifugo yao katika Wilaya ya Karagwe na Mikoa mingine ndani. Mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Karagwe, tunapongeza sana hatua ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, wananchi wa Karagwe hawaamini kwamba jambo hilo lingeweza kutokea, wanaona kama ni ndoto. Kwa kweli wananchi wa Karagwe wamefurahi mno. Naomba Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mkaze uzi msirudi nyuma. Tunaomba mpaka mfugo wa mwisho uondoke katika ardhi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi yetu hii tumepewa na Mwenyezi Mungu ni zawadi ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia na ni kwa manufaa yetu sisi pamoja na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, tusikubali katu katu kutishwa wala kubabaishwa na mtu yeyote ambaye anataka kuchezea ardhi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Hivi ninavyozungumza ni kwamba, zoezi liko linaendelea. Namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa *Col.* Enos Mfuru. Kazi hii anaifanya kazi vizuri sana. Nampongeza Mzee David Daudi, *DC* wangu wa Karagwe, kazi hiyo anaifanya vizuri na napongeza vile vile na wananchi wanavyotoa ushirikiano katika zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana na jambo la kusikitisha, ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, anisikilize kwa makini hapa. Ni kwamba wametokea baadhi ya Watendaji ambao wamepewa zoezi hili kurudisha mifugo hii kwenda nje ya Tanzania. Zoezi hili wamelitumia kwa maslahi yao binafsi, ni kwamba wanachokifanya kule badala ya kuondoa mifugo ya raia wa kigeni, wao wanakamata mifugo ya Raia wa Tanzania, wanahakikisha kwamba ile mifugo wakishaikamata wanawatoza hela nyingi sana kwa kisingizio kwamba waliikuta ile mifugo inazurura katika malisho yao ya siku zote.

Ninazo barua nyingi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuwa nakuandikia, nakuletea. Mmojawapo ni ndugu yangu Salvatory Karabamu ambaye alitozwa kiasi cha Sh. 3,900,000/=. Kuna mtu anatozwa mpaka Shilingi milioni 10, milioni 15. Sasa hawa watu badala ya kuwaondoa wafugaji haramu, wao sasa wameanza kuwanyanyasa wananchi wa Karagwe. Kusema kweli hii imechafua, imetia dosari na ni aibu sana kwa Serikali yetu na ni aibu kwa kazi nzuri sana ambayo inafanyika. Nitaomba sana Serikali inisaidie katika hili na fedha hizo zinapotolewa, nyingine zinatolewa risiti na nyingine hazitolewi risiti hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naipongeza Serikali kwa kugawa ardhi ya iliyokuwa *ranch* ya Kitengule ambayo iko katika Kata ya Kihanga katika Wilaya ya Karagwe kwa wafugaji katika *blocks* zao. Ninafahamu kwamba waombaji ni wengi sana, lakini waliopata ni wachache na hiyo Serikali naipongeza mno. *(Makofi)*

Lakini kwa bahati mbaya sehemu hizo ambazo zimegawiwa mtu ambaye amepewa ardhi kuna mashamba ya wananchi ambao walikuwa mle, kuna nyumba tayari zimeshajengwa humu siku nyingi, lakini vile vile kuna Shule za Msingi. Kuna Shule moja inaitwa Shule ya Msingi Mshabaigulu. Sasa hiyo Shule unakuta mtu amegawiwa kwamba hilo shamba analimiliki kuchunga mifugo yake pale. Naiomba Serikali iwe

makini na jambo hili watusaidie kulitatua kwa haraka sana kabla halijaleta madhara. Ninajua ninapozungumza hapa wananchi wa Kata hii ya Kihanga, hasa Kijiji cha Katandanda, Kijiji cha Mshabaigulu, Kijiji cha Kibwela najua huko wananiangalia kwenye luninga wakijua kwamba Serikali itawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ahadi za Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni Jimboni kwangu Karagwe. Nikisoma kitabu hiki, mwelekeo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na ahadi za Mgombea Urais wa CCM ukurasa wa 25 Mkoa wa Kagera umeonyesha kwamba kuna ahadi za Mgombea wa Urais wa CCM. Nitasoma kwa haraka haraka. Ya kwanza ni kujenga barabara za Bukoba – Biharamulo – Geita kwa Kiwango cha lami na kuhakikisha barabara ya Ngara – Kayanga – Karagwe – Kyaka inapitika kwa wakati wote. Hii nasema siyo sahihi. *(Makofi)*

Ninaomba sasa nizieleze ahadi za Mgombea wa Urais wa CCM - Mheshimiwa Kikwete, alizotoa pale Kayanga- Karagwe pamoja na Mji wa Nkwenda. Ahadi ya kwanza aliahidi kwamba atatupatia maji Mji wa Mrushaka pamoja na Kayanga; ya pili aliahidi kwamba tutapata umeme Kijiji cha Nyakasimbi, Kijiji cha Mji wa Nyashozi pamoja na Mji wa Ngwendo; ahadi ya tatu, Mheshimiwa Rais aliahidi akina mama na vijana kwamba watapata mikopo; ahadi ya nne, Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya Kyaka – Kayanga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Sasa nasikitika kwamba hayo yote ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi na juzi alipokuja kushukuru pale Bukoba Mjini alikumbushia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya Kayanga mpaka Kyaka yeye mwenyewe sasa humu ndani hayupo. Ninaomba sana kwa wale wanaohusika, nadhani hawapo, ninaomba sana kwa wale wanaohusika wayaweke vizuri na kama wamesahau nitawaletea mkanda wa video ili waweze kujikumbusha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la michezo, wenzangu wamezungumza sana lakini juzi nilifurahishwa nilipomwona Rais wetu ameingia uwanjani kushuhudia mechi ya *Moro United* pamoja na Ulinzi ya Uganda. Akashangilia lile goli lililofungwa na Julius Mrope lakini baadaye tulipokuja kufungwa goli la pili na la ushindi na wale wa Ulinzi wa Uganda, nilimwona Rais wetu jinsi alivyonyong’onyea. Nilitaka kusema kimoyomoyo kwamba hiyo ndiyo soka ya Tanzania. Sasa nataka niwaombe wale ambao wana jukumu la kuboresha michezo hapa nchini, tuanzie kwanza mashuleni. Vijana wadogo kuanzia miaka saba na kuendelea waanze kufundishwa michezo wawe wasichana, wawe wavulana, ninaomba waanzie huko. *(Makofi)*

Naomba sana Shule Maalum za Michezo zijengwe na vile vile ninaomba watalaam watafutwe wapelekwe nje wakasomee michezo. Vinginevyo, tutabaki kushabikia Ghana. Ghana imetoka, sasa sijui tunaelekea wapi! Baadaye utasikia Brazil, Brazil, ikitoka sijui Agentina au Italy! Kwa hiyo, naliomba sana hilo tusije tukaendelea kumsononesha Rais wetu ambaye ni mpenzi wa Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda bado ninao, naomba sasa nizungumzie suala la bei ya kahawa. Bei ya kahawa kule kwangu Karagwe sasa hivi kilo moja ni Sh. 400/=. Kuzalisha kilo moja ya kahawa inachukua karibu Sh.1,500/=. Sasa hii ni hesabu gani, anaingia gharama kubwa kuzalisha, lakini kuuza anapata kidogo? Kwa kweli wananchi wamekata tamaa sana. Sasa ninashauri kwamba kuna ushuru mbalimbali ambao unatozwa kwenye kahawa, kwa mfano ule ushuru wa Halmashauri asilimia tano, naomba sana Serikali iangalie aondoe na ule ushuru mwingine mwingi ambao unafanya mpaka mkulima anapata hela kidogo. Ninaomba uondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, ningetamani sana mkulima wa kahawa mwisho wa siku apate kuanzia asilimia 80 mpaka 90 na hapo ndio atakapoweza kuendeleza hilo shamba lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, ninayo mambo mengi sana ya kuzungumza, sitaki unipigie kengele ya pili, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja Hotuba ya Waziri Mkuu. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. SIJAPATA S. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa, natoa pongezi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupata kura nyingi za kishindo kule Chimwaga.

Nisiwe mnyimi wa fadhila, niwapongeze Wapigakura wangu wote wa Kigoma walioweza kunipa nafasi nikaja kuungana na Wabunge wenzangu katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, nisikusahau wewe mwenye viwango nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachangia moja kwa moja katika ukurasa wa 40 na 41. Naomba kunukuu moja ya ahadi kubwa za Chama cha Mapinduzi "Kushughulikia wananchi matatizo ya ajira hasa kwa vijana na wanawake na Serikali inasisitiza kuwa kujiajiri binafsi ndio yenye nafasi nyingi za ajira katika nchi yetu. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imetenga Shilingi milioni 500 kila Mkoa na fedha hizo zitatolewa kwa mmoja mmoja au kivikundi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Kigoma kuna tabaka za wanawake tatu. Tabaka la kwanza ni wale wanawake wanaokaa Mjini. Wale wanaokaa Mjini wana uwezo wa kujitafutia kipato chao kikubwa. Hao wanaweza wakakopeshwa mtu mmoja mmoja Sh. 500,000/= kwa sababu wana uwezo wa kupata Sh.5,000/= kila wiki. Tabaka la pili ni wale wanawake wanaoishi Mjini na Vijijini ambao kipato chao ni kidogo. Hao wanaweza wakakopeshwa Sh. 200,000/= kila mtu, kwa sababu wana uwezo wa kujitafutia kuanzia mwanzo wa wiki hadi mwisho wa wiki wakapata faida ya Sh.3,000/=.

Tabaka la tatu ni wale wanaoishi Vijijini ambao hawana chochote kabisa, kipato chao ni *zero.* Wanawake hao huamka asubuhi kwenda kutafuta chochote, labda kwenda kulima kwa mwenzake au kwenda kutafuta kuni, akishapata hizo kuni anakuja kuziuza anapata Sh. 500/=. Akipata hizo Sh. 500/= ananunua chakula cha watoto na ananunua

unga pamoja na mchicha, maana hela ya kununua dagaa au nyama, hana. Sasa nilikuwa naomba Serikali, hawa wanawake wenye kipato cha chini kabisa ambacho ni *zero*, iwaangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwa masikitiko makubwa, kuna wanawake ambao wanakaa kando kando ya reli ambao wanakaa Nguruka, Uvinza, Kazolamimba, wale akina mama huwa wanajifanyia biashara ndogo ndogo, wanakwenda kuwauzia abiria walioko kwenye treni. Lakini kunatokea mgambo wanaanza kuwapiga wanasema wasiuze biashara pale, wakati mwingine wanachukua zile biashara wanawamwagia hasa Kazolamimba wanawapiga halafu wanawaweka ndani. Baada ya kuwaweka ndani baada ya siku mbili wanawatoa, wanatoza Sh.4,000/=. Hizo Sh. 4,000/= hazina risiti. Nilikuwa naomba Serikali iweze kuliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Bibi Maendeleo na Afisa Maendeleo wasiwe ni watu wa kukaa Ofisini. Inatakiwa waende wakawaelekeze akina mama jinsi ya kukopa na kuweka, siyo wasubiri Wabunge wakati wa kwenda kwenye ziara ndiyo wanafuatana nao. Kazi yao ni ya kwenda Vijijini kuwafundisha akina mama hao *advantages* na *disadvantages* za mikopo.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia uzalishaji mali katika Mkoa wetu wa Kigoma. Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma ni Mkoa ambao uliepukana na balaa la njaa, kwa hiyo, wakati wa kilimo sasa unakaribia, mvua kule kwetu Kigoma huwa zinaanza kunyesha mwezi wa kumi na kuanzia sasa hivi tumebakiza miezi mitatu tu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, Serikali itupe pembejeo za kilimo na utalaam iwezekanavyo ili pembejeo hizo ziwafikie wananchi mapema ili wanawanchi waweze kuwa na uhakika wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuchangia katika eneo la walemavu, katika ukurasa wa 62. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza jinsi kundi hili litakavyoboreshwa mfano watapata fursa katika ajira na huduma za msingi kama vile elimu na afya. Lakini katika Mkoa wa Kigoma kuna Shule moja ambayo iko Kigoma Vijijini, inaitwa Uvinza. Shule hiyo ina watoto mchanganyiko, yaani kuna watoto wenye mtindio wa ubongo na watoto wasioona. Jumla yake watoto hao ni 75 na mikondo yao ni minne kuanzia Darasa la Kwanza mpaka Darasa la Nne. Kuna Mwalimu mmoja ndiye aliyechukua mafunzo ya kuwafundisha watoto hao.

Mheshimiwa Spika, watoto wako katika mazingira magumu, kwani hawana Walimu. Mwalimu wao ni mmoja tu, aliyesomea *physiology*. Hawana vifaa vya kusomea vinavyotosheleza. Uji na chakula wanavyovipata watoto hao ni shida tu. Serikali Kuu ndiyo inayotoa Shilingi laki tatu kila mwezi kuwapelekea wale watoto kwa ajili ya kuwalisha.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba watoto hao waweze kujengewa bweni la kukaa moja kwa moja wasiwe wanarudi majumbani. Nilikuwa naiomba Serikali kupunguza adha wanayoipata watoto hao ikiwa ni pamoja na kutembea mwendo mrefu

na hata wale watoto wanaoishi katika Vijiji vya jirani na wenyewe waweze kupata elimu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelekea kipengele cha afya. Katika utaratibu wa uagizaji dawa za Mikoa, Zahanati za Vijiji na Vituo vya Afya vimekuwa vikipata dawa za *Box* aina ya *Kit*. Ndani ya *Kit* hiyo, kuna aina nyingine ambazo hazitumiki na nyingine zinatumika. Wakati mwingine kunakuwa na mtaalam mmoja au wataalam wawili ambao hawajui *dygnosis* ya dawa nyingine.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali ianze mfumo wa *indents* kwa ile Mikoa ambayo bado haijaanza ili kuepuka uharibifu wa dawa ambazo mpaka sasa zimesha-*expire.* Zipo nyingi tu zimelundikana kwenye Vituo*. Indent* hii itakapoanzishwa katika Mikoa ambayo bado, inatakiwa Mganga aagize dawa kutokana na zile *top ten disease* alizonazo pale kwenye *area* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, samahani, naona nilighafilika kidogo ilikuwa ni Mheshimiwa Switi ndiyo anafuatia. Samahani sana. Nafasi itakayofuata itakuwa yako baada ya Mheshimiwa Switi.

**MHE. ELIATTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Natoa pongezi kwanza kwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake iliyokuwa na umakini wa hali ya juu.

Natoa pia pongezi kwa Serikali nzima kwa sababu imeweza kukubali na kuendesha Bajeti kwa mfumo wa jinsia, yaani Bajeti inaanza kupangwa chini na kwenda juu, *top and upward Budget* huku ikizingatia vipaumbele.

Bajeti hii tukiipamba na ufuatiliaji wa Wabunge na kurudisha utekelezaji wake hapa Bungeni, itaweza kutufikisha kwenye kitu kinaitwa maisha bora kwa Mtanzania. Ni taratibu hii ya maandalizi ya Bajeti imesababisha Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano kuunga mkono Bajeti na kuiona kwamba inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, sisi Watanzania tutaweza kufika mbali isivyopasa, kwa sababu tutakuwa tunakwenda kwa mtindo huo. Mimi nilikuwa nimepelekwa Kenya. Huko, Bajeti huandaliwa na Wizara, halafu inapelekwa tu kwa Wabunge kupitisha.

Mheshimiwa Spika, lakini nakushukuru wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipeleka huko nikajionee jinsi gani wenzetu wanadai kwamba walio juu wanaweza

wakaendelea kuifaidi nchi na wale maskini wakaendelea kupata shida. Nashukuru sana kwa hilo. Sasa napenda kuchangia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikipanga kuwa na Kamati mbalimbali kushughulikia nchi nzima, naomba Serikali itoe nafasi kubwa kwa Mikoa yenye kutoa chakula kuangalia masuala ya mazingira. Kwa sababu kama hawakufanya hivyo, itafikia mahali ambapo nchi hii tutakosa chakula. Yapo mapori makubwa huko Mkoa wa Rukwa ambayo yanaanza kutoweka, yapo mapori ya Mpanda Ndogo Wilaya ya Mpanda, mapori ya Sumbawanga Vijijini, Jimbo la Kalambo ambapo kuna Sokwe, nao wanaweza kutoweka. Naiomba Serikali iangalie mapori haya ili sokwe hawa wasije wakatoweka, waendelea kuwa ni faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia masuala ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Serikali imeonekana kujali sana maendeleo ya jinsia na watoto. Lakini suala hili bado linaleta utata kwa sababu wanawake wengi hufa na watoto pia hufa wakati mama hawa wakiwa wanajifungua. Katika kila watoto wanaozaliwa 1,000, watoto 58 hufa. Kati ya akina mama 10,000 wanaojifungua, akina mama 524 hufa. Jambo hili linatisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nizungumzia masuala ya mikopo ya wanawake. Naomba sana mikopo hii ielekezwe sana Vijijini kwa sababu wanawake wanaoishi Vijijini ni maskini sana na wala hawawezi kupata mikopo katika Mabenki kwa sababu hawana dhamana. Japokuwa sasa hivi Serikali imeshatunga Sera ambayo inawawezesha akina mama kuwa na ardhi, lakini bado utekelezaji wake siyo mzuri.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia suala la watoto. Kwa kweli watoto wanaoishi katika mazingira magumu na yatima wana hali mbaya. Naiomba Serikali ivitembelee Vituo hivi na kuona jinsi gani watoto hawa hawawezi kuhudumiwa vizuri kwa sababu fedha za kuendesha Vituo hazitoshi. Watoto wanaoishi katika mazingira magumu wamewekwa katika *Centers* mbalimbali, lakini matunzo yao si mazuri hata kidogo. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke mkazo kwenye vituo hivi na watoto wengine wote wanaozungukazunguka waweze kupewa elimu na waweze kupewa maisha mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa kiasi kikubwa haijapata Bajeti kubwa ya kuweza kuendesha Wizara. Najua fedha zetu ni finyu, Keki ya Taifa ni ndogo. Lakini ninaiomba Serikali iijali Wizara hii katika Bajeti ijayo ili iweze kuleta maendeleo ya wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Wilaya ambazo zilianza siku nyingi, lakini huduma zake za jamii ni duni. Kwa mfano, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini ina Zahanati za Serikali 83 na Vituo vya Afya saba. Lakini wana magari matatu tu kuweza kutoa huduma. Kwa hakika gari tatu haziwezi kuhudumia Wilaya nzima yenye Zahanati na *Dispensary* saba. Akina mama wengi wamepoteza maisha kwa sababu kila walipohitaji gari, gari haikupatikana, na hasa wale wanaopanda mlima kutoka Rukwa wengi wamefia pale mlimani.

Mheshimiwa Spika, akina mama wengi wa Sumbawanga Vijijini, pia wamekufa mara walipofika Hospitali kubwa ya Mkoa wa Sumbawanga kwa sababu hali ya barabara sio nzuri, ni nyembamba kabisa halafu sio nzuri. Kwa hiyo, kama ameshazidiwa akifika pale, anaishia pale pale. Wilaya ya Sumbawanga Vijijini haina Hospitali ya Mkoa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iruhusu kuwepo kwa Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Laela ni Kijiji kimoja ambacho kiko Sumbawanga Vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, keti chini, nadaiwa mwongozo.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni ya 49(3), mzungumzaji anasoma.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nasita kusimama, lakini sasa nadhani baada ya mwenzetu mmoja kudhihirisha hilo, napenda nimkumbushe aliyekuwa anachangia hoja hivi sasa, kwamba, Kanuni ya 49(3) inasema hivi: "Isipokuwa kama ameruhusiwa na Spika, Mbunge hatasoma hotuba yake."

Kwa hiyo, iko wazi kabisa. Mheshimiwa umeonekana kama vile unakwenda na kitu ulichokiandaa, unaendelea kukisoma. Hairuhusiwi na Kanuni. Kama kungekuwa na tatizo, ungekuwa umeniomba ruhusa, ndiyo ningekuruhusu usome. Lakini kwa kuwa wala hukuniomba, basi sikuruhusu kusoma. Kwa hiyo, changia hoja yako bila kusoma. Ila anaruhusiwa kusoma dondoo katika kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa kwa kujikumbusha. Tuendelee Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ELIATTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu watumishi wanaostaafu. Watumishi wengi huwa wanafanya kazi ya aina moja na bila kupanda vyeo kwa muda mrefu. Kwa hiyo, wanapostaafu huwa wanakuwa na kiasi kidogo tu cha fedha kiasi kwamba wanapopewa marupurupu huwa ni kidogo mno yasiyowawezesha kuanzisha miradi na kuweza kuishi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia *HIV/AIDS.* Ijapokuwa tumeambiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba milioni 2.5 ya waadhithirika ndiyo inaweza kuwa kiwango cha juu kabisa cha waathirika katika nchi hii, mimi nasema, waathirika hawa ni wengi kuliko hawa waliotajwa. Kwa sababu wale wanaokwenda kupimwa kwa hiari ni wachache na wako Mijini tu.

Lakini wale wanaokuwa Vijijini hawana hata habari na huduma hii. Lakini pia, *CD4 Machines* zinapatikana katika Hospitali kuu za Mikoa. Kwa hiyo, naomba Hospitali za Wilaya nazo zipatiwe *CD4 Machines.* Kwa sababu wanaoishi Vijijini wengine wanapewa tu dawa zile, sijui wanazipataje, wananunua mahali halafu wanakunywa bila kupimwa. Baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Subiri Mheshimiwa Mikidadi. Inanibidi nimkumbushe naye anayekufuatia ambaye ni Mheshimiwa Dunstan Mkapa, ajiandaye.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kukutana na Bunge hili Tukufu na wageni wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ambayo kwa kweli sio rahisi kuipata. Nashukuru kwa hilo. Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kutoa hongera na pongezi kubwa kwa Sekretarieti yetu mpya ya Chama Cha Mapinduzi, Uongozi mzima na Mwenyekiti. Hongera sana na mimi siko mbali na wenzangu kwa kushukuru jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amefanya mipango na *Cabineti* yake kutuwezesha wananchi wa Tanzania kupewa chakula cha njaa. Kwa kweli tunashukuru sana. *(Makofi)*

Vile vile, nichukue nafasi hii nishukuru kwa Bajeti hii na hotuba ya Waziri Mkuu, Bajeti na hotuba imelenga kabisa matakwa ya wananchi. Kwa kweli tunashukuru kwa sababu mengi yalioandikwa katika Bajeti hii yamegusa ahadi za Rais, yamegusa matakwa ya wananchi na yamegusa maslahi ya wananchi. Kwa kweli tunatoa pongezi sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuunga mkono Bajeti hii na hoja hii kabla sijapigiwa kengele. Nasema, kwa kweli naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa nasikiliza wenzangu wote ambao wamezungumza, Wilaya hadi Wilaya, Mkoa hadi Mkoa, wengi wamelalamika kuhusiana na matatizo mbalimbali yaliyopo katika maeneo yao ikiwemo maji, afya, kilimo na mengi mengineyo. Yameyataja mambo 20, maana nikiyataja hapa nitakosa nafasi ya kuzungumza. Nilikuwa nahesabu, wametaja matatizo 20 katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo ni mengi katika Mkoa wa Lindi na Mtwara. Nasema hivyo kwa sababu ni jirani, tunayo na nikiyataja hapa nitamaliza muda, lakini nimeyaandika kwa maandishi, nimekuletea. Kwa matatizo ya Mkoa wa Lindi, nafikiri tufanye kitu kimoja kama inawezekana, kwamba sasa Mheshimiwa Waziri na *Cabinet* yake na Watendaji tujipange upya. Kwa sababu watu tumeongezeka kama Wabunge wamefika 300 ina maana watoto wameongezeka na kwa hiyo wananchi wameongezeka. Kwa hiyo tunahitaji zaidi huduma zote mara mbili zaidi. Ndiyo malalamiko yanatokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba tujipange upya, *Cabinet* ijipange, Mawaziri wajipange upya, waende katika maeneo haya ambayo yanalalamikiwa, kulikoni? Kuna tatizo gani? Kisha warudi wapange mpango wa kazi, waangalie wapi kuna matatizo. Je, matatizo yaliyozungumziwa ni ya kweli? Mpango wa kazi unatakiwa upya. Baada ya mpango wa kazi, sasa waanze kutekeleza. Baada ya kutekeleza waanze kufuatilia, Watendaji wanafanya kazi? Baada ya kufuatilia, watathmini: Je, ule mpango umefanikiwa? Matatizo yanaendelea au yamepungua.? Hilo la kwanza kwamba tujipange upya tufanye kazi kwa kuandika mpango wa kazi. *(Makofi)*

Najua kutakuwa na mpango wa utekelezaji kwa sababu hauna pesa. Lakini tatizo la fedha litakuja tu, kwa sababu sisi hatuna viwanda, hatuna kile na hiki. Ningeshauri tukope, kwa sababu kukopa ni heshima. Katika nchi zilizoendelea, kukopa ni heshima. Unapokwenda kukopa, unaulizwa wewe ulikwishakukopa mahali? Kama hujawahi kukopa hawakukopeshi. Kwa sababu hawajui tabia yako.

Kwa hiyo, ninachoshauri hapa, ili masuala haya yaweze kutekelezeka, lazima tukope. Hakuna njia nyingine, kuna maeneo mengi tu ya kukopa. Kuna hawa wenzetu wa *HIPC* wanakopesha. Kuna *World Bank*, Benki nyingi tu. Kwa hiyo, tukope! Kukopa ni heshima, vinginevyo hatuwezi kutekeleza haya yote ambayo Wabunge wamelalamika. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili niende moja kwa moja katika suala la mahusiano na nchi za nje ukurasa wa 59-60 wa kitabu hiki ambako kuna hoja ya Waziri Mkuu. Tanzania tumebahatika kuwa na Jumuiya mbalimbali. Kuna Jumuiya ya Afrika Mashiriki, kuna *SADC*, Jumuiya ya Maendeleo ya Baraza la Usalama wa Taifa, Jumuiya ya Wanawake na kadhalika na nchi jirani yaani rafiki. Sasa mimi nina wasiwasi na kitu kimoja. Wanapokwenda kwenye Mikutano kukutana na nchi hizo za Jumuiya, maazimio yanayotolewa pale yanafanyiwa kazi? Yanatekelezwa? Yanaletwa kwenye Bunge ili na sisi tuyafuatilie? Mimi nina wasiwasi sana kwa sababu kulikuwa na azimio moja la Mkutano wa *SADC* ambao ulifanyika huko nchi moja kati ya nchi zile za *SADC*. Nchi za *SADC* mojawapo ni Tanzania, Mozambique, Zambia na Malawi.

Azimio hilo kati ya maazimio yote yamegusa nchi zao pamoja na Tanzania. Katika Tanzania, Mikoa ambayo iliguswa ni Rukwa, Lindi, Mtwara, Iringa, Pwani, Morogoro, Mbeya na Ruvuma. Hiyo Mikoa iliguswa kwa sababu ni Mikoa ambayo iko nyuma. Sasa hivi ina jina inaitwa Mikoa maskini au Mikoa iliyokuwa pembezoni. Tanzania iligusa Mikoa hiyo kwa makusudi kabisa. Katika mazungumzo yao wakasema kwamba lazima tufanye kitu fulani katika Mikoa hii ili kuiendeleza katika Mkutano huo wa *SADC*. Mwaka 2004 nchi hizi za *SADC* ziliweka saini ili mambo hayo 16 yaliyoainishwa yatekelezwe ili Mikoa hii kuinusuru. Mambo haya 16 yangetekelezwa hapa, leo hakungekuwa na malalamiko, kwangu pakavu nitilie mchuzi tule; hapa sina kile; sina hiki! Hakungekuwa na malalamiko. *(Makofi)*

Mikoa hii yote hapa imetoa matatizo, imelalamika, lakini sababu mojawapo ni kwamba maazimio ambayo yametolewa mengine hayatekelezwi. Hayafanyiwi kazi! Ningetaka kusema baadhi ya maazimio. Samahani. Baadhi ya maazimio, kwanza kuendeleza barabara. Naomba ninukuu: Maazimio hayo yalikuwa kama hivi: “Kuendeleza barabara toka Manda hadi Mchuchuma *Project* kwa ajili ya kusafirisha umeme kutoka *Mchuchuma Village* na kuunganisha umeme wa gridi ili utumike katika machimbo ya *Lake Victoria* na Mikoa ya *Mtwara Corridor* kwa maana ya Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Morogoro na Pwani.” Je, imefanyika? *(Makofi)*

Si hiyo tu, kuendeleza Bandari ya Mtwara, Manda, Mbambabay, Lindi, Kilwa na Bandari kadhaa muhimu katika *Mtwara Corridor.* Sio hilo tu, lingine kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Songea na Njombe; Barabara ya Mchuchuma hadi

Mlimba; Daraja la Umoja wa Tanzania na Mozambique; Barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi - Mtwara hadi Mbambabay; Barabara ya Mbambabay hadi Mtwara na Reli yake; Reli ya Mtwara - Songea - Manda, Reli ya Manda - Mchuchuma -Mlimba; Kupatikana kwa maji safi kwa Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro na Pwani. Aidha, mawasiliano ya Mikoa ya *Mtwara Corridor* yoyote ile; Reli ya Tunduma - Sumbawanga - Kasanga na kuboresha barabara ya gari. Mwisho, mradi wa gesi ya Mnazibay/Mtwara/Kilwa Songo Songo na miradi mingine nimeiacha, nimesoma tu haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama miradi hii ingetekelezwa, hakungekuwa na malalamiko hapa kwa sababu hizi zote ni njia za mawasiliano, maji na kadhalika, kwani Waheshimiwa Wabunge hapa hasa wa Ruvuma amelalamikia tatizo la maji. Sasa mimi naomba sana tusaidie utekelezaji wa maazimio mbalimbali yanayofanywa na Jumuiya zetu za nchi za nje kwa sababu wao wanaweka maazimio haya kwa makusudi kabisa ili kuendeleza Mikoa hii. *(Makofi)*

Sasa hivi katika Mikoa ile yote ambayo imetajwa katika *Mtwara Corridor*, maskini sana ni Lindi na Mtwara. Afadhali wengine. Sasa nisingependa kutaja matatizo yote ambayo yapo lakini, Mawaziri wanafahamu. Waziri Mkuu anafahamu, alikuja mpaka Ruangwa, Lindi akaona matatizo tuliyokuwanayo sisi Wilayani Ruangwa. Kwa hiyo, ningeomba sana tusaidie Mikoa maskini, tusaidiwe Mikoa ya pembezoni, tusaidiwe mikoa hii ya *Mtwara Corridor* kwa sababu wana matatizo.

Tunaomba sana tusaidiwe na mimi nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais amegundua suala hili na ndiyo maana akasema kwamba Mikoa ya pembezoni isaidiwe. Kwa sababu sisi hatukuwa maskini kwa kutaka, tulikuwa maskini kwa sababu maalum. Hii Mikoa sasa inaitwa Mikoa ya pembezoni. Kwanza, kulikuwa na mawasiliano duni kutoka Kusini kwenda Mikoa mingine kwa sababu kulikuwa na mlima mkubwa unaitwa Likumburu. Halafu kulikuwa na Mto Rufiji, watu wanashindwa kuvuka kuja kwetu, wanasema kule kuna mashetani, wanakula watu, mwisho Rufiji. Watu hawaji.

Kwa hiyo, kutokana Mto Rufiji na milima ile mikubwa watu walishindwa kuja Kusini kufanya mawasiliano, kufanya biashara na kadhalika. Tukabaki nyuma hatujui wenzetu wanafanya nini. Pili, ilikuwa ni vita vya ukombozi. Mikoa hii ilitumika kwa ajili ya kuwalinda wenzetu duniani. Kulikuwa na vita Afrika Kusini, Mozambique na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa fursa hii uliyonipa ili niweze na mimi kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, ningependa nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM Tanzania. *(Makofi)*

Pia, ningependa niwapongeze Watendaji Wakuu wote wa CCM ambao wameteuliwa naye kuongoza CCM, niseme Sekretarieti nzima yote. Halafu ningependa nimpongeze Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuachia ngazi zote mbili kwa ushujaa na heshima zote bila kutetereka. *(Makofi)*

Napenda pia nikipongeze Chama, Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Masasi na Wapigakura wa Wilaya ya Nanyumbu kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni na kuwawakilisha ili tuweze kupata maendeleo katika Wilaya yetu ya Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo kama kweli Watendaji wake wakuu watafuatilia maelekezo yote yaliyomo humo, basi hapana shaka yoyote nchi yetu itapiga hatua kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuwapongeza Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Masasi na Kambi yake yote ya Madiwani, pamoja na Watendaji wa Kata na Watendaji ya Vijiji kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kwa ugawaji mzuri wa chakula cha msaada. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri na tunaishukuru Serikali kwa msaada huo wa chakula. *(Makofi)*

Pia niwapongeze Kampuni ya Safari ya Miombo ya Uwindaji Miombo kwa kupunguza makali ya njaa katika Wilaya yangu ya Nanyumbu. Lakini kama nilivyosema katika swali langu la nyongeza, nilipouliza Wizara ya Maliasili na Utalii, ndovu walishambulia sana mashamba ya wanakijiji kule Nanyumbu. Kwa hiyo, namtahadharisha Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba njaa bado itakuwepo, watu mashamba yao yameharibiwa, hawana chakula, watahitaji bado msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu, amesema kwamba, lengo kubwa la Serikali ni kuwawezesha wananchi kubadili maisha yao yawe bora zaidi. Mimi Wilayani kwangu akina mama wako hoi sana. Akina mama ni jamii moja ambayo ni maskini sana, hawajui haki zao, wanakuwa kama yatima, hawajui hii mikopo inapatikana wapi. Ukiwaambia suala la mikopo, wanaachama midomo wazi na wanakushangaa. Hawajui! Haijawafikia hata kidogo! Kwa hiyo, naomba huu mgao wa Shilingi milioni 500 wa kila Mkoa utufikie Wilayani Nanyumbu ili wanawake wale waweze kujikomboa umaskini. Kwa kweli ni maskini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie suala la miundombinu, Wabunge wenzangu wamezungumza sana kuhusu barabara ya Dar es Salaam, Kibiti, Lindi hadi Mnanzi Mmoja. Lakini kwa sababu na mimi navaa kiatu hicho hicho, sina budi na mimi nizungumzie hii barabara. Barabara hii kwa kweli imezungumzwa sana tangu awamu ya kwanza hadi hivi sasa awamu ya nne.

Kwa kweli sasa tunaomba Serikali ione kwamba sasa hivi imetosha. Tunaomba sana barabara hii imalizike katika muda uliopangwa. Mkitaka kuona Maktaba ya magari mabovu na ya zamani, basi kasimame barabara kati ya Dar es Salaam, Lindi mpaka Mnazi Mmoja. Kule ndiko utakuta magari ya zamani, yale Albion. Sijui magari yale mengine ya zamani kule ndiko yanakopelekwa! Mtu ameshatengeneza huko hela yake

nzuri, basi ikiwa mbovu mbovu anaipeleka kule. Sio kwamba natania, nilitaka ndoa yangu na mke wangu iishe, kwanza tulikwenda kwake, yeye ni mtu wa Songea, lami mpaka kwake. *(Makofi)*

Ikaja zamu yangu sasa. Nilikuwa nampiga chenga. Ananiambia twende kwako, namwambia ngoja, subiri. Lakini ikafika wakati uwongo ukaniishia. Mimi nilivyovaa akanishangaa. Vipi? Mbona umevaa hivyo? Nikamwambia wewe huko tunakokwenda utaona mwenyewe. Yeye akajitia na vipondozi, viatu vya mchuchumio, nikamwambia utafika? Tumefika katika barabara ya Mavuji, mvua kubwa ikaanza, ndani ya gari inanyesha, na nje inanyesha. *(Kicheko)*

Sasa ananiuliza, sasa tufanyeje? Nikamwambia, haya si unaona vipodozi vinaanza kung'oka! Hivyo, mpaka ndani ya gari inanyesha! Magari mabovu yanapelekwa kwenye barabara mbovu. Tutoke nje tukasukume gari, mwenzangu ana viatu vya mchuchumio. Nikamwambia vua. Akashika mkononi, baadaye nikamtania viatu vinavaliwa mkononi bwana! Kwa kweli, hali ni mbaya sana. Tumenuniana pale, akaniambia kumbe kwenu kubaya hivi! Nikamwambia ulinipendea nini! Hali ni mbaya sana! Hali ni mbaya kweli kweli! *(Kicheko)*

Tunaomba sana Serikai isikilize kilio chetu watu wa Kusini, barabara ile iishe. Lakini mimi labda niulize, Ofisi ya Waziri Mkuu mtuambie kipande kati ya Nyamwage mpaka Somanga ambacho mpaka hivi sasa hakijaguswa, sijui Mkandarasi wake ni nani na kitaanza lini kutengenezwa? Hilo kwa kweli ningependa nipate majibu kutoka kwa Waziri Mkuu.

Mhesimiwa Spika, kuna huu mradi wa Mtwara *Corridor*. Wakati wa kampeni kuelekea Uchaguzi Mkuu ulikuwa ndio wimbo wetu, Mtwara *Corridor,* Mtwara *Corridor!* Lakini mpaka hivi sasa hakuna dalili zozote za kuanzishwa kwa barabara hiyo inayotoka Mtwara, Masasi, hadi Tunduru. Labda tungependa kupata maelezo, tujue barabara ile itaanza lini.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo sana Wilaya ya Nanyumbu. Kama alivyosema mwenzangu mmoja, akina mama wanaamka asubuhi sana, Alfajiri, wanakwenda kutafuta ndoo moja tu ya maji. Kwa kweli tatizo kubwa la maji Wilaya ya Nanyumbu limekithiri maeneo kama Sengenya, Maratani, Mkohora, Shigweje kule, sehemu kama Michiga, Mikokona, Mkangaula na kwingineko. Hali ya maji ni ngumu sana! Usisahau kwamba *DC* karibu atapatikana pale Mangaka na kuna shida kubwa sana ya maji,. Sasa sijui utampigia simu! Kama simu yenyewe ipo, basi mtafika huko kwenye simu mtaambiwa labda kaenda kutafuta maji huyo *DC*.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutupatia Nanyumbu Wilaya mpya na ninategemea karibuni uteuzi wa *DC* utaanza. Lakini *DC* yule atakuja hakuna mawasiliano yoyote, hakuna simu, hakuna *radio call* wala hakuna umeme. Ukitaka kupiga simu, kuna sehemu unakwenda unapanda juu mti ndio unaongea. Sasa usije ukaona kwamba *DC* anafuatana na mhudumu wake anatafuta ule mti naye akapende apige simu kwa Waziri Mkuu. Ataongea na wewe akiwa juu ya mti chini yuko mhudumu

na mafaili, ili limekwisha, lete faili fulani, atampelekea huko juu. Akifurahishwa akaachia lile tawi, ataanguka chini. Sasa tunaomba huduma za jamii kama simu, umeme, maji vipelekwe haraka sana Wilayani Nanyumbu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la Afya. Tuna Vituo vya Afya ambavyo kwanza tunaishukuru sana Serikali imetujengea lakini hadi hivi sasa watumishi ni wachache sana. Vituo hivi vya Afya viko pale Michiga lakini hakuna watumishi. Kuna Kituo cha Afya pale Nanyumbu hakina watumishi, kuna Kituo cha Afya Mangaka, watumishi hawatoshi. Sasa hii huwafanya watu wengi wafariki kwa kukosa huduma bora. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atasidie kwa hilo kutuletea Watumishi wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, wenzangu wengi wamezungumza uhaba wa Walimu, lakini ukizungumza uhaba wa Walimu kwa Wilaya yangu ya Nanyumbu, ni kubwa sana, iko mpakani kule, ilikuwa ndio uwanja wa mapambano ya vita. Ukiwapeleka kule Walimu, hawaendi. Shule zinakosa Walimu, watoto wanakuwa mbu mbu mbu, mtoto anamaliza Darasa la Saba hajui kusoma wala kuandika. Tafadhali sana, kama Waziri wa Elimu na Ufundi yupo, naomba unisikilizie kilio hiki. Naona unanipungia mkono kuashiria kwamba umekubali ombi langu. Ahsante. *(Makofi)*

Ajira, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi kule ajira ni kama ndoto. Labda niseme tu kwamba sisi ni wakulima wazuri wa korosho. Sasa tunaomba Wizara inayohusika mtuletee mashine ndogo ndogo za kubangulia korosho, basi vijana wetu angalau wapate ajira waache kuja huku Dar es Salaam kuwa wamachinga wakati kuna ajira kule majumbani kwao. Nafikiria ombi hilo limefika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautuwezeshi kuendelea kusikiliza wachangiaji katika hoja hii. Ninayo matangazo machache. Nakumbusha tena kwamba kuanzia leo umeanzishwa utaratibu wa kuhamia au kuhamishia nyaraka katika vijisanduku vilivyoko katika jengo hili jipya, badala ya kutumia vijisanduku au *pigeon holes* za kule sebule ya zamani kule, sasa visanduku vya hapa vina funguo, unaweza kufunga. Tatizo Waheshimiwa ni kwamba, mnaweza mkasahau funguo zenu au mbaya zaidi ukaipoteza. Kwa taarifa yenu tu, ukipoteza ufunguo, ili upate mwingine, maana yake tuna uwezo wa kufyatua hata ufunguo. Kwa hiyo, ili upate mwingine itabidi ulipie. *(Makofi)*

Tusipofanya hivyo, itabidi tuanzishe Idara Ndogo ya Kufyatulia funguo tu, kitu ambacho kitakuwa hakina maana na ndio itakuwa ubadhirifu huo. Kwa hiyo, nawakumbusha hilo. Tunahamia kwenye *pigeon holes* na majina yenu na ni salama zaidi.

La pili, kwa wenzetu waumini wa dini ya Kiislamu, kile Chumba mahsusi kwa ajili ya swala, kinakamilika kesho asubuhi. Kwa hiyo, mkiwaomba vijana wetu hawa wanaotuhudumia na vikaratasi, *page boys* na *page girls* watakuonyesheni. Kwa hapa

nilipo ni kushuka ngazi chini upande wa kulia huku na kimeandaliwa vizuri na kinafaa kabisa. Nimepata watu ambao wanajua mambo haya na wamethibitisha kwamba hivyo kilivyo kinafaa. *(Makofi)*

La tatu, nikiboresha tangazo langu kuhusu hivi vitabu, wengine waliniuliza wakati tulipositisha shughuli mchana kwamba, labda itakuwa ni adha kubwa kutembea na vitabu vyote hivi vitatu. Mimi nasema ukivileta kesho na kwa sababu Kamati ya Matumizi sasa ndio itakuwa ndio mwenendo hadi mwezi wa nane, ipo nafasi hapa hapa katika meza hizi, ukishakuja navyo kesho, sio mzigo tena, unaviacha hapa hapa na vinakuwa rejea kwa shughuli zinazokuja.

Mwisho kabisa, leo ni siku ya Taifa la Canada, Taifa rafiki ambalo limekuwa na uhusiano mzuri sana na nchi yetu kwa miaka mingi sana. Nakuombeni Waheshimiwa Wabunge mara linapoahirishwa Bunge jioni hii, basi tusogee katika sehemu yetu ya hafla ili tuweze kuwaunga mkono wananchi wa Canada wakiongozwa na Balozi wao kushereheka nao kwa siku hii ya Taifa la Canada. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na yote, nimepokea taarifa chini ya Kanuni ya 21(9), taarifa ya Mheshimiwa Mbunge mwenzetu ambaye anataka kutoa maelezo binafsi. Sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu, naruhusu, ila tu namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala ya Bunge - Mheshimiwa Juma Akukweti, chini ya Kanuni hiyo hiyo 21(6) aweze kutoa Hoja ya Kuahirisha Bunge, halafu tutatoa nafasi kwa Mheshimiwa Malangalila kutoa maelezo yake binafsi.

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Kwa mujibu wa Kanuni Na. 21(6) naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liahirishwe sasa dakika mbili kabla ya muda, ili likutane kesho.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ingawa hoja hiyo imekwisha ungwa mkono lakini nitawaomba muamue baada ya kuwa tumesikiliza maelezo binafsi. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Malangalila aweze kutoa maelezo yake chini ya Kanuni ya 21(9)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kufuatana na Kanuni za Bunge kifungu cha 40 niweze kutoa maelezo yangu binafsi. Juzi tarehe 27 Juni, 2006, nilipokuwa nachangia hotuba ya Waziri Mkuu,

pamoja na mambo yote niliyosema, nilizungumzia pia kuhusu hali ya Kiwanda cha Mufindi *Pap Mill*, *MPM* nilisema, ninanukuu:

"Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposikia mwekezaji amefika nikafurahi. Sasa mwekezaji mwenyewe huyu, ameanza mambo ambayo mimi nimeshindwa kuyaelewa na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini tumeshindwa kuelewa na naamini kabisa na ninyi mtakaposikia hapa hamtamwelewa. Mwekezaji huyu ana *General Manager* wake anaitwa Shodri, ni Mhindi. Anatupa ovyo madawa makali ambapo kuna mto mkubwa sana unaopita kwenda Kilombero na Rufiji. Wakati wa mvua yale madawa yanavuja na kuingia mtoni.

Sasa ndugu zangu wa Kilombero na Rufiji nawapeni pole tena sana. Amekuwa akishauriwa kuwa, pale zamani kulikuwa na *treatment plan* ambapo haya madawa ya sumu kutoka kiwandani yalikuwa yanasafishwa ili yasilete madhara kwa wananchi, haelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia ambalo nimezungumzia hapa, huyu Mhindi ni mbaguzi. Kwa sababu gani nasema ni mbaguzi? Akishauriwa na watu weusi anawaita mbwa, halafu akishauriwa zaidi, anasema mimi Serikali yenu hainifanyi chochote kwa sababu Viongozi wote wa Serikali wako mikononi mwangu. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, uko mikononi mwa huyo Mhindi. Nampa pole Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa mimi nimependekeza iundwe Tume." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Aliyekuwa Mwenyekiti wa Kikao alinitaka nifute usemi wangu wa kuwa Serikali ya Waziri Mkuu iko mikononi mwa Mhindi au nithibitishe tuhuma hiyo na nikapewa muda wa siku saba kutoa uthibitisho. Mimi nilitamka kuwa nafuta kauli hiyo wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 50, Mbunge akifuta kauli yake inakuwa ameondoa maneno hayo kabisa. Napenda kueleza Umma wa Tanzania na Waandishi wa Habari kuwa, kauli yangu ya kwamba Serikali pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa wamewekwa mikononi mwa Mhindi wa Mufindi *Pap Mill,* niliifuta na sasa narudia kusema kwamba maneno hayo nimeyafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumwomba radhi Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Malangalila. Huo ndio ukomavu wa kisiasa na wala sio udhaifu. Unapoona jambo limekaa vibaya, basi tunarekebisha tunakwenda mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, wachangiaji wa kesho wamebaki wanne na wote watapata nafasi ya kuchangia, kwa sababu asubuhi nilisema wasingeweza kufikiwa lakini kwa matukio mbalimbali imewezekana. Nawataja sasa ili wajiandae kesho kuchangia. Wa kwanza kesho atakuwa Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage - Viti Maalum *(CUF)* Kagera, Mheshimiwa John Shibuda (CCM) - Mbunge wa Maswa,

Mheshimiwa Laus Mhina (CCM) - Mbunge wa Korongwe Vijijini na atakayefunga uchangiaji ni Mheshimiwa Ramadhani Maneno (CCM) - Mbunge wa Chalinze.

Sasa tulikuwa na hoja mbele yetu ya kuahirisha Bunge Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo iliungwa mkono. Naona walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho asubuhi saa tatu.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 01.48 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 30 Juni, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*